**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# WIZARA YA AFYA

# HOTUBA YA WAZIRI WA AFYA, MHE. JENISTA J. MHAGAMA (MB.) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA AFYA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/26



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa ameshika Tuzo Maalumu ya The Global Goalkeeper Award' aliyotunukiwa na Taasisi ya Gates Foundations ya Marekani Februari 4. 2025 Jijini Dar es Salaam.*

**Juni, 2025** **Dodoma**




*Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akipata maelezo kutoka kwa watumishiwa Bohari ya Dawa (MSD) katika ufunguzi wa kongamano la Kisayansi na mkutano wa 54 wa Chama cha Wafamasia Tanzania Desemba 4, 2024 Jijini Dodoma.*




*Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto Biteko akipokea tuzo kwa niaba ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kutoka kwa Waziri wa Afya Mhe. Jenister Mhagama iliyotolewa wakati wa kongamano la 37 la Kisayansi la Wataalam wa Maabara za Afya kutambua mchango wake katika sekta ya afya Oktoba 2, 2024 jijini Dodoma.*



*Waziri wa Afya Mhe. Jenista Mhagama na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Dkt. Tedros Ghebreyesus wakiwa wamembeba mtoto walipofanya ziara kwenye Kituo cha Afya Makole Januari 20, 2025 kwa lengo la kujionea hali ya utoaji huduma katika kituo hicho.*




*Waziri wa Afya Mhe. Jenista Mhagama akizindua huduma za dharura kwa watu maalum katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Arusha, Mount Meru Januari 10, 2025. Uongozi wa Hospitali hiyo unaendelea kuboresha huduma ikiwemo za kibingwa ili kuvutia zaidi huduma za tiba utalii.*



*Naibu Waziri wa Afya Mhe. Dkt Godwin Mollel akiwajua hali baadhi ya wananchi waliofika kupata huduma za matibabu kwenye kambi ya huduma za mkoba za kliniki na matibabu ya magonjwa ya moyo ilioratibiwa na Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, Julai Mosi, 2024, Jijini Arusha.*




*Menejimenti ya Wizara ya Afya ikiwa katika moja ya vikao vyake vya kawaida kujadili utekelezaji wa vipaumbele vya Wizara katika kuhakikisha nchi inakuwa na jamii yenye afya bora na ustawi ambayo itachangia kikamilifu katika maendeleo binafsi na ya nchi.*

## YALIYOMO

**SEHEMU YA I:**
UTANGULIZI ........................................................1

**SEHEMU YA II:**
MAMBO MAKUBWA YALIYOTEKELEZWA NA SERIKALI YA AWAMU YA SITA KATIKA SEKTA YA AFYA KUANZIA MWAKA 2021 HADI 2025 ..............9

**SEHEMU YA III:**
MWENENDO WA UTEKELEZAJI WA BAJETI KATIKA KIPINDI CHA JULAI 2024 HADI MACHI 2025 ........................................................29

**SEHEMU YA IV:**
UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA 2024/25. ..................................................33

Huduma za Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto............33
Udhibiti wa Magonjwa Yasiyoambukiza ..................42
Huduma za Tiba ..................................................53
Mapambano Dhidi ya Magonjwa ya Kuambukiza .106
Magonjwa ya Milipuko na Huduma za Afya Mipakani ........................................................116
UTOAJI WA HUDUMA ZA KINGA.........................121
Huduma za Dawa, Vifaa, Vifaa Tiba na Vitendanishi ....................................................134
Huduma za Uchunguzi wa Magonjwa...................138
Huduma za Uuguzi na Ukunga.............................144
Uhakiki Ubora wa Huduma za Afya .......................147
Rasilimali Watu Katika Sekta ya Afya ...................150
Matumizi ya TEHAMA............................................156
Ufuatiliaji na Tathmini ..........................................157

Ugharamiaji wa Huduma za Afya..........................159
Miradi ya Maendeleo ............................................161
Utekelezaji wa Majukumu ya Taasisi zilizo Chini ya Wizara.........................................................................163
Utekelezaji wa Majukumu ya Bodi za Usajili na Mabaraza ya Kitaaluma ........................................191
**SEHEMU YA V:**
VIPAUMBELE VYA WIZARA YA AFYA NA BAJETI YA MAPATO, MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/26. ..........................................................207
**SEHEMU YA VI:**
MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2025/26…………………………………………….223

# HOTUBA YA WAZIRI WA AFYA MHE. JENISTA J. MHAGAMA (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA AFYA KWA MWAKA 2025/2026

## SEHEMU YA I: UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** leo hii baada ya kupokea taarifa iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI ambayo imepitia na kuchambua kwa kina bajeti ya Wizara ya Afya, naomba kwa mujibu wa **Vifungu namba 118 hadi 123 vya Kanuni za kudumu za Bunge toleo la mwaka 2023**, kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2024/25 na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2025/26.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kuwasilisha hotuba yangu siku ya leo. Aidha, kipekee naomba kuchukua fursa hii kumshukuru kwa dhati, **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan** kwa Imani yake kwangu na kuniteua kusimamia Wizara ya Afya.

**Namshukuru Mheshimiwa Rais kwa dhamira yake ya kuendelea kuipa kipaumbele Sekta ya Afya kwa kufanya uwekezaji mkubwa wa rasilimali na kuimarisha kwa viwango vya juu vya Diplomasia ya Kimataifa katika eneo la Afya pamoja na kuboresha upatikanaji wa huduma za afya zenye ubora kwa wananchi**. Hakika Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **ni jemedari na kiongozi mbobezi** wa aina ya kipekee anayefanya mapinduzi makubwa katika Sekta ya afya. Uwekezaji alioufanya unajidhihirisha kupitia mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi cha miaka minne cha uongozi wake kwani unagusa maisha ya kila siku ya wananchi kutokana na ukweli kwamba **Mtu ni Afya, Afya ni Mtaji na Afya ni Usalama na Ustawi wa Nchi**.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** nachukua nafasi hii pia kumpongeza **Mheshimiwa Rais** kwa kuaminiwa na Chama cha Mapinduzi na kuchaguliwa kwa kishindo kuwa mgombea wa nafasi ya urais kwa kipindi kijacho cha miaka mitano (5) katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika mwezi Oktoba, 2025. Pia, nampongeza **Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi** kwa kuteuliwa na kuchaguliwa kuwa mgombea mwenza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, nampongeza **Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi** kwa kupendekezwa na Chama cha Mapinduzi kuwa

Mgombea wa urais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutoa shukrani za dhati kwa **Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango,** Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ameendelea kuwa mstari wa mbele kumsaidia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuimarisha huduma za afya nchini. Pia, nitumie fursa hii kumshukuru **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb)**, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake katika kumsaidia Mheshimiwa Rais kuratibu huduma zinazotolewa na Sekta ya Afya nchini. Aidha, nampongeza **Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb),** Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kumsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu kusimamia Sekta ya Afya pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa nishati unaowezesha kuimarisha huduma bora za afya nchini.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kukupongeza wewe binafsi kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu Tukufu kwa umahiri mkubwa unaodhihirika katika kufikia maamuzi yenye manufaa kwa ustawi wa Taifa letu licha ya majukumu uliyonayo ya Urais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU). Aidha, nampongeza **Naibu Spika**, **Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu**, kwa kuendelea kukusaidia vyema katika kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uadilifu mkubwa. Nitumie fursa hii pia kuwapongeza

Wenyeviti wa Bunge kwa kusimamia vyema mijadala ndani ya Bunge.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee napenda kumpongeza Mheshimiwa **Elibariki Emmanuel Kingu (Mb)** Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kwa kuiongoza vyema Kamati. Hakika Mwenyekiti wetu wa Kamati ni kiongozi mchapakazi na mwenye upeo wa juu katika kusimamia Sekta ya Afya. Napenda kumshukuru yeye na wajumbe wa Kamati kwa ushauri na maelekezo wanayotoa katika kuboresha utendaji wa Wizara. Aidha, **ninawashukuru Waheshimiwa wabunge wote** kwa ushirikiano mzuri wanaonipatia ikiwemo kutoa ushauri na maoni mbalimbali yenye lengo la kuboresha huduma za afya kwa Watanzania. Ninawaahidi waheshimiwa Wabunge kwamba, Wizara itazingatia ushauri wenu katika utekelezaji wa majukumu yetu ya kila siku kwa wananchi. Vilevile, ninatoa shukrani zangu za dhati **kwa Katibu wa Bunge na watumishi wa Bunge** kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia. Niwahakikishie kuwa viongozi na watumishi wa Sekta ya Afya nchini tutaendelea kutekeleza wajibu wetu wa kutoa huduma bora za afya kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu za utoaji huduma za afya.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee nimpongeze Mheshimiwa **Steven Masatu Wasira** kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Chama

cha Mapinduzi Tanzania Bara. Vilevile nichukue fursa hii kumshkuru sana Waziri wa nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI pamoja na kuwashukuru Waheshimiwa mawaziri wenzangu na **Mwanasheria Mkuu wa Serikali** kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia katika kuboresha usimamizi wa utoaji huduma bora za afya nchini.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutoa pongezi za dhati kwa **Mhe. Dkt. Godwin Oloyce Mollel** (Mb), Naibu Waziri wa Afya, kwa mchango wake muhimu katika Sekta ya afya na kuendelea kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kunisaidia kusimamia Sekta hii na kwa uchapaji kazi wake huo ninawaomba wananchi wa Siha kuendelea kumuamini. Vilevile, nawapongeza **Dkt. Seif Abdallah Shekalaghe**, Katibu Mkuu, **Ndugu Ismail Hassan Rumatila**, Naibu Katibu Mkuu, pamoja na **Dkt. Grace Elias Magembe**, Mganga Mkuu wa Serikali kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kushika nyadhifa hizo na ninawashukuru kwa ushirikiano wao wa dhati kwangu. Kipekee niishukuru **Menejimenti ya Wizara ya Afya na watumishi wote wa Sekta ya Afya** kwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, moyo wa kizalendo na imani thabiti kwa uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita. Aidha, nichukue nafasi hii kumpongeza **Prof. Tumaini J. Nagu** kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** nichukue fursa hii kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** katika kuimarisha mizania ya ukuaji wa mahusiano ya kidiplomasia ya afya, jambo lililowezesha nchi yetu **kutambulika, kukubalika na kuaminiwa** na mataifa mengine na kupewa nafasi adhimu za uongozi wa Sekta ya Afya kimataifa. Napenda kumpongeza **Prof. Mohammed Yakub Janabi** kuchaguliwa kwa ushindi wa kihistoria na kishindo kuwa Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani Kanda ya Afrika. Nafasi hii tumeshinda kwa mara ya pili baada ya Mkurugenzi Mteule **Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile** kufariki dunia. Aidha, napenda kumpongeza Dkt. Ntuli Angyelile Kapologwe kwa kuchaguliwa kuwa Mtendaji Mkuu wa Jumuiya ya Afya ya nchi za Afrika Mashariki, Kati na Kusini. Nafasi hii tumeipata kwa mara nyingine baada ya **Dkt. Winnie Mpanju** ambaye alishika kipindi cha nyuma. Ushindi wao umeleta heshima kwa Bara la Afrika na kwa watanzania kwa ujumla.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia Bunge lako tukufu napenda kuishukuru Kamati ya Kampeni iliyowezesha wagombea wetu kushinda kwa kishindo. Kipekee namshukuru **Mheshimiwa Dkt Jakaya Mrisho Kikwete, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyekuwa Mwenyekiti wa Kampeni** pamoja na kamati nzima kwa kufanya kazi usiku na mchana bila kuchoka na kwa weledi

mkubwa. Aidha, napenda kutambua michango ya Wizara zote zikiongozwa na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Hivyo, kwa niaba ya Sekta ya Afya nasema asanteni sana

11. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kumpongeza **Dkt. John Christian Rwegasha** kwa kuteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Tiba katika Kamisheni ya Umoja wa Afrika. Aidha, nampongeza **Prof. Kaushik Ramaiya** kwa kutunukiwa tuzo ya **Pravasi Bharatiya Samman** ya Rais wa India inayotambua mchango wake kwa jamii katika kupambana na magonjwa yasiyoambukiza.

12. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee naishukuru familia yangu kwa ushirikiano wanaonipa, sala na maombi yao wakati wote ninapotekeleza majukumu yangu. Kipekee na kwa unyenyekevu mkubwa, nitumie fursa hii mbele ya Bunge lako Tukufu kuwashukuru kwa moyo wa dhati **wananchi wote wa jimbo langu pendwa la Peramiho** kwa namna mnavyoniamini na kunipa ushirikiano wa kiwango cha juu katika kipindi chote ninachowatumikia kama Mbunge wenu. Mara zote ninajikuta mwenye nguvu na ari kubwa ya kuwatumikia pasipo kuchoka na ninawathibitishia kwamba bado nina nia, nguvu na ari ya kuendelea kushirikiana nanyi katika kuendeleza kazi tuliyoianza kwa pamoja ya kuleta maendeleo. Mahaba yangu kwa wananchi wa jimbo la Peramiho hayana kipimo, moyo na akili zangu muda wote ni kuhusu namna ya kuendelea kuwatumikia. Mimi mtoto wenu

ninawaahidi kuwa baada ya shughuli hii nitarudi kuungana nanyi na ninaamini kuwa mtaendelea kuniunga mkono kama mlivyofanya katika vipindi vilivyopita.

***13.*** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa masikitiko napenda kutoa pole kwako wewe Binafsi na Bunge lako Tukufu, wanafamilia wote, ndugu, jamaa, marafiki, na wananchi wote kwa ujumla kwa kuondokewa na wapendwa wetu; **Cleopa David Msuya** aliyewahi kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; **Profesa Philemon Sarungi,** aliyewahi kuwa Waziri katika Wizara mbalimbali, **Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile** aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kigamboni na Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani Kanda ya Afrika na **Jaji Frederick Werema** aliyewahi kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

***14.*** ***Mheshimiwa Spika,*** natoa pole kwa watumishi wa Sekta ya Afya kwa kuwapoteza watumishi wenzao katika kipindi hiki na watanzania wote, waliopoteza ndugu zao kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na magonjwa, ajali na majanga mbalimbali ikiwemo kuporomoka kwa jengo la ghorofa Kariakoo Jijini Dar es Salaam. Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

## SEHEMU YA II: MAMBO MAKUBWA YALIYOTEKELEZWA NA SERIKALI YA AWAMU YA SITA KATIKA SEKTA YA AFYA KUANZIA MWAKA 2021 HADI 2025

*15.* ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kutoa maelezo yangu ya utangulizi, naomba sasa kutambua mafanikio makubwa ya kiuwekezaji yaliyopatikana kupitia utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2020-2025 chini ya Uongozi wa **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tangu alipoingia madarakani

### Kuimarika kwa Huduma za Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto

*16.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imekamilisha ujenzi wa jengo la kutoa huduma za afya ya Mama na Mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya ambayo tayari inatumika na imegharimu Shilingi Bilioni 13.2. Kukamilisha ujenzi wa majengo ya huduma za Mama na Mtoto (Maternity Blocks) kwenye Hospitali za Rufaa za Mikoa ambazo ni Sekou Toure (Mwanza), Geita, Simiyu, Mawenzi, Njombe na Songwe ambazo zimegharimu kiasi cha Shilingi Bilioni 71.1. Kuongezeka kwa idadi ya vituo vyenye uwezo wa kutoa huduma za upasuaji wa dharura wa kumtoa mtoto tumboni kutoka vituo 388 mwaka 2021 hadi

kufikia vituo 577 Machi, 2025 ikiwa ni ongezeko la vituo 178. Kuongezeka kwa wodi/vyumba maalum kwa ajili ya huduma za watoto wachanga wanaozaliwa na uzito pungufu (NCU), kutoka 80 mwaka 2021 hadi kufikia 362 Machi, 2025. Huduma hizi zinapatikana katika Hospitali 318 za Halmashauri, Hospitali za Rufaa za Mikoa 28, Hospitali za Rufaa za Kanda sita (6), Hospitali ya Taifa na 108 Hospitali za Mashirika ya Dini na Binafsi. Kuimarisha upatikanaji wa bidhaa za Afya ya Uzazi na Mtoto ambao umeongezeka kutoka asilimia 82.5 mwaka 2021 hadi asilimia 88 Machi 2025.

***17.*** ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio mengine ni kuongezeka kwa idadi ya vifaa tiba vya afya ya uzazi, mama na mtoto vyenye thamani ya Shilingi Bilioni 10.8 katika vituo vya kutolea huduma za afya. Vifaa hivyo ni pamoja na "BP Machine" 50,000 zenye thamani ya Shilingi Billioni 3.01; mashine za CPAP 130 zenye thamani ya Shilingi Milioni 213; vifaa vya CPAC vyenye thamani ya Shilingi milioni 276; vifaa vya NICU 120 vyenye thamani ya Shilingi Bilioni 6.2; mashine 140 (Thermalcoagulator) za uchunguzi wa saratani ya mlango wa kizazi zenye thamani ya Shilingi Bilioni 1.1.

***18.*** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia kampeni za Madaktari Bingwa wa Dkt. Samia kwa awamu ya kwanza na ya pili jumla ya wagonjwa 154,015 kutoka katika Halmashauri 184 nchini waliweza kupata huduma za

ubingwa na ubingwa bobezi za Afya ya uzazi na ukunga, Watoto wachanga, upasuaji magonjwa ya ndani, kinywa na meno, usingizi na ganzi. Aidha, kupitia kampeni hiyo jumla ya watumishi wa afya wapatao 9,434 walijengewa uwezo katika kutoa huduma za dharura za uzazi mama na mtoto. Huduma hizo katika awamu zote mbili zimegharimu kiasi cha Shilingi Bilioni 3.8

19. ***Mheshimiwa Spika,*** Maono ya Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, uwekezaji katika miundombinu ya upasuaji kwa wajawazito, dawa za uzazi salama, uwepo wa mfumo wa rufaa wa dharura kwa wajawazito (M-MAMA), kuimarika kwa uwajibikaji wa watendaji katika ngazi zote za utoaji huduma na ushirikishwaji wa vyama vya kitaaluma umefanikisha kupunguza vifo vya akinamama vitokanavyo na uzazi kutoka 556 hadi 104 kwa kila vizazi hai 100,000.
***Mafanikio hayo yamesababisha Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutunukiwa tuzo ya kimataifa ijulikanayo kwa jina la Goalkeeper Award, iliyotolewa na Taasisi ya Gates ya Marekani, tarehe 4 Februari, 2025.*** **Tuzo hii hutolewa kwa Viongozi waliofanikiwa kutekeleza kwa mafanikio Malengo ya Maendeleo Endelevu;**

- Mheshimiwa Rais amekuwa Rais wa

kwanza Barani Afrika kutunukiwa tuzo hii

- Amekuwa Rais wa kwanza mwanamke kutunukiwa tuzo hii
- Amekuwa ni Rais wa kwanza kutunukiwa tuzo hii nchini kwake
- Amekuwa ni Rais wa kwanza Duniani kutunukiwa tuzo ya kuokoa vifo vya wanawake wakati wa uzazi
- Amekuwa ni Rais wa kwanza kupokea tuzo hiyo na kuikabidhi kwa watumishi wa Sekta ya Afya waliochangia kuokoa vifo vya akinamama na watoto.

***20. Mheshimiwa Spika,*** katika utekelezaji wa **Mpango Jumuishi wa Wahudumu wa Afya ngazi ya Jamii** kwa lengo la kuwafikia wananchi katika ngazi ya kaya, jumla ya wahudumu 12,832 wamechaguliwa na kati yao 3,706 wamehitimu mafunzo na 4,309 wanaendelea na mafunzo katika vyuo 45 nchini. Lengo ni kufikia wahudumu ngazi ya jamii 137,294 ifikapo 2029.

**"*Wahudumu wa Afya ngazi ya Jamii ni macho yetu, masikio yetu, na mikono yetu katika kaya, vijiji na mitaa. Wanaelimisha, wanatambua mazingira hatarishi ya kiafya mapema na kuwezesha jamii na Serikali kuchukua hatua za udhibiti mapema. Wahudumu hao si tu watoa huduma, bali ni viongozi wa mabadiliko ya afya katika jamii zao. Hivyo wananchi wawapokee na*

***kuwapa ushirikiano wanapokuwa kwenye majukumu yao maana ni kiungo muhimu katika kufikia afya bora kwa wote".***

**Kuimarika kwa Miundombinu ya kutolea Huduma za Afya**

***21. Mheshimiwa Spika,*** vituo vya kutolea huduma za afya vimeongezeka kutoka vituo 8,549 mwaka 2021 na kufikia vituo 12,846 Machi, 2025 sawa na ongezeko la vituo 4,297 vilivyojengwa katika kipindi cha Awamu ya Sita. Aidha, kuna ongezeko la majengo mapya katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kaskazini – KCMC, Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya na Hospitali ya Benjamin Mkapa-Dodoma, Hospitali ya Rufaa ya Kanda Bugando, Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe na Hospitali ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto, Hospitali ya Rufaa ya Kanda Kusini Mtwara na Hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato pamoja Hospitali za Rufaa za Mikoa ya Ligula (Mtwara), Sekou Toure (Mwanza), Maweni (Kigoma), Sumbawanga (Rukwa), Kitete (Tabora), Ukerewe (Mwanza) pamoja na ujenzi wa hospitali mpya katika mikoa mipya mitano (Katavi, Njombe, Geita, Simiyu na Songwe) na kuhamisha Hospitali tano (5) kutoka majengo yake ya zamani kwa kujenga Hospitali mpya katika maeneo mapya, Hospitali hizo ni Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma, Shinyanga, Singida, Mara na Lindi. Maboresho hayo na ujenzi vimegharimu jumla ya Shilingi Trilioni 1.03. Vilevile,

kumefanyika ukarabati wa majengo ya zamani katika Hospitali Kongwe 50 za Halmashauri, ukamilishaji wa maboma ya Zahanati 980, ujenzi wa Vituo vya Afya 390, ujenzi wa kituo cha kutibu magonjwa ya milipuko Kisopwa mkoani Pwani, ujenzi wa mitambo 21 ya kuzalisha hewa tiba ya oksijeni kwa ajili ya wagonjwa mahututi na Wagonjwa wa dharura na ujenzi wa nyumba za Watumishi wa afya 270.

22. ***Mheshimiwa Spika***, idadi ya **vitanda vya wagonjwa** katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini imeongezeka kutoka vitanda 86,131 mwaka 2021 hadi vitanda 153,683 Machi, 2025. Ongezeko la vitanda vya wagonjwa limesaidia kuongeza ubora na ufanisi wa huduma za afya hususan huduma za afya ya mama na mtoto. Aidha, idadi ya vitanda katika vituo vya umma kwa ajili ya wagonjwa mahututi (ICU) imeongezeka kutoka vitanda 258 vya mwaka 2021 hadi kufikia vitanda 1,362 Machi 2025. Ongezeko hili limejumuisha vitanda vya wodi za watoto wachanga wagonjwa (NCU).

***Ongezeko la vitanda vya wagonjwa mahututi (ICU) katika Hospitali za umma linalenga kuboresha huduma na kupunguza vifo vinavyotokea ndani ya hospitali ambavyo vinaweza kuzuilika.***

**Kuimarika kwa upatikanaji na uimarishaji wa Huduma za Uchunguzi**

***23.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha huduma za uchunguzi wa mionzi kwa wagonjwa, Serikali imenunua na kusimika vifaa tiba vya uchunguzi na matibabu ya wagonjwa vyenye thamani ya Shilingi Bilioni 228.1 ambavyo vinapatikana kuanzia ngazi ya Hospitali ya Taifa hadi katika ngazi ya Afya ya Msingi ambapo Mwaka 2021 hadi Machi 2025 MRI zimeongezeka kutoka saba (7) hadi kufikia 13, CT Scan 12 hadi 45, Mini Angio Suite tano (5), kipimo cha uchunguzi na tiba ya magonjwa ya mfumo wa chakula na mfumo wa uzazi (Fluoroscopy) 13, Digital X-ray 147 hadi 491, Ultrasound 476 hadi 970, huduma ya kutibu matatizo ya moyo ya dharura (CATHLAB) moja (1) hadi nne (4) na matibabu ya hali ya juu ya magonjwa ya saratani (PET CT SCAN) haikuwepo sasa ipo moja (1) nchini yenye thamani ya Shilingi Bilioni 18.5. Aidha, kuongezeka kwa vifaa, vifaa tiba vya uchunguzi kumepunguza rufaa za ndani na nje ya nchi, kumewezesha kusogeza huduma kwa wananchi kwa gharama nafuu na kusaidia kutoa matibabu sahihi zaidi na kwa wakati sahihi.

## Kuimarika kwa Magonjwa ya Milipuko na Huduma za dharura

24. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa miaka ya hivi karibuni nchi yetu imekuwa ikikabiliwa na milipuko ya magonjwa mbalimbali ikiwemo UVIKO-19, Kipindupindu, Homa ya Mgunda, Kimeta, Surua, Marburg pamoja na ongezeko la magonjwa ya mafua makali ya influenza na virusi vingine. Vilevile nchi yetu imekuwa katika hatari ya kupata magonjwa mengine kutokana na uwepo wa milipuko ya magonjwa hayo katika nchi jirani ikiwa ni pamoja na Polio, Ebola na Homa ya Manjano katika nchi za jirani. Hivi Karibuni, mnamo mwezi Machi 2025, nchi yetu ilithibitisha uwepo wa ugonjwa wa Mpox ambao kwa kipindi cha miaka miwili (2) tangu ulipoathiri nchi za Ulaya, Amerika na nchi nyingine za Afrika, Serikali imekuwa ikipambana kuuzuia usiingie nchini.

25. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kufanya tathmini ya utayari kwa nchi kufuatia mlipuko wa ugonjwa wa Ebola uliotokea kwa nyakati tofauti katika mwaka 2022, 2024 na 2025 katika nchi jirani ya Uganda, Rwanda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Kongo, hivyo kuimarisha uchunguzi wa wasafiri na udhibiti wa ugonjwa kuingia nchini kupitia mipaka na mikoa iliyoko katika hatari zaidi mfano mikoa ya Kagera, Kigoma, Mwanza, Mara, Geita, Arusha, Dodoma, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mbeya na Songwe. Hatari hiyo ni kutokana na

mwingiliano katika shughuli za kiuchumi na kijamii na nchi hizo. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI ilichukua hatua za kuzuia kuingia kwa maambukizi nchini na kuimarisha hali ya utayari katika Mikoa yote. Hadi kufikia Machi 2025, hakuna taarifa za uwepo wa mgonjwa aliyethibitika kuwa na ugonjwa wa Ebola nchini.

***26.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika kukabiliana na matishio ya magonjwa haya ya milipuko Serikali imeendelea kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa salama dhidi ya magonjwa hayo kwa kuweka miundombinu imara katika maeneo ya mipaka, viwanja vya ndege, bandari na stendi za mabasi. Aidha, Serikali imeongeza vituo vya menejimenti ya matukio ya dharura za afya ya jamii (Public Health Emergency Operations Centers - PHEOC) mikoani kutoka vituo sita (6) mwaka 2021 hadi kufikia vituo 20 Machi, 2025. Vilevile, Serikali imeimarisha miundombinu na kununua vifaa vya kisasa vya TEHAMA na samani vyenye thamani ya Shilingi Bilioni 4.02 kwa ajili ya vituo hivyo katika Mikoa 20 hadi kufikia Machi 2025. Vituo hivi vinawezesha kupokea na kuchakata taarifa za matukio na milipuko ya magonjwa kutoka katika mifumo mingine ya ufuatiliaji wa magonjwa ili kuchukua hatua na kuratibu afua za udhibiti kwa haraka.

***27.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha uwezo wa uchunguzi wa maabara nchini ikiwemo

maboresho ya miundombinu na vifaa vya kisasa kwa kujenga maabara ya kisasa ya Usalama wa Kibailojia Daraja la 3 katika hospitali ya Kibong'oto. Maabara hii ni mojawapo ya maabara tano (5) Afrika zenye hadhi ya kuwa maabara za rufaa za kimataifa. Aidha, maboresho yamefanyika katika Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii ikiwemo ununuzi wa Maabara jongezi mbili (2) za uchunguzi wa maabara, zinazoweza kutumika eneo lolote nchini ambako mlipuko utatokea. Maabara hizi ziliwezesha nchi yetu kupima na kugundua virusi hatari vinavyosababisha ugonjwa wa Marburg bila kusafirisha sampuli nje ya nchi. Vilevile, Serikali imeimarisha uchunguzi wa magonjwa ya mlipuko katika mipaka ya nchi kavu, majini na viwanja vya ndege kwa kuweka mashine za kisasa za uchunguzi wa jotomwili (thermoscanners) 16 kwa ajili ya kuchunguza wasafiri wote wanaoingia au kutoka nchini kwa mujibu wa kanuni za afya za kimataifa.

28. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha huduma za matibabu ya magonjwa hatari ya kuambukiza kwa kuanzisha hospitali ambayo itakuwa ni kituo cha umahiri cha kuwatenga na kutibu magonjwa ya kuambukiza ikiwemo Marburg, Ebola na magonjwa mengine ya mlipuko katika mkoa wa Kagera. Eneo limepatikana katika mji wa Bukoba, upembuzi yakinifu umekamilika na Serikali imesaini makubaliano ya kuanza ujenzi wa hospitali hiyo na

Serikali ya watu wa Falme za Kiarabu (UAE) ili ujenzi huo uanze mapema mwaka huu.

29. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia uwekezaji katika miundombinu na kuzijejengea uwezo timu za wataalam , Tanzania iliweza kukabiliana kwa mafanikio makubwa dhidi ya ugonjwa wa UVIKO 19 kwa mwaka 2021 hadi 2023. Vilevile, nchi yetu ilikumbwa na mlipuko wa ugonjwa wa Marburg kwa mara ya kwanza mwaka 2023 Mkoani Kagera ambapo tuliweza kukabiliana nao ndani ya siku 69 na kuudhibiti. Mnamo Januari 2025 ulitokea mlipuko wa pili wa ugonjwa wa Marburg ambao uliweza kudhibitiwa na kutokomezwa ndani ya siku 54 ikilinganishwa na siku 69 za mlipuko wa kwanza.

30. ***Mheshimiwa Spika,*** nchi yetu imekuwa kinara kwa kushiriki kufanya tathmini za kimataifa za kupima uwezo wa kukabiliana na dharura za afya zenye athari kimataifa, ambapo Februari 2016 Tanzania ilikuwa ya kwanza duniani kufanya *Joint External Evaluation (JEE),* ambapo wataalam wa sekta mbalimbali ndani na nje ya nchi hufanya tathmini ya uwezo wa nchi wa kuzuia, kugundua na kukabiliana na dharura za afya ya jamii ikiwemo magonjwa ya mlipuko. Nchi yetu imefanya tathmini ya pili mwaka 2023 na kuonesha kuimarika zaidi kwa uwezo wa ndani wa nchi katika kujikinga, uchunguzi wa kimaabara na kukabiliana na magonjwa ya afya ya jamii. Hatua hii inawezesha nchi kufanya vizuri katika

utekelezaji wa Kanuni za Afya za Kimataifa za Shirika la Afya Duniani (WHO) na agenda ya usalama wa afya kimataifa (Global Health Security Agenda) inayotutaka kuimarisha uwezo wa kubaini mapema, kupima, kuthibitisha na kutoa taarifa na namna nchi inavyokabiliana na dharura hizi na kudhibiti zisisambae katika nchi zingine bila kuathiri biashara na usafirishaji wa bidhaa na watu.

***31.*** ***Mheshimiwa Spika,*** mnamo Novemba, 2024 Tanzania ilifanya tathmini nyingine ya hiari ya kimataifa iliyoanzishwa na Shirika la Afya Duniani inayoitwa *Universal Health and Preparedness Review.* Taarifa ya tathmini hiyo ilizinduliwa na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kufanya nchi yetu kuwa ya tano (5) katika Afrika na ya nane (8) duniani kujifanyia tathmini ya uwezo wa kukabiliana na dharura za afya na kuhakikisha ngazi ya juu ya Serikali na jamii yote inashirikishwa na kutambua kuwa suala la mapambano dhidi ya milipuko ya magonjwa ni la sekta zote na la kila mtu chini ya afya moja yaani afya ya wanyama na mifugo, afya ya vyakula, afya ya mazingira na afya ya binadamu.

***32.*** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa sasa Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-TAMISEMI na Sekta zingine, inaendelea kutekeleza  na afua za udhibiti wa mlipuko wa Mpox kwa kutoa elimu kwa umma, ufuatiliaji wa wahisiwa na wagonjwa katika jamii na

kuimarisha matibabu kwa wagonjwa wanaothibitika kuwa na maambukizi ya Mpox. Hadi kufikia Machi, 2025 wagonjwa waliokuwa wakifika katika vituo vya kutolea huduma za afya wameendelea kupatiwa matibabu na afya zao kuimarika na kuruhusiwa. Wizara inaendelea kuwahimiza wananchi kuendelea kushiriki kikamilifu kudhibiti na kuzuia usambaaji wa ugonjwa huu kwa kuchukua hatua za kinga hususani kuepuka kujamiiana na mpenzi au mwenza mpya usiyejua hali yake ya kiafya, kuepuka kumhudumia au kugusa majimaji ya mwili ya mtu mwenye dalili za ugonjwa bila kinga, kuweka vitakasa mikono katika maeneo ya mikusanyiko ikiwemo Masoko, Shule, Kumbi za Starehe, Nyumba za ibada, majumbani na maeneo mengine ya shughuli za kila siku. Afua hii itapunguza uwezekano wa kusambaa kwa maambukizi ya Mpox na magonjwa mengine ya kuhara na kutapika.

***33. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutoa mafunzo maalum kuhusu magonjwa ya mlipuko, huduma za wagonjwa mahututi, na tahadhari za kuzuia maambukizi kwa mikoa yote iliyopo kwenye hatari ya magonjwa hayo. Kwa kuwa Tanzania inatarajia kuwa mwenyeji wa mashindano ya AFCON mwaka 2027, Wizara imeongeza idadi ya madaktari bingwa 48 wa magonjwa ya dharura kwa kuwagharamia masomo katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi, Muhimbili. Hatua hii inalenga kupunguza uhaba wa wataalam wa huduma za

dharura na kuboresha utoaji wa huduma wakati wa mashindano hayo muhimu. Aidha, madaktari 20 wa dharura kutoka Muhimbili, Amana, Temeke, Kigamboni, Tumbi, na Arusha wamepatiwa mafunzo maalum nchini Uturuki mwaka 2024, yanayolenga kuimarisha huduma za dharura nchini.

**Kuongezeka kwa Rasilimali Watu katika Sekta ya Afya**

***34.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuajiri wataalam katika Sekta ya Afya ambapo jumla ya wataalam 48,633 wa kada mbalimbali wameajiriwa na kusambazwa katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini katika kipindi cha kuanzia mwaka 2021 hadi 2024 na hivyo kufanya idadi ya watumishi katika Sekta ya Afya kufikia 177,711 mwezi Machi, 2025 . Aidha, watumishi 8,146 waliajiriwa kwa mikataba kutumia vyanzo vya ndani vya mapato ya vituo vya kutolea huduma za afya.

***35.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa wataalam bingwa na bingwa bobezi kwa ajili ya utoaji wa huduma za uubingwa na ubingwa bobezi kwa kuanzisha **Samia Health Super Specialization Scholarship Program** ambapo hadi sasa, jumla ya wataalam 2,779 wamepata mafunzo mbalimbali ya uubingwa na ubingwa bobezi kazini na hivyo kuongeza idadi ya wataalam wa mafunzo ya

ubingwa na ubingwa bobezi kutoka 768 mwaka 2021 hadi 1,420 Machi, 2025.

**Jitihada hizo zimesaidia kupata wataalam wa afya kwenye fani za kibingwa na bobezi watakaotumika kujenga uwezo wa wataalam wetu wa afya katika vyuo vya mafunzo ya afya nchini pamoja na kupunguza rufaa za matibabu kwa wagonjwa nje ya nchi. Vilevile, jitihada hizo zitaimarisha tiba utalii nchini.**

**Kuimarika na Kuongezeka kwa Hali ya Upatikanaji wa Bidhaa za Afya**

***36.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2021 hadi Machi, 2025 hali ya upatikanaji wa bidhaa za afya muhimu za kipaumbele 382 ngazi ya vituo vya kutolea huduma za afya imeimarika kutoka asilimia 58 mpaka asilimia 87 sawa na ongezeko la asilimia 29. Katika kipindi hicho, Zahanati asilimia 69 hadi kufikia asilimia 78, Vituo vya Afya asilimia 68 hadi kufikia asilimia 76, Hospitali za Wilaya asilimia 72 hadi kufikia asilimia 81, Hospitali za Rufaa za Mikoa asilimia 83 hadi kufikia asilimia 97, Hospitali za Kanda, Maalum na Taifa asilimia 58 hadi kufikia asilimia 99.

***37.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2021 hadi Machi, 2025, Jumla ya Shilingi Bilioni 529.2 zimetolewa kwa ajili ya kugharamia ununuzi wa bidhaa za afya kupitia Bohari ya Dawa (MSD). Pia,

katika kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vya dawa na bidhaa za afya nchini Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kumewezesha kuanzishwa kwa viwanda vipya 10 vya dawa na vifaa tiba ambavyo ni viwanda vya kuzalisha maji tiba viwili (2), viwanda vya kuzalisha vitendanishi vya maabara vitatu (3), viwanda vya kuzalisha dawa za vidonge na maji viwili (2) na viwanda vya kuzalisha vifaa tiba vitatu (3).

***38.*** ***Mheshimiwa Spika***, **kuimarika kwa uwekezaji wa viwanda vya dawa na bidhaa za afya nchini** ambapo Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imewezesha kuanzishwa kwa viwanda vipya 10 vya dawa na vifaa tiba. Viwanda hivi vitawezesha uwepo endelevu wa maji tiba, vitendanishi vya maabara, dawa za vidonge na maji hususan dawa za ARV ambapo Serikali kupitia MSD imeanzisha utaratibu wa kufufua na kukiwezesha kiwanda cha Tanzania Pharmacetical Industry (TPI) kilichopo Arusha kuanza kuzalisha ARV.

***39.*** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuimarisha kiwanda cha **Viuadudu Kibaha** kwa kutoa jumla ya Shilingi Bilioni 7 kwa ajili ya kuendeleza kiwanda hicho hususan katika eneo la uimarishaji wa matumizi ya teknolojia. Fedha hizo, zimewezesha ununuzi wa lita 583,333.3 ambazo zinaendelea kusambazwa katika Halmashauri zote nchini.

40. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba, imeendelea kuimarisha usimamizi na udhibiti wa vifaa tiba nchini ambapo **Mamlaka ya Dawa na Vifaa tiba nchini (TMDA) imeendelea kuwa kinara** kwa kushikilia cheti cha utambuzi wa umahiri katika mifumo ya udhibiti ubora wa dawa kwa vigezo vya Shirika la Afya Duniani (WHO) kwa ngazi ya tatu (Maturity Level 3). Hii ikimaanisha kuwa, wananchi wameendelea kupata bidhaa za afya kwa ubora unaokubalika kimataifa.

**Kuimarika kwa Huduma za Ubingwa na Ubingwa Bobezi**

41. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuboresha huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi katika Hospitali ya Taifa, Hospital Maalum, Hospitali za Rufaa za Kanda, na Hospitali za Rufaa za Mikoa ili kuhakikisha huduma hizi zinapatikana ndani ya nchi. Huduma za ubingwa bobezi zilizotolewa ni pamoja na upandikizaji wa vifaa vya usikivu kwa Watoto, Upandikizaji wa figo, Kuwekewa Puto tumboni, Upasuaji wa Moyo bila kufungua kifua, Upasuaji wa moyo kwa kufungua kifua, Upasuaji ubongo, Upasuaji wa uti wa mgongo, Upandikizaji wa nyonga bandia, Tiba ya saratani ya mlango wa kizazi, Tiba ya saratani ya matiti, Tiba ya saratani ya umio, Tiba ya saratani ya Ngozi, Tiba ya saratani ya tezi dume, Upasuaji wa goti bandia, *Kurekebisha mishipa ya damu ya kwenye ubongo*, Upasuaji wa Ubongo kwa njia ya Matundu, Upasuaji wa Vichwa Vikubwa

na Mgongo wazi, Upasuaji wa Kiuno, Upasuaji wa Magoti kwa njia ya Matundu na Radiolojia Tiba .

***Uwekezaji katika huduma za ubingwa na ubingwa bobezi umewezesha watanzania wengi kupata huduma hizi ndani ya nchi kwa gharama nafuu ambapo hapo awali walikuwa wakizifuata huduma hizo nje ya nchi.***

**Kuimarika kwa Tiba Utalii**

***42. Mheshimiwa Spika,*** kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali katika kuboresha huduma za ubigwa na ubingwa bobezi nchini, uwekezaji huo umevutia wagonjwa mbalimbali kutoka nje ya nchi. Katika kipindi cha mwaka 2021 hadi Machi, 2025 idadi ya wagonjwa kutoka nje ya nchi waliokuja kutibiwa nchini imeongezeka kutoka wagonjwa 5,705 mwaka 2021 hadi kufikia wagonjwa 12,180 Machi, 2025. Wagonjwa hao ni kutoka katika nchi za **Comoro, Malawi, Burundi, Zambia, Rwanda, Afrika Kusini, Msumbiji, Congo DRC, Sudan, Uganda, Zimbabwe, Ethipia, Somalia, Kenya, Egypt, na Mauritius.** Aidha Wagonjwa hao walihudumiwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Saratani Ocean Road, Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete, Taasisi ya Mifupa Muhimbili, Hospitali ya Aga khan na Hospitali ya Saifee.

**Kupitishwa kwa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote**

43. ***Mheshimiwa Spika,*** **kupitishwa kwa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote na Bunge lako tukufu Novemba,** 2023 kutahakikisha watanzania wote wanapata huduma bora za afya katika vituo vya kutolea huduma za afya bila kikwazo cha fedha kipindi watakapougua

44. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha huduma za chanjo nchini ambapo usimamizi wa mfumo wa utoaji huduma za chanjo umeimarika na **kiwango cha utoaji wa chanjo za kawaida kimepanda kutoka asilimia 81 hadi kufikia asilimia 97**. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imejenga maghala tisa (9) ya kuhifadhia chanjo pamoja na kununua magari 96 kwa ajili ya kutoa huduma za chanjo nchini.

45. ***Mheshimiwa Spika,*** utoaji wa huduma kwa magonjwa yasiyopewa kipaumbela umeendelea kuimarika kwa **kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais katika azimio la Kigali ambapo takriban watu milioni 34.4 wameweza kukingwa na magonjwa hayo.** Mafanikio hayo yamepunguza idadi ya watu wanaohitaji kinga kwa asilimia 76. Aidha, jumla ya watu 11,228 walipata huduma ya upasuaji wa mabusha na watu 13,779 walipata huduma ya upasuaji mdogo wa kusawazisha vikope ili kuwakinga na upofu utokanao na maambukizi ya trakoma na hivyo kufanya Tanzania kuwa kinara

katika kutokomeza magonjwa hayo ndani na nje ya Afrika.

46. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha huduma za Lishe nchini jumla ya mashine 230 za kunyunyizia virutubishi (dosifiers) kwenye vyakula zimefungwa katika Mikoa 26 nchini na hivyo kufanya jumla ya mashine zote zilizofungwa kufikia 1,402 katika kipindi cha mwaka 2021 hadi Machi, 2025. Kufungwa kwa mashine hizo kutaimarisha maendeleo ya ukuaji wa afya ya watoto na hivyo kuboresha afya zao na kuwakinga na maradhi mbalimbali yanayoweza kuzuilika.

## SEHEMU YA III: MWENENDO WA UTEKELEZAJI WA BAJETI KATIKA KIPINDI CHA JULAI 2024 HADI MACHI 2025

**47.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza majukumu yake, Wizara imeendelea kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025), Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa Taifa (2021/22– 2025/26), Sera ya Afya ya Mwaka 2007, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya 2020-2025, Mpango Mkakati wa Tano wa Sekta ya Afya - HSSP V (2021/22 – 2025/26), Mpango Mkakati wa muda wa kati wa Wizara wa mwaka (2021/22 – 2025/26), Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs - 2030) pamoja na makubaliano ya Kimataifa na kikanda yenye lengo la kuimarisha utoaji wa huduma za afya kwa wananchi.

**48.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika bajeti ya mwaka 2024/25, Wizara kwa kushirikiana na Wizara nyingine, Idara na Taasisi za Serikali, Wakala za Serikali na Wadau wa Maendeleo ilipanga kutekeleza afua mbalimbali zenye lengo la kuboresha utoaji huduma za afya katika maeneo yafuatayo: -

i. Kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa;
ii. Kuimarisha upatikanaji na ubora wa huduma za afya zinazotolewa na vituo vya kutolea huduma za afya kuanzia ngazi ya Zahanati hadi Taifa;

iii. Kuimarisha mifumo ya ugharamiaji wa huduma za afya nchini;
iv. Kuimarisha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto ili kupunguza vifo vya wajawazito na watoto wachanga;
v. Kuimarisha upatikanaji na uendelezaji wa wataalam katika Sekta ya Afya kwa fani za kati, ubingwa na ubingwa bobezi;
vi. Kuimarisha huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi nchini;
vii. Kuendeleza na kusimamia afua za Tiba Asili na Tiba Mbadala;
viii. Kuimarisha upatikanaji wa huduma za tiba dhidi ya magonjwa ya kuambukiza, magonjwa yasiyoambukiza na magonjwa ya mlipuko;
ix. Kuimarisha huduma za afya ya akili, huduma za utengamao hususan kwa watoto, wazee na watu wenye ulemavu; na
x. Kusimamia Tafiti na matumizi ya matokeo ya tafiti mbalimbali za afya.

## MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA

***49. Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Fungu 52 hukusanya mapato kutokana na huduma zitolewazo katika Hospitali na Taasisi zilizo chini yake ikiwemo uchangiaji wa huduma mbalimbali, ada za Vyuo na uuzaji wa zabuni.

50. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2024/25, Wizara na Taasisi zilizo chini yake ilikadiria kukusanya kiasi cha Shilingi 756,866,060,248.00 ambapo kati ya fedha hizo, Shilingi 70,828,500,189.69 ni kutoka Makao Makuu ya Wizara (ikiwemo Bodi, Mabaraza ya Kitaaluma, Elimu ya Afya kwa Umma na Afya Mipakani), Shilingi 134,171,499,810.31 kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa na Shilingi 551,866,060,248.00 ni kutoka Hospitali za Rufaa za Kanda, Hospitali Maalum, Hospitali ya Taifa pamoja na Taasisi zilizo chini ya Wizara.

51. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi, 2025, Wizara na Taasisi zilizo chini yake zimekusanya jumla ya kiasi cha Shilingi **603,699,104,749.50** sawa na **asilimia 80** ya lengo la kukusanya maduhuli ya Shilingi **756,866,060,248.00**. Kati ya fedha hizo, kiasi cha Shilingi **52,396,314,305.99** sawa na **asilimia 74** ya makadirio kimekusanywa kutoka Makao Makuu ya Wizara, kiasi cha Shilingi **117,897,942,665.16** sawa na asilimia **88** kimekusanywa kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa na kiasi cha Shilingi **433,404,847,778.35** sawa asilimia **79** kimekusanywa kutoka katika Taasisi zilizo chini ya Wizara. ***Kiambatisho Na. 1 kinaonesha makusanyo ya maduhuli hayo.***

52. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25 Wizara iliidhinishiwa na Bunge lako tukufu kutumia jumla ya kiasi cha **Shilingi 1,311,837,466,000.00** ili kutekeleza majukumu yake.

Kati ya fedha hizo, kiasi cha **Shilingi 632,267,220,000.00** ni kwa ajili ya **Matumizi ya kawaida** ambapo Mishahara ni **Shilingi 484,935,496,000.00** na matumizi mengineyo ni **Shilingi 147,331,724,000.00**. Aidha, jumla ya **Shilingi 679,570,246,000.00** zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa **Miradi ya Maendeleo** ambapo Fedha za Ndani ni **Shilingi 416,258,609,000.00** na Fedha za Nje ni **Shilingi 263,311,637,000.00**.

***53.*** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya kiasi cha **Shilingi 1,231,841,808,986.02** kimepokelewa sawa na **asilimia 94** ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **Shilingi 472,676,230,409.77** sawa na **asilimia 75** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo Mishahara ni **Shilingi 375,215,222,929.79** na Matumizi Mengineyo ni **Shilingi 97,461,007,479.98**. Aidha, kiasi cha **Shilingi 759,165,578,576.25** sawa na asilimia 112 ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ambapo Fedha za Ndani ni **Shilingi 501,120,174,316.25** sawa na asilimia 120 na Fedha za Nje ni **Shilingi 258,045,404,260.00** sawa na asilimia 98.

## SEHEMU YA IV: UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA 2024/25.

### Huduma za Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuboresha na kusogeza huduma za afya karibu na wananchi ikiwa ni pamoja na kuongeza na kuboresha miundombinu ya kutolea huduma, upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi na kuongeza watumishi wa Sekta ya Afya. Maboresho hayo ni pamoja na kuimarisha huduma za afya ya uzazi mama na mtoto ambapo katika kipindi cha miaka mitano, vifo vitokanavyo na uzazi vimepungua kutoka vifo 556 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2015/16 hadi kufikia vifo 104 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2022.

**55.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha huduma za Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto ili kufikia malengo ya kitaifa na kimataifa, ambapo ifikapo mwaka 2030, lengo ni **kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kutoka 104 ya sasa hadi 70** kwa vizazi hai 100,000, vifo vya watoto wachanga kutoka 24 hadi 12 kwa vizazi hai 1,000, na vifo vya watoto chini ya miaka mitano kutoka 43 hadi 25 kwa vizazi hai 1,000. Kwa kasi iliyopo sasa ni dhahiri kwamba Tanzania itakuwa miongoni mwa nchi chache zitakazoweza kufikia malengo hayo kwa wakati.

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutoa kipaumbele katika **kuboresha miundombinu** ya kutolea huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto.

Uboreshaji huo wa miundombinu umewezesha huduma za dharura za uzazi kuendelea kuimarika kwa kiwango kikubwa. Baadhi ya miundombinu iliyokamilishwa au kuboreshwa katika kipindi hiki ni pamoja na kuboresha vituo vya afya ili viweze kuwa na uwezo wa kufanya upasuaji wa dharura wa kumtoa mtoto tumboni (Comprehensive Emergency Management of Obstetric and Newborn Care - CEmONC), ambapo hadi kufikia Machi 2025 **vituo vinavyotoa huduma za CEmONC vimefikia 577 kutoka vituo 525** kipindi kama hicho mwaka 2024.

***57.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya **wajawazito 2,127,548 walihudhuria kliniki** angalau mara moja kati ya wajawazito **2,077,689** waliotarajiwa. Ongezeko hilo la matumizi ya huduma za kliniki wakati wa ujauzito limetokana na utoaji wa elimu, uwepo wa vituo vya kutolea huduma za afya karibu na wananchi, pamoja na utekelezaji wa mwongozo wa huduma muhimu wakati wa ujauzito.

***58.*** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuzingatia vigezo vya Umoja wa Mataifa, Wizara imeendelea kuimarisha **huduma wakati wa kujifungua** na kuhamasisha wajawazito kujifungulia katika vituo vya kutolea huduma za afya. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya wajawazito 1,928,708 walijifungua na kati yao**, wajawazito 1,686,476 sawa na asilimia 87.4 walijifungulia kwenye vituo** vya kutolea huduma. Aidha, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, wajawazito 1,586,953 sawa na

asilimia 94.6 walihudumiwa na watoa huduma wenye ujuzi, ikilinganishwa na wajawazito 1,543,856 sawa na asilimia 93.7 katika kipindi kama hiki mwaka 2024.

59. ***Mheshimiwa Spika,*** asilimia 60 ya vifo vitokanavyo na uzazi hutokea baada ya kujifungua, hususan siku tatu za mwanzo, vinavyosababishwa na kupoteza damu nyingi baada ya kujifungua, kifafa cha mimba na maambukizi ya bakteria. Wizara imeendelea kuimarisha upatikanaji wa **huduma za afya baada ya kujifungua**. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 **jumla ya akina mama 1,525,672 sawa na asilimia 89.4 ya waliojifungua walipatiwa huduma ndani ya siku tatu za mwanzo** baada ya kujifungua. Sambamba na hilo, jumla ya watoto wachanga 1,517,219 sawa na asilimia 88.9 ya watoto waliozaliwa hai walipata huduma ndani ya siku tatu baada ya kuzaliwa.

***'Nitumie fursa hii kuwapongeza na kuwahimiza kinamama kuendelea kuwahi katika vituo vya kutolea huduma za afya wakati wa ujauzito ili changamoto zao ziweze kugunduliwa na kushughulikiwa mapema. Naomba nitumie fursa hii pia kuwaomba waheshimiwa wabunge wanaume kuwa vinara (champions) wa kuwasindikiza wenza wao kupata huduma wakati wa mahudhurio ya kliniki, wakati wa kujifungua na baada ya kujifungua. Naomba kuwasihi waheshimiwa wabunge wanaume kuwa mfano bora wa matumizi ya huduma hii'.***

60. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha **upatikanaji wa bidhaa za uzazi salama** ikiwemo; Sindano ya *Magnesium Sulphate* kwa ajili ya kifafa cha mimba dozi 335,668 sawa na asilimia 91 ya lengo, dawa ya sindano ya *Oxytocin* dozi 3,468,001 sawa na asilimia 95 ya lengo, kwa ajili ya kukinga na kuzuia kupoteza damu wakati na baada ya kujifungua, dozi 150,583,100 za *Fefol* sawa na asilimia 93 ya lengo, kwa ajili ya kuhakikisha mjamzito ana damu ya kutosha, *Misoprostol* vidonge 349,385 sawa na asilimia 92 ya lengo na dozi 1,963 za *Anti D* sawa na asilimia 86 ya lengo, kwa ajili ya kuzuia kuharibika mimba.

61. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, **Wizara imeanza ujenzi wa NCUs 121**, **hivyo kufikisha jumla ya NCUs 362 ikilinganishwa na 241 zilizokuwepo kwa kipindi kama hiki mwaka 2024**. Kati ya NCUs 362 zilizopo, 318 zipo kwenye ngazi ya Hospitali na 44 zipo katika ngazi ya Vituo vya Afya vinavyofanya upasuaji wa dharura wa kumtoa mtoto tumboni - CEmONC. Aidha, kati ya NCUs 318 zipo kwenye ngazi ya hospitali; 175 ni hospitali ngazi ya Halmashauri, 28 Hospitali za Rufaa za Mikoa, sita (6) Hospitali yza Rufaa za Kanda, moja (1) Hospitali ya Taifa na 108 Hospitali za Mashirika ya Dini na Binafsi.

62. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 Wizara imeendelea kuimarisha **huduma za Afya kwa watoto wachanga wagonjwa na wale waliozaliwa kabla ya wakati**. Wizara

imenunua na kusambaza mashine za kumsaidia mtoto mchanga kupumua aina ya "Continuous Positive Airway Pressure, CPAP" 130, ambazo zilisambazwa kwenye hospitali za halmashauri 100 zenye Wodi Maalum ya watoto wachanga yaani "Neonatal Care Unit, NCUs". Pia, Wizara kupitia Bohari ya Dawa ilinunua dawa ya kusaidia watoto wachanga kupumua, aina ya "Surfactant" dose 550, ambazo zilisambazwa kwenye kanda zote za Bohari ya Dawa nchini.

"***Nitoe rai kwa viongozi ngazi ya Vituo vya kutolea huduma za Afya, Halmashauri na Mikoa kuhakikisha NCUs zote zilizoanzishwa zina vifaa na zifanye kazi; Hospitali na Vituo vya Afya ambavyo bado havijaanzisha NCUs zianzishe na kila Zahanati na wodi za kujifungulia ziwe na "stabilization corner".***

***63.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea kuimarisha huduma kwa watoto chini ya miaka mitano, Wizara imenunua dawa aina ya *Amoxilin* kidonge myeyuko kwa ajili ya kutibu homa ya mapafu (Nimonia) Vidonge 43,763,700 sawa na asilimia 86 ya lengo. Aidha, katika kipindi hicho, Wizara imenunua dawa ya kutibu kuharisha aina ya Zinki na ORS zilizofungashwa pamoja, pakiti 967,425 sawa na asilimia 89 ya lengo. Upatikanaji wa bidhaa hizi umeimarika hadi kufikia asilimia 90 ikiwa ni ongezeko la asilimia 3 ikilinganishwa na kipindi kama hiki mwaka 2024.

***“Tiba dhidi ya Nimonia na Kuharisha kwa watoto ni muhimu katika kuimarisha ubora wa huduma za watoto chini ya miaka mitano, nawasisitiza Viongozi ngazi ya vituo vya kutolea huduma, Halmashauri na Mkoa kuhakikisha, dawa hizi zinapatikana muda wote”.***

***64.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi Julai 2024 hadi Machi 2025, Wizara imeimarisha **upatikanaji wa vitabu vya kliniki ya mtoto na mama (kadi za kliniki)**, kwa kuchapisha na kusambaza nakala 2,350,000 kwa ajili ya kliniki za wajawazito na Watoto, ikilinganishwa na nakala 1,200,000 katika kipindi kama hiki mwaka 2024. Vitabu hivyo vinalenga kuwasaidia wazazi na watoa huduma kufuatilia afya na maendeleo ya ujauzito na maendeleo ya watoto.

***‘Napenda kuwakumbusha watoa huduma za Afya katika Halmashauri na Mikoa, kuwa “Vitabu vya Kliniki ya Mama na Mtoto haviuzwi na wahakikishe vinapatikana muda wote bila malipo kwa wajawazito na watoto’.***

***65.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea **kuboresha huduma rafiki ya Afya ya uzazi kwa vijana, wenye umri kati ya miaka 10 hadi 24** kwa kuzingatia mwongozo wa Ajenda ya Kitaifa ya kuwekeza katika afya na Maendeleo ya vijana (NAIA-AHW) yenye nguzo kuu sita; (i) Kupunguza maambukizi ya VVU kwa vijana, (ii) kupunguza mimba katika umri mdogo,

(iii) kupunguza madhara ya ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto, (iv) kuimarisha afya lishe kwa vijana, (v) kuhakikisha vijana wa kike na kiume wanabaki shuleni na kumaliza masomo yao na (vi) kuwajengea ujuzi vijana ili waweze kujiajiri au kuajiriwa. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, elimu kwa vijana zaidi ya 450 katika Mikoa ya Njombe, Ruvuma, Iringa, Manyara, Dodoma, Morogoro, Pwani na Tabora imetolewa, na idadi ya vituo vya kutoa huduma rafiki ya Afya ya uzazi kwa vijana vimeongezeka hadi kufikia 1,561 ikilinganishwa na 1,111 kipindi kama hiki mwaka 2024.

***66. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutoa huduma **kwa manusura wa matukio ya ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto (GBV & VAC)**. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya manusura wa matukio ya ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto (GBV & VAC) 183,824 walipatiwa huduma. Kati ya manusura hao, 58,784 sawa na asilimia 32 walifanyiwa ukatili wa kimwili, 17,896 sawa na asilimia 10 ukatili wa kingono, na 6,673 sawa na asilimia 4 walikuwa ni manusura wa ukatili dhidi ya watoto. Aidha, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, idadi ya vituo jumuishi vya kutoa huduma kwa manusura wa matukio ya ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto "One-Stop Centre", imeongezeka na kufikia vituo 31 kutoka vituo 27 katika kipindi kama hiki mwaka 2024.

**“Natoa wito kwa jamii kuzuia vitendo vya ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto, na inapotokea manusura wafikishwe kwenye vituo vya kutolea huduma haraka kwa ajili ya uchunguzi na matibabu”**

***67.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha **huduma za uzazi wa mpango,** ambapo katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 **jumla ya wateja 5,930,037** walipatiwa huduma za uzazi wa mpango. Kati ya hao wateja wapya walikuwa 3,951,648 sawa asilimia 67 ya wateja wote. Aidha, Wateja 1,430,955 sawa na asilimia 24 walipata huduma hizo kupitia huduma mkoba. Vilevile, wanawake 711,626 walipatiwa huduma za uzazi wa mpango mara baada ya kujifungua. Wizara imeendelea kuhamasisha wanaume kutumia njia za uzazi wa Mpango ikiwemo ya kufunga uzazi (Vasectomy) ambapo kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, wanaume 305 walitumia njia hiyo.

***68.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imeendelea **kununua na kusambaza dawa mbalimbali kwa ajili ya huduma za uzazi wa mpango**. Bidhaa zilizonunuliwa na kusambazwa ni pamoja *Depo provera* dozi 3,874,810 sawa na asilimia 92 ya lengo, Vidonge vya uzazi wa mpango 3,610,038 sawa na asilimia 99 ya lengo, Vipandikizi aina ya *Implanon NXT* 297,721 sawa na asilimia 65 ya lengo, Vipandikizi aina ya *Jadelle* 277,942 sawa na asilimia 87 ya lengo na Vitanzi aina ya *Copper T* 62,470 sawa na asilimia 82 ya lengo.

69. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara, katika kuimarisha **huduma ya saratani ya mlango wa kizazi** kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, **jumla ya wanawake 527,606 walifanyiwa uchunguzi** wa awali. Kati ya hao, 20,528 walionesha mabadiliko ya mlango wa kizazi ambapo 15,614 walikuwa na mabadiliko ya awali ya saratani ya mlango wa kizazi na 4,914 walionesha dalili za saratani. Aidha, wateja 546,993 walifanyiwa uchunguzi wa matiti na kati ya hao 4,692 walikutwa na dalili za awali za Saratani ya Matiti na kupewa huduma stahiki.

70. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha **uchunguzi wa saratani ya mlango wa kizazi,** kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Wizara imeanzisha utaratibu wa kutumia kipimo cha *HPV DNA testing*, katika Mikoa 14 ya; Iringa, Njombe, Mbeya, Songwe, Tanga, Dar es Salaam, Dodoma, Mara, Tabora, Kagera, Shinyanga, Arusha, Simiyu na Mwanza. Aidha, katika kipidi hicho, Wizara imenunua jumla ya mashine 70 za tiba joto (Thermocoagulators)kwa ajili ya kutibu mabadiliko ya awali ya saratani ya mlango wa kizazi. Mashine hizo zimesambazwa katika vituo 70 vya kutolea huduma za afya nchini.

”***Natoa wito kwa wanawake kwenda katika vituo vya kutolea huduma za Afya kwa ajili ya uchunguzi wa Saratani ya mlango wa kizazi na matiti, kwani aina hizo za saratani zinatibika iwapo zitagundulika mapema***”.

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya **watoa huduma 12,330** wamepatiwa mafunzo elekezi kazini kuhusu stadi mbalimbali ikiwemo namna ya kutibu matatizo yatokanayo na uzazi na matatizo ya watoto wachanga (EmONC) katika Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara, ikilinganishwa na watoa huduma 6,000 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Mafanikio haya yametokana na utekelezaji wa programu ya **Madaktari Bingwa wa Dkt. Samia** katika Hospitali za Halmashauri zote 184 nchini na utekelezaji wa mafunzo elekezi kazini kwa kutumia mfumo wa *"**Hub and Spoke**"***.**

**72.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kulifahamisha Bunge lako tukufu kuwa Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sera ya Afya ya mwaka 2007 tamko la 5.3.4 (c) linaloeleza kuhusu kutolewa kwa huduma bila malipo kwa wajawazito na watoto wenye umri chini ya miaka mitano, pamoja na changamoto mbalimbali zinazoikabili ikiwemo mahitaji makubwa ya dawa ikilinganishwa na bajeti inayoidhinishwa na bunge.

**Udhibiti wa Magonjwa Yasiyoambukiza**

**73.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa afua mbalimbali zenye lengo la kuzuia na kudhibiti magonjwa yasiyoambukiza ikiwemo kisukari, magonjwa ya moyo na shinikizo la juu la damu, saratani, magonjwa sugu ya mfumo wa upumuaji, matatizo ya afya ya akili, selimundu, magonjwa ya macho na magonjwa ya figo. Afua za

kuzuia na kudhibiti magonjwa yasiyoambukiza zinajumuisha afua za mazoezi dhidi ya tabia bwete; udhibiti wa matumizi ya tumbaku; udhibiti wa matumizi ya pombe kupita kiasi; pamoja na afua za lishe ikiwemo udhibiti wa matumizi makubwa ya chumvi, sukari na mafuta. Afua nyingine ni pamoja na kuimarisha huduma za afya ya akili, afya ya macho pamoja na huduma za elimu na uhamasishaji wa utambuzi wa viashiria hatarishi vya magonjwa hayo pamoja na matibabu yanayojumuisha huduma za utengamao na huduma shufaa.

***74.*** ***Mheshimiwa Spika***, takwimu za utafiti na ufuatiliaji wa viashiria hatarishi vya magonjwa yasiyoambukiza uliofanywa na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) mwaka 2024, zinaonesha kuwa **ugonjwa wa kisukari katika jamii umepungua kwa asilimia 6.2 kutoka asilimia 9.1 mwaka 2012 hadi asilimia 2.9 mwaka 2023** na tatizo la **shinikizo la juu la damu limepungua kutoka asilimia 26 mwaka 2012 hadi asilimia 22 mwaka 2023**. Hali hii inaweza kuwa imechangiwa na kupungua kwa matumizi ya pombe kutoka asilimia 29.3 mwaka 2012 hadi asilimia 20 mwaka 2023 na matumizi ya tumbaku kutoka asilimia 14.1 mwaka 2012 hadi asilimia 10 mwaka 2023. Aidha, takwimu zinaonesha ongezeko la hali ya ufanyaji mazoezi, hata hivyo kumekuwa na ongezeko la hali ya unene na unene uliokithiri kutoka asilimia 26.0 mwaka 2012 hadi asilimia 30.8 mwaka 2023. Vilevile, kwa mujibu wa taarifa za Shirika la Afya Duniani (WHO) idadi ya wagonjwa wapya wa saratani imeongezeka kutoka

visa vipya 40,464 na vifo vitokanavyo na saratani 26,945 mwaka 2020 na kufikia visa vipya 44,931 na vifo 29,743 mwaka 2022 mtawalia.

75. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na tatizo la magonjwa yasiyoambukiza, Serikali imeimarisha afua za udhibiti katika ngazi zote ikijumuisha udhibiti katika ngazi ya jamii, mashuleni na mahali pa kazi. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, **takribani watu milioni 20 walipatiwa elimu kuhusu magonjwa yasiyoambukiza na afua za kuzuia na kudhibiti magonjwa hayo** kupitia njia mbalimbali ikiwemo usambazaji wa nakala ngumu 15,050 za kitabu cha mtindo bora wa maisha, kuelimisha kuhusu ugonjwa wa kisukari, udhibiti wa pombe na tumbaku pamoja na nakala laini za ujumbe mfupi na kurusha video fupi zaidi ya 10,000 kupitia mitandao ya kijamii.

76. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha tunaifikia jamii na kujenga mazingira wezeshi ya kuelimisha jamii na kuhamasisha utekelezaji wa afua za kuzuia na kudhibiti magonjwa yasiyoambukiza kila mwaka, Wizara huazimisha wiki ya kuzuia na kudhibiti magonjwa yasiyoambukiza ambayo hutekelezwa katika mikoa na halmashauri zote nchini. Katika maadhimisho ya mwezi Novemba, 2024 takribani watu **5,634,348** walipata elimu kuhusu magonjwa hayo na afua za kuzuia na kudhibiti magonjwa yasiyoambukiza. Aidha, watu 412,816 walifanyiwa uchunguzi na kupatiwa huduma ambapo kati yao **watu 11,557 walibainika kuwa na shinikizo la juu**

**la damu na watu 13,796 walibainika kuwa na tatizo la kisukari**. Zoezi la upimaji na uibuaji wa wagonjwa wakati wa maadhimisho, kambi Maalum na huduma mkoba limekuwa na mchango mkubwa katika kuibua wagonjwa wakiwa katika hatua za awali na limesaidia kujenga uelewa katika jamii.

***77.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Ofisi ya Rais -TAMISEMI, Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Chama cha Olimpiki Duniani (IOC) na Shirika la Afya Duniani (WHO) ilitoa mafunzo na kuwajengea uwezo watu 10,780 wakiwemo wasimamizi wa rasilimaliwatu, waratibu wa mipango kutoka Wizara zote, watumishi wa afya, walimu kutoka shule za sekondari na msingi kuhusu ya udhibiti wa Magonjwa hayo kwa lengo la kuimarisha uratibu na usimamizi wa afua hizo mahala pa kazi.

***78.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefanya mapitio ya mwongozo jumuishi wa matibabu ya magonjwa yasiyoambukiza ili kuruhusu utoaji wa huduma sambamba na huduma nyingine zinazotolewa katika miradi misonge ikiwemo huduma kwa wagonjwa ya VVU, kifua kikuu, magonjwa ya ngono, na Homa ya Ini kwa kujumuisha magonjwa yasiyoambukiza na afya ya akili. Wizara ilifanya tathmini na kuandaa mpango kazi wa utekelezaji (Action Plan for National Scale-Up of Integrated HIV and NCD Services and Mental Health (2025-2027). Utekelezaji wa mpango kazi umeanza katika mikoa ya Dar es Salaam,

Pwani, Kagera na Kigoma ambapo katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya WAVIU 317,335 walifanyiwa uchunguzi na kati yao WAVIU 13,777 walibainika kuwa na shinikizo la juu la damu na kuanzishiwa matibabu.

**79.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora kwa wagonjwa wa Kisukari na Shinikizo la Damu na Selimundu, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais -TAMISEMI imewajengea uwezo watoa huduma 427 kutoka katika Vituo vya kutolea huduma za Afya kuanzia ngazi ya Hospitali ya Taifa hadi ngazi ya afya ya Msingi pamoja na kwenye kambi za wakimbizi.

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuhakikisha upatikanaji wa **vipimo na dawa za kukabiliana na ugonjwa wa kisukari na magonjwa mengine yasiyoambukiza**. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 Wizara ilisambaza mashine 710 na vitendanishi 355,000 vya uchunguzi wa kisukari katika vituo vya afya vya umma 710 nchi nzima kwa ajili ya uchunguzi na ufuatiliaji wa huduma za kisukari. Aidha, Wizara imesambaza dawa za kisukari ikiwemo *Metformin* vidonge milioni 4.5 na *insulin vichupa* 395,000 kwa watoto na vijana wanaoishi na ugonjwa wa kisukari. Mafanikio haya yamewezesha watu wengi zaidi kuzifikia huduma karibu na maeneo yao.

81. ***Mheshimiwa Spika,*** uwekezaji mkubwa katika mapambano dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza umechangia kuongezeka kwa wagonjwa wanaoibuliwa mapema kwenye vituo vya kutolea huduma za afya na kwenye jamii na hivyo **kupunguza vifo** vitokanavyo na magonjwa hayo. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, idadi ya vifo vilivyotokana na shinikizo la damu vinavyoripotiwa katika mfumo wa takwimu za afya nchini (DHIS-2) vimepungua kutoka vifo 502 hadi vifo 439 sawa na punguzo la asilimia 12 la vifo vitokanavyo ugonjwa huo kipindi kama hicho mwaka 2024.

82. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Machi 2025 jumla ya vituo 73 vimesajiliwa kutoa huduma ya kuchuja damu katika mikoa yote nchini kupitia hospitali za rufaa za mikoa, hospitali za rufaa za kanda, Hospitali Maalum, hospitali ya Taifa na hospitali binafsi. **Uwepo wa huduma za kuchuja damu karibu na wananchi** kumeokoa maisha na kupunguza gharama za matibabu kwa wagonjwa wenye uhitaji. Aidha, Serikali kupitia Bohari ya Dawa (MSD) imeendelea kuwekeza kwenye huduma za figo nchini kwa kuongeza mashine 137 za kuchuja damu katika hospitali 15 za umma na kuhakikisha upatikanaji wa vifaa vinavyotumika katika huduma za kuchuja damu kwa bei nafuu. Vilevile, Serikali imeendelea kuimarisha huduma za upandikizaji figo ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2025 jumla ya wagonjwa 155 walipatiwa huduma ya upandikizaji figo.

83. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, **jumla ya wagonjwa wa Saratani 11,801 wapya walibainika** na kuanza matibabu katika Taasisi ya Saratani Ocean Road, Hospitali ya KCMC, Hospitali ya Rufaa ya Kanda Benjamin Mkapa, Hospitali ya Rufaa ya Kanda Bugando, Hospitali ya Taifa Muhimbili na Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya. Ili kuimarisha utoaji wa huduma, Serikali inafanya upanuzi wa huduma za matibabu na uchunguzi wa Saratani kwa kuongeza majengo na mashine za tiba mionzi kwenye Taasisi ya Saratani Ocean Road, Bugando, KCMC, Hospitali ya Kanda Mbeya na Hospitali ya Benjamin Mkapa.

84. ***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania ni miongoni mwa nchi tano duniani zinazoongoza kwa idadi kubwa ya ugonjwa wa Selimundu ambapo **asilimia 15 ya watanzania wanaishi na vinasaba vya ugonjwa huo**. Katika kudhibiti ugonjwa huu, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeanzisha kampeni Maalum ya elimu ya ugonjwa wa Selimundu na kampeni ya **vunja mduara** ambayo inalenga vijana kutambua hali zao ya vinasaba. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya **vijana 10,601 kutoka katika Mikoa ya Mwanza, Morogoro, Pwani, Mara, Arusha, Dodoma, Dar es Salaam na Tabora walipatiwa elimu na fursa ya kupima vinasaba vya ugonjwa wa Selimundu**. Aidha, Wizara pia ilitoa elimu ya ugonjwa adimu wa Himofilia kwa wazazi, walezi na wagonjwa 1,690 katika Mikoa ya Morogoro, Manyara, Tanga na Arusha.

85. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea na upimaji wa ugonjwa wa Selimundu kwa watoto wachanga ambapo katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya **watoto wachanga 3,171 walipimwa vinasaba vya ugonjwa wa Selimundu** ili kubaini ugonjwa katika hatua za awali. Aidha, hadi sasa jumla ya Wagonjwa 34,220 wa Selimundu wanaendelea kupatiwa matibabu ambapo zaidi ya asilimia 60 ya wagonjwa hawa wanapata matibabu kwa kutumia dawa ya *Hydroxyurea* na wagonjwa 11 wa Selimundu walipandikizwa uloto katika Hospitali ya Benjamin Mkapa. Kupanuka kwa huduma za Hemofilia na Selimundu kutapunguza vifo vya watoto chini ya miaka mitano vinavyotokana na magonjwa haya.

86. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia uwekezaji mkubwa wa Serikali katika kuboresha huduma za macho nchini ikiwemo uwekezaji kwenye rasilimali watu, miundombinu pamoja na mifumo ya ukusanyaji wa taarifa; **jumla ya watu 745,668 walifanyiwa uchunguzi wa macho** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 ambapo watu 21,723 walifanyiwa upasuaji wa macho. Katika kipindi hicho, magonjwa yaliyoongoza kwa wagonjwa wa nje wa macho ni pamoja na Mzio (Asilimia 40.1), Mtoto wa Jicho (Asilimia 15) na Shinikizo la juu la macho (Asilimia 11.4). Vilevile, asilimia **43.8 ya mahudhurio ya wagonjwa wa macho yalisababishwa na upeo mdogo wa macho** kuona unaorekebishika kwa miwani, ambapo jumla ya watu 45,058 walipatiwa

huduma ya miwani tiba, sawa na asilimia 66.3 ya waliokutwa na uhitaji wa miwani.

87. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 Wizara imejengea uwezo walimu na wanafunzi 250 kuhusu matatizo ya afya ya akili na elimu ya kukinga na kuzuia kujiua. Aidha, zaidi ya vijana 100,000 walijengewa uwezo kupitia elimu na midahalo iliyotolewa kwenye mitandao ya kijamii. Vilevile, katika kipindi hicho, watumishi 350 kutoka taasisi za umma walipatiwa elimu ya afya ya akili mahali pa kazi.

88. ***Mheshimiwa Spika*****,** Wizara inaendelea na **uboreshaji wa Huduma za Kinywa na Meno na** katika kipindi cha Julai 2024 mpaka Machi 2025, imefanya ununuzi na kusambaza mashine 13 za CT-Scan Maalum za kinywa na meno zenye thamani ya Shilingi 3,599,900,000.00 zilizopelekwa katika Hospitali za Rufaa za Kanda za Chato na Kusini - Mtwara pamoja na Hospitali za Rufaa za Mikoa za Dodoma, Iringa, Manyara, Sekou Toure-Mwanza, Songea, Bombo, Singida, Mawenzi, Temeke, Bukoba na Hospitali ya Jeshi Lugalo. Mpaka sasa ni asilimia 66.7 ya Hospitali za Rufaa za Mikoa na asilimia 33.3 ya Hospitali za Rufaa za Kanda zenye Mashine hii. Hadi kufikia Machi 2025 jumla ya mashine Maalum za x-ray ya kinywa zipatazo 57 zenye thamani ya Shilingi 4,354,800,000.00 zimewasili Bohari ya Dawa (MSD) ambapo tayari Hospitali za Halmashauri 20 (sawa na asilimia 10.9) zimeshapokea mashine hiyo. Hospitali hizo ni

Hospitali ya Manispaa ya Morogoro, Hospitali za Halmashauri ya Wilaya Morogoro, Mvomero, Kilosa, Ulanga, Chalinze-Msoga, Mbarali, Igunga, Tanganyika, Kilwa, Sikonge, Urambo, Muheza, Kasulu, Rombo, Bukoba, Mkomaindo-Masasi, Hospitali ya Uhuru-Chamwino na Hospitali ya Mbagala-Temeke na Kituo cha Afya Kaloleni-Arusha. Serikali pia imesambaza mashine za X-ray maalum za meno 48 kwenye Hospitali za Wilaya 6 na vituo vya afya 38. Mpaka sasa asilimia 100 ya hospitali za Rufaa za Kanda, Mikoa na Taifa, asilimia 80 ya Hospitali za Halmashauri na asilimia 30 ya Vituo vya Afya zina X-ray maalum za meno. Vilevile, Wizara imeendelea kusambaza *Dental Chairs* 114 kwenye Hospitali za Halmashauri 25 na vituo Vya Vfya 85.

***89.*** ***Mheshimiwa Spika,*** kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya wagonjwa 571,566 walipatiwa matibabu ya kinywa na meno nchini, kati yao wagonjwa 385,633 sawa na asilimia 67.4 walikuwa na tatizo la kuoza kwa meno, wagonjwa 54,155 sawa na asilimia 9.4 walikuwa na tatizo la magonjwa ya fizi na wengine walikuwa na matatizo mengine ya kinywa na meno. Kati ya wagonjwa wenye tatizo la kuoza meno, 159,300 sawa na asilimia 41.3 walipewa matibabu ya kuziba meno. Aidha, kumekuwa na ongezeko kubwa la Watanzania wanaoziba meno kutoka asilimia 35.6 mwaka 2024 hadi asilimia 41.3 mwaka 2025 ambapo ongezeko hili limechangiwa na uwekezaji mkubwa wa eneo la kinywa na meno unaofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita.

***Nasisitiza kuwa dawa ya jino siyo kung'oa, jino linatibika na kupona kabisa.***

***90.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu utoaji wa huduma za utengamao kwa watu wenye ulemavu na wenye mahitaji Maalum wakiwemo watoto na wazee. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, **jumla ya wagonjwa 237,174 walipatiwa huduma.** Aidha, katika kipindi hiki huduma zifuatazo zilitolewa; Fiziotherapia wateja 196,766, tiba kazi (Occupational Therapy) wateja 34,029, Matamshi na Lugha (Speech and Language Therapy) wateja 1,685, Vifaa Tiba Saidizi (Assistive Devices) wateja 2,019 na Viungo tiba na vifaa tiba saidizi (Prosthesis and Orthosis) wateja 5,028.

***91.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 **hospitali za Rufaa za Mikoa saba (7) zimeweza kutoa seti tatu (3) kati ya nne (4) ya huduma za utengamao** ambazo ni *Fiziotherapia, Occupational Therapy* na *Prosthesis and Orthosis.* Hospitali hizo ni Hospitali za Rufaa za Mikoa Dodoma, Tumbi, Iringa, Songea, Maweni, Katavi na Simiyu. Aidha, Wizara inaendelea kujenga uwezo kwenye Hospitali za Rufaa za Mikoa zilizobaki.

***92.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, **imeanzisha klabu 32 za afya za wazee (Healthy Ageing Club)** katika Mikoa ya

Ruvuma (9), Mbeya (8), Tanga (7) na Dodoma (8) kwenye ngazi za Kata. Lengo la klabu hizi za afya za wazee ni kuhamasisha wazee kufanya mazoezi ya pamoja, kujifurahisha na kupinga tabia bwete ili kujilinda na magonjwa yasiyoambukiza na magonjwa ya uzeeni.

***93.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya hospitali nane (8) zilifanya upimaji wa usikivu kwa watoto wachanga ili kubaini tatizo la ulemavu wa kusikia. Hospitali hizo ni Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali za Rufaa za Kanda Benjamin Mkapa, Bugando na Mbeya pamoja na Hospitali za Rufaa za Mikoa za Dodoma, Tumbi, Bombo na Mtakatifu Francis Ifakara. Katika kipindi hiki, jumla ya watoto wachanga 3,163 walipimwa usikivu mara baada ya kuzaliwa na kati yao, 232 walionekana kuhitaji uchunguzi zaidi.

**Huduma za Tiba**

***94.*** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuhakikisha wananchi wake wanapata huduma bora za afya zinazotolewa na watoa huduma wenye weledi na ujuzi, pamoja na uboreshaji wa miundombinu ya vituo vilivyopo, Wizara imeendelea kujenga vituo vipya ili kuleta huduma karibu na wananchi. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 vituo vya kutolea huduma za afya nchini vimeongezeka hadi kufikia 12,846 kutoka vituo 12,266 vilivyokuwepo kipindi kama hicho mwaka 2024 ikiwa ni ongezeko la vituo 580. Kati ya vituo

hivyo 12,846, Vituo vya umma vilikuwa 7,627 na binafsi ni 5,219. **(Kielelezo Na1. Kinaonesha Idadi na Mgawanyo wa Vituo vya Kutolea Huduma za Afya nchini)**




***Kielelezo Na. 1. Idadi na Mgawanyo wa Vituo vya Kutolea Huduma za Afya nchini.***

***95.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi, 2025, Wizara **imeendelea kuboresha mazingira ya kutolea huduma za afya kwa wananchi** katika vituo vya kutolea huduma za afya ambapo vitanda vimeongezeka kutoka 145,374 hadi kufikia vitanda 153,683. Hivyo kufanya uwaino wa vitanda 2.1 kwa kila watu 1,000 ukilinganisha na Mwongozo wa Shirika la Afya Duniani (WHO) unaoelekeza kuwa na uwiano wa vitanda 2.5 kwa kila watu 1,000. Aidha, kati ya vitanda 153,683 vitanda 49,285 vipo katika ngazi ya Hospitali, vitanda 30,937

vipo katika Vituo vya Afya, vitanda 71,102 vipo katika Zahanati na vitanda 2,359 vinapatikana katika kliniki na vituo vinginevyo nchini, kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 1** hapa chini.

***Jedwali Na. 1. Mchanganuo wa Idadi ya Vitanda*.**

| | **Vivyohitajika** | **Vilivyopo wodini** | **Vitanda vya kujifungulia** | **Vitanda vya uchunguzi** | **Jumla ya Vitanda** |
|---|---|---|---|---|---|
| Hospital | 58,802 | 43,664 | 1,709 | 3,912 | 49,285 |
| Vituo vya Afya | 35,119 | 24,051 | 2,851 | 4,035 | 30,937 |
| Zahanati | 73,711 | 36,906 | 15,156 | 19,040 | 71,102 |
| Kliniki | 2,030 | 1,211 | 112 | 1,036 | 2,359 |
| Jumla | **169,662** | **105,832** | **19,828** | **28,023** | **153,683** |

***96.*** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kusimamia utoaji wa huduma za matibabu kwa wananchi ambapo, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, **jumla ya mahudhurio 39,386,226 ya wananchi** walipata huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya hapa nchini ikilinganishwa na wateja 38,031,200 waliopata huduma kipindi kama hiki mwaka 2024. Kati yao, asilimia 8.2 walipata huduma katika ngazi ya Hospitali ya Taifa, Hospitali Maalum na Hospitali za Rufaa za Kanda, asilimia 11 ngazi ya Hospitali za Rufaa za Mikoa, asilimia 15.9 Hospitali za Wilaya, asilimia 20.8 vituo vya afya na asilimia 37.5 katika ngazi ya Zahanati, asilimia 4 ngazi ya Kliniki, asilimia 0.10 *Maternity and Nursing Home* na asilimia 2.4 ni vituo vinginevyo. Takwimu za utoaji wa huduma za afya zinaonesha kwamba **wananchi**

**asilimia 81 wanapata huduma katika ngazi ya afya ya msingi**, hali hiyo inaonesha juhudi kubwa zilizofanywa na Serikali katika uwekezaji na uimarishaji wa huduma katika ngazi ya afya ya msingi na kuleta huduma karibu na wananchi **(Jedwali Na. 2)**.

***Jedwali Na. 2. Idadi ya Wagonjwa Katika Vituo vya Huduma za Afya, Julai 2024 hadi Machi 2025.***

| AINA YA KITUO CHA HUDUMA | WAGONJWA WA NJE (OPD) | WAGONJWA WA KULAZWA (IPD) | JUMLA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| Taifa, Maalum na Kanda | 2,753,942 | 487,412 | 3,241,354 | 8.2% |
| Rufaa ngazi ya Mkoa | 3,974,663 | 363,423 | 4,338,086 | 11.0% |
| Rufaa ngazi ya Wilaya | 5,728,111 | 515,158 | 6,243,269 | 15.9% |
| Vituo vya Afya | 7,747,809 | 454,788 | 8,202,597 | 20.8% |
| Zahanati | 14,763,996 | 10,451 | 14,774,447 | 37.5% |
| Kliniki | 1,590,716 | 101 | 1,590,817 | 4.0% |
| Nyinginezo | 940,058 | 20,343 | 960,401 | 2.4% |
| Vituo vya Kujifungulia | 35,255 | | 35,255 | 0.1% |
| | **37,534,550** | **1,851,676** | **39,386,226** | |

97. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 **magonjwa yaliyoongoza kwa wagonjwa wa nje (OPD) wenye umri chini ya miaka mitano** yalikuwa ni maambukizi katika mfumo wa hewa (Asilimia 37.6), Malaria (Asilimia 9.2) na Kuhara pasipo upotevu wa maji (Asilimia 9.1). Katika umri wa miaka mitano na zaidi magonjwa yaliyoongoza yalikuwa ni maambukizi katika mfumo

wa hewa (Asilimia 17.3) na maambukizi katika njia ya mkojo (Asilimia 15.4). **(Jedwali Na. 3)**

***Jedwali Na. 3. Mchanganuo wa Idadi ya Mahudhurio ya nje (OPD) kwa magonjwa yote katika ngazi za zote Huduma za Afya.***

| Wagonjwa wa nje wenye umri zaidi ya miaka mitano | | | Wagonjwa wa nje wenye umri chini ya miaka mitano | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Aina ya ugonjwa** | **Idadi** | **Asilimia** | **Aina ya ugonjwa** | **Idadi** | **Asilimia** |
| Maambukizi katika Mfumo wa Hewa | 3,640,510 | 17.3 | Maambukizi katika Mfumo wa Hewa | 4,521,142 | 37.6 |
| Maambukizi katika Njia ya mkojo | 3,247,002 | 15.4 | Malaria (BS +ve, Clinical, mRDT +ve) | 1,103,491 | 9.2 |
| *Other Diagnosis* | 1,705,269 | 8.1 | Kuhara pasipo upotevu wa maji | 1,089,108 | 9.1 |
| Shinikizo la juu la Damu | 1,366,693 | 6.5 | Maambukizi katika Njia ya mkojo | 816,782 | 6.8 |
| Malaria (BS +ve, Clinical, mRDT +ve) | 1,247,270 | 5.9 | *Other Diagnosis* | 769,669 | 6.4 |
| *Peptic Ulcers* | 870,143 | 4.1 | *Other Non-Infectious GIT Diseases* | 505,666 | 4.2 |
| *Other Non-Infectious GIT Diseases* | 727,340 | 3.5 | Kichomi kisicho kikali - NonSevere | 398,394 | 3.3 |
| Kisukari | 617,999 | 2.9 | Kuhara na upotevu wa maji | 306,644 | 2.6 |
| *Rheumatoid and Joint Diseases* | 475,324 | 2.3 | Magonjwa ya ngozi - *Fungal* | 261,731 | 2.2 |
| Magonjwa ya ngozi - *Fungal* | 366,455 | 1.7 | Minyoo ya tumbo | 231,350 | 1.9 |

**98. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi hiki magonjwa yaliyoongoza kwa wagonjwa waliolazwa (IPD) wenye umri chini ya miaka mitano yalikuwa ni Magonjwa ya mfumo wa hewa (asilimia 51.6) na magonjwa ya mfumo wa mkojo (asilimia 9.3). Aidha, magonjwa yaliyoongoza kwa wenye umri wa miaka mitano na zaidi yalikuwa ni magonjwa ya mfumo wa hewa (asilimia 21.1) na magonjwa ya mfumo wa mkojo (asilimia 18.9) kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 4**.

***Jedwali Na. 4. Magonjwa yaliyoongoza kwa wagonjwa wa kulazwa chini ya umri wa miaka mitano na umri zaidi ya miaka mitano.***

| **Wagonjwa wa kulazwa wenye umri zaidi ya Miaka Mitano** | | | **Wagonjwa ya kulazwa wenye umri chini ya Miaka Mitano** | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Aina ya Ugonjwa** | **Idadi** | **%** | **Aina ya Ugonjwa** | **Idadi** | **%** |
| Magonjwaya mfumo wa hewa | 3,640,510 | 21.1 | Magonjwa ya mfumo wa hewa | 521,142 | 51.61 |
| Magonjwa ya mfumo wa mkojo | 3,247,002 | 18.9 | Magonjwa ya mfumo wa mkojo | 816,782 | 9.32 |
| *Other Diagnosis* | 1,705,269 | 9.9 | *Other Diagnosis* | 769,669 | 8.79 |
| Shinikizo la juu la damu | 1,366,693 | 7.9 | Magonjwa ya Ngozi-Non-Fungal | 410,569 | 4.69 |
| Vidonda tumbo | 870,143 | 5.1 | Kichomi kisicho kikali | 398,394 | 4.55 |
| Kisukari | 617,999 | 3.6 | Magonjwa ya ngozi - *Fungal* | 261,731 | 2.99 |
| *Rheumatoid and Joint Diseases* | 475,324 | 2.8 | Kichomi kikali | 186,159 | 2.12 |
| Magonjwa ya ngozi - *Fungal* | 366,455 | 2.1 | Magonjwa ya Ngozi-*Non-Infectious* | 165,254 | 1.89 |
| Upungufu wa damu | 324,115 | 1.9 | Upungufu wa damu | 153,145 | 1.75 |

| Wagonjwa wa kulazwa wenye umri zaidi ya Miaka Mitano | | | Wagonjwa ya kulazwa wenye umri chini ya Miaka Mitano | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Aina ya Ugonjwa** | **Idadi** | **%** | **Aina ya Ugonjwa** | **Idadi** | **%** |
| Magonjwa akina Mama | 303,125 | 1.8 | *Acute Ear Infection* | 115,023 | 1.31 |

## UIMARISHAJI WA HUDUMA ZA MATIBABU YA UBINGWA NA UBINGWA BOBEZI

***99.*** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kufanya uwekezaji mkubwa katika kuimarisha upatikanaji wa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi katika hospitali **za Rufaa za Mikoa, Hospitali za Rufaa za Kanda, Hospitali Maalum na Hospitali ya Taifa** kwa lengo la kusogeza huduma hizi kwa wananchi na kuhakikisha wananchi wengi zaidi wanapata huduma nchini kwa wakati na kwa gharama nafuu bila kuhitajika kuzifuata nje ya nchi. Aidha, uwekezaji huu unatoa fursa kwa wagonjwa kutoka nje ya nchi kupata huduma na kukuza dhana ya tiba utalii.

***100.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, **jumla wa wagonjwa 7,579,440** walipatiwa huduma katika hospitali hizo. Kati ya wagonjwa hao, wagonjwa wa nje (OPD) walikuwa **6,728,605** na wa ndani (IPD) walikuwa **850,835** Aidha, Wizara imeendelea kuhakikisha **wananchi wasio na uwezo wanapata huduma za afya kwa kupitia utaratibu wa misamaha** mbalimbali inayotolewa na Hospitali. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Hospitali za kitaifa, Hospitali

maalum, Hospitali za rufaa za kanda na mikoa zimeweza kutoa huduma za afya kwa njia ya **msamaha zenye thamani ya Shilingi** 34,720,233,085.28 **kwa wagonjwa 268,244** waliopatiwa huduma hizo katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, Kanda, Maalum na Taifa**.** Huduma zilizoongoza kutolewa misamaha ni huduma za uchujaji damu (Dialysis), huduma za mionzi kwa wagonjwa wa saratani, vipimo vya maabara, huduma za radioiojia, huduma za upasuaji, gharama za kumuona daktari, dawa na huduma za wagonjwa mahututi (ICU).

***101.*** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kufanya uwekezaji mkubwa katika kuimarisha upatikanaji wa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi katika hospitali **za Rufaa za Mikoa, Hospitali za Rufaa za Kanda, Hospitali Maalum na Hospitali ya Taifa** kwa lengo la kusogeza huduma hizo kwa wananchi na kuhakikisha wananchi wengi zaidi wanapata huduma nchini kwa wakati na kwa gharama nafuu bila kulazimika kuzifuata nje ya nchi. Aidha, uwekezaji huu unatoa fursa kwa wagonjwa kutoka nje ya nchi kupata huduma na kukuza dhana ya tiba utalii.

***102.*** ***Mheshimiwa Spika***, baadhi ya huduma za ubingwa na ubingwa bobezi zilizoendelea kutolewa ni pamoja na upandikizaji wa figo (Wagonjwa 21) , upandikizaji wa vifaa vya usikivu (Wagonjwa 16), upandikizaji wa uloto (Wagonjwa 7), upandikizaji wa meno (Wagonjwa 64), upasuaji wa kupunguza uzito

(Wagonjwa 13), upasuaji wa nyonga na goti (Wagonjwa 320), tiba mionzi (Wagonjwa 152,287), tiba kinga (Wagonjwa 42), upandikizaji wa mimba (Wanawake 8), upasuaji wa Moyo bila kufungua kifua (Wagonjwa 3,103), Upasuaji wa moyo kwa kufungua kifua (Wagonjwa 1,086), upasuaji wa ubongo (Wagonjwa 89), tiba ya saratani ya mlango wa kizazi (Wagonjwa 527,606), tiba ya saratani ya matiti (546,993), kuwekewa Puto tumboni (Wagonjwa 153), kuchuja damu (Wagonjwa 1,095) na radiolojia tiba (Wagonjwa 264).

***103. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, **huduma mpya** za ubingwa bobezi zilizoanzishwa katika hospitali za umma ni pamoja na upandikizaji wa mimba, upasuaji na uchunguzi wa kichwa na ubongo bila kufungua fuvu, upasuaji wa mgongo kwa kufungua eneo dogo, upasuaji wa kuondoa uvimbe kwenye ubongo kupitia tundu la pua na upandikizaji meno.

***104. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuhakikisha **upatikanaji wa huduma angalau nane (8) za msingi za ubingwa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa**. Huduma hizo zinahusisha akina mama na uzazi, watoto, upasuaji, upasuaji wa mifupa, tiba ya ndani, dawa za usingizi na ganzi, radiolojia na dharura. Aidha, idadi ya madaktari bingwa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa imeongezeka kutoka 321 Machi 2024 hadi kufikia 431 Machi 2025 sawa na ongezeko la asilimia 25. Hadi kufikia Machi 2025, Hospitali 15 sawa na asilimia 54 zimefikisha lengo la

kutoa huduma za fani nane (8) za kibingwa ikilinganishwa na Hospitali nane (8) katika kipindi kama hiki mwaka 2024.

105. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, **Hospitali za Rufaa za Mikoa zimeendelea kuimarisha huduma za ubingwa kwa kuanzisha huduma mpya za ubingwa** katika fani za magonjwa ya macho, mfumo wa mkojo, afya ya akili, masikio, pua na koo, kuchuja damu (dialysis), magonjwa ya ngozi, saratani na magonjwa ya mfumo wa chakula ambapo wagonjwa 10,898 walihudumiwa na kati ya hao, 944 walipata huduma ya kuchuja damu katika Hospitali za Rufaa za Mikoa 13. Huduma hizi zimeanzishwa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa ya Kagera, Geita, Iringa, Katavi, Mtwara, Manyara, Kigoma, Kilimanjaro, Morogoro, Arusha, Njombe, Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Lindi, Songwe na Pwani.

106. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia kampeni ya **Madaktari Bingwa wa Dkt. Samia** zaidi ya Madaktari 250 kutoka katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, Hospitali za Rufaa za Kanda, Hospitali ya Taifa na Hospitali Maalum wa fani za kibingwa zaidi ya 14 walishiriki kutoa huduma katika kambi za madaktari bingwa na ubingwa bobezi nchini. Lengo kuu la kampeni hii ni kufikisha huduma za ubingwa na ubingwa bobezi karibu na wananchi, kupunguza gharama za huduma za kibingwa na kujenga uwezo wa wataalam wa afya katika utoaji wa huduma za

ubingwa na bobezi zenye ubora. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya wagonjwa 99,888 walihudumiwa kupitia kambi za madaktari bingwa wa Dkt. Samia zilizofanyika katika Halmashauri na katika Hospitali za Rufaa za Mikoa sita (6) ya Iringa, Rukwa, Mara, Njombe, Dar es Salaam na Kilimanjaro*.* Kati ya wagonjwa hao, 5,998 walipatiwa huduma za upasuaji, 3,563 walipata rufaa kutoka ngazi ya msingi kwenda Hospitali za Rufaa za Mikoa na 258 walipatiwa rufaa kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa kwenda kupata matibabu zaidi katika Hospitali za Kanda na Taifa.

***107.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya **wataalam 4,638** wa kada mbalimbali waliopo katika vituo vya ngazi ya msingi wamepatiwa mafunzo elekezi na kujengewa uwezo katika kutoa huduma za ubingwa wakati wa kambi za madaktari bingwa wa Dkt. Samia. Maeneo mahususi waliyojengewa uwezo ni pamoja na huduma za magonjwa ya wanawake na afya ya uzazi, magonjwa ya ndani, magonjwa ya watoto, upasuaji, huduma za dawa ya usingizi na ganzi na huduma za afya ya kinywa na meno.

***'Naomba kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge kuhamasisha wananchi kujitokeza kwa wingi ili kufaidika na huduma hizi kipindi wataalam hawa wanapofika kwenye maeneo yetu'.***

***108.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuboresha **tiba utalii** nchini, Serikali imeimarisha huduma za ubingwa

bobezi katika Hospitali ya Taifa, Hospitali Maalum na Hospitali za Rufaa za Kanda nchini. Uimarishaji huu umewezesha wananchi kupata huduma na kuvutia wagonjwa kutoka nchi za nje hususan nchi za ukanda wa Afrika. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya wagonjwa 4,337 waliweza kupata huduma za ubingwa bobezi nchini katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Taasisi ya Mifupa - MOI, Taasisi ya Saratani -Ocean Road, Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), Saifee na Aga Khan. Wagonjwa hawa walitoka katika nchi za Comoro, Malawi, Burundi, Zambia, Rwanda, Afrika Kusini, Msumbiji, Congo DRC, Sudan, Uganda, Zimbabwe, Ethiopia, Somalia, Kenya, Egypt, na Mauritius. Huduma zilizotolewa kwa wagonjwa hao ni pamoja na huduma za moyo, mifupa, mifumo ya fahamu, figo na Saratani.

***109. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Wizara kupitia Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI), Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili (MOI), Taasisi ya Saratani -Ocean Road, Hospitali ya Benjamin Mkapa kwa kushirikiana na Wadau wa Sekta binafsi walikwenda nje ya nchi na kutoa **huduma Mkoba** (**outreach services**) kwa wagonjwa katika nchi za Malawi, Visiwa vya Comoro na Burundi pia kutangaza huduma za kibingwa na ubingwa bobezi zinazopatikana nchini. Jumla ya **wagonjwa 2,770** walihudumiwa katika kambi hizo. Utoaji wa huduma hizi ni mkakati maalum wa kutangaza huduma za tiba

utalii na kuimarisha diplomasia ya afya ya nchi Kimataifa.

### Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) – Upanga

**110.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili imetoa huduma kwa **wagonjwa 579,973** kati ya wagonjwa hao wagonjwa waliolazwa ni 254,881 na wagonjwa wa nje ni 325,092 ikilinganishwa na wagonjwa 354,926 waliohudumiwa katika kipindi kama hiki mwaka 2024 ikiwa ni ongezeko la asilimia 63.4. Aidha, hospitali ilitoa **msamaha kwa wagonjwa wasio na uwezo wa kumudu gharama** ambapo imetoa msamaha wenye thamani ya Shilingi 10,640,269,858 kwa wagonjwa 42,714 ikilinganishwa na msamaha wa Shilingi 10,653,345,520 kwa wagonjwa 46,307 kwa kipindi kama hicho mwaka 2024. Huduma zinazoongoza kutolewa misamaha ni pamoja na uchujaji wa damu (Dialysis), Wagonjwa mahututi (ICU), vipimo vya CT Scan na MRI pamoja na dawa.

**111.** ***Mheshimiwa Spika,*** Hospitali imeendelea kuimarisha huduma za ubingwa bobezi kwa **kuanzisha huduma mpya** ya kupandikiza mimba (IVF) ili kusaidia wanawake wenye changamoto ya kushika mimba kwa njia ya kawaida. Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya wanawake nane (8) walipatiwa huduma hizo, hivyo kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma hizi katika hospitali za umma sambamba na kupunguza gharama za huduma hiyo.

**112. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, huduma za ubingwa na ubingwa bobezi zimeendelea kutolewa ambapo upandikizaji wa figo kwa wagonjwa tisa (9) ulifanyika na hivyo kufanya jumla ya wagonjwa kufikia 90 tangu huduma hiyo ilipoanzishwa mwaka 2017. Vilevile, upandikizaji wa vifaa vya usikivu ulifanyika kwa wagonjwa 16, hivyo kufanya jumla ya wagonjwa kufikia 88 tangu huduma hiyo ilipoanzishwa mwaka 2017.

**113. *Mheshimiwa Spika*,** Hospitali imeendelea kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za afya kwa kufanya marekebisho kwenye majengo mbalimbali ikiwemo; majengo ya kutoa huduma na ofisi za utawala kwa gharama ya kiasi cha Shilingi 1,656,000,000 pamoja na kununua mashine za kisasa za usingizi kwa gharama ya Shilingi 650,000,000. Aidha, Wizara inaendelea kutekeleza mpango wa maboresho ya Hospitali ya Taifa Muhimbili kwa kushirikiana na Serikali ya Korea ambapo upembuzi yakinifu wa kufanya maboresho ya miundombinu ya Hospitali umekamilika.

**114. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Hospitali ya Taifa Muhimbili imeendelea kushirikiana na Taasisi za ndani na nje ya nchi ikiwemo Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu, Taasisi ya Afya Ifakara, *National Institute of Health* (NIH - Marekani) na *The Gates Foundation* (Marekani) katika tafiti mbalimbali

za kimatibabu. Kupitia tafiti hizo, Hospitali imetoa machapisho 382 ya masuala ya afya katika majarida mbalimbali.

115. ***Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, **Tiba Utalii** iliendelea kushika kasi ambapo wagonjwa 844 toka nchi mbalimbali (Comoro, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Mauritius na Zambia) walihudumiwa ikilinganishwa na wagonjwa 567 katika kipindi kama hiki mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 49.

**Hospitali ya Taifa Muhimbili - Mloganzila**

116. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Hospitali imetoa huduma kwa **wagonjwa 158,528,** kati ya wagonjwa hao, waliolazwa walikuwa 9,564 na wagonjwa wa nje ni 148,964 ikilinganishwa na wagonjwa 147,071 waliohudumiwa kwa kipindi kama hiki mwaka 2024 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 1.3. Aidha, Hospitali imeanzisha huduma mpya moja (1) ya ubingwa na ubingwa bobezi ya upandikizaji meno ambapo wagonjwa 64 walipatiwa huduma za upandikizaji wa meno bandia. Katika kipindi hicho hospitali ilitoa msamaha kwa wagonjwa 6,955 wasio na uwezo wa kumudu gharama za matibabu zenye thamani ya Shilingi 3,338,583,678.94. Huduma zinazoongoza kutolewa misamaha ni pamoja na uchujaji wa damu (Dialysis), Huduma za dharura (Emergency), ICU, vipimo vya *CT Scan, X-ray* na huduma za kulazwa.

117. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, huduma za **ubingwa bobezi zilizoendelea** kutolewa na Hospitali ni pamoja na huduma za kupunguza uzito kwa kupunguza ukubwa wa mfuko wa chakula kwa wagonjwa 13, huduma ya upasuaji rekebishi (Cosmetic Surgeries) ambapo wagonjwa 46 walifanyiwa upasuaji huo, huduma ya upasuaji wa nyonga na magoti kwa wagonjwa 117, Upandikizaji wa mfupa (Bone grafting) kwa wagonjwa 5 na huduma za upandikizaji meno (Dental Implant) kwa wagonjwa 64. Vilevile, wagonjwa 12 walipatiwa huduma ya upandikizaji wa figo na wagonjwa 153 walipatiwa huduma ya kuwekewa Puto Tumboni kwa ajili ya kupunguza uzito wa mwili.

118. ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali imeendelea kutoa **huduma za uchunguzi wa magonjwa** mbalimbali ambapo **vipimo 28,819** vya Radiolojia vilifanyika. Kati ya vipimo hivyo, MRI vipimo 3,093, CT scan vipimo 2,146, X-Ray vipimo 11,412, Ultrasound vipimo 11,504, Panorama vipimo 565 na Mammography vipimo 99. Jumla ya **vipimo vya maabara 288,288** vimefanyika kwa kutumia vifaa vya kisasa na upatikanaji wa bidhaa tiba ni asilimia 94.

119. ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali ya Mloganzila imeendelea **kuratibu mafunzo** ambapo katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, wataalam 86 wapo masomoni katika fani mbalimbali za ubingwa na ubingwa bobezi ndani na nje ya nchi kwa ufadhili wa Serikali. Hospitali imeendelea kutoa **huduma za**

**mkoba** (Outreach Services), ambapo kliniki za mkoba sita (6) zilifanyika na jumla ya wagonjwa 754 walipatiwa huduma za kibingwa, kati ya wagonjwa hao wagonjwa 43 walipatiwa huduma za upasuaji.

120. ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa **Tiba Utalii**, katika kipindi cha Julai 2024 hadi kufikia Machi 2025, wagonjwa 81 kutoka nchi za Comoro, Uganda, Sudan, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Kenya walipatiwa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi. Huduma walizopatiwa ni pamoja na upandikizaji wa nyonga na magoti bandia, huduma za kupunguza uzito kwa kuwekewa puto pamoja na huduma za uchunguzi kwa vipimo vya maabara na radiolojia.

### Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI)

121. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi 2025, Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) imetoa **huduma kwa wagonjwa 222,803** kati ya wagonjwa hao, waliolazwa ni 12,070 na wagonjwa wa nje ni 210,733. Taasisi imeweza kufanya huduma ya kuchunguza mishipa ya miguu kwa wagonjwa 86 na kuzibua mishipa ya miguu kwa wagonjwa 28. Huduma nyingine za **ubingwa na ubingwa bobezi zilizoendelea** kutolewa ni uchunguzi wa mishipa ya damu ya moyo kwa wagonjwa 1,305, kufunga vifaa visaidizi vya moyo kwa wagonjwa 115, kuzibua mishipa ya damu ya moyo kwa wagonjwa 244, kutibu hitilafu ya mfumo wa umeme wa moyo kwa wagonjwa 46, kuziba matundu ya moyo kwa Watoto

wagonjwa 64 na kuchunguza matatizo ya moyo kwa Watoto wagonjwa 80.

**122.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi hicho Hospitali ilitoa **msamaha** kwa wagonjwa 710 wasio na uwezo wa kumudu gharama za matibabu zenye thamani ya Shilingi 825,762,214 ikilinganishwa na gharama ya Shilingi 1,146,206,145 kwa wagonjwa 1,167 katika kipindi kama hiki mwaka 2024. Huduma zinazoongoza kutolewa misamaha ni pamoja na vipimo vya maabara, upasuaji wa moyo kwa njia ya tundu dogo na malazi kwa upande wa wagonjwa mahututi.

**123.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi 2025, Taasisi **imeendelea kutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi** za upasuaji wa moyo kwa kufungua kifua na mishipa ya damu kwa wagonjwa 455 na hivyo kufanya idadi ya wagonjwa waliopatiwa huduma hii kufikia 8,249 tangu kuanza kwa huduma hiyo mwaka 2015. Gharama ya kufanya upasuaji wa moyo kwa kufungua kifua na mishipa ya damu ni wastani wa Shilingi 15,450,000 kwa mgonjwa mmoja ndani ya nchi ikilinganishwa na wastani wa Shilingi 50,800,000 kwa mgonjwa mmoja akitibiwa nje ya nchi. Vilevile, Taasisi imefanikiwa kufanya upasuaji wa moyo kwa njia ya tundu dogo kwa wagonjwa 2,632 na hivyo kufanya idadi ya wagonjwa waliopatiwa huduma hii kufikia 36,022 tangu huduma hizo zilipoanza kutolewa. Gharama ya kufanya upasuaji huo katika Taasisi ni wastani wa Shilingi

6,000,000 kwa mgonjwa mmoja ikilinganishwa na wastani wa Shilingi 20,000,000 kwa mgonjwa mmoja akitibiwa nje ya nchi.

***124.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Taasisi imeendelea kutoa **huduma za uchunguzi** wa magonjwa ya moyo ambapo vipimo vya ECHO vilikuwa 23,023, *Holter* vilikuwa 2,710, *Stress ECG* vilikuwa 2,523, *Dobutamine* vilikuwa 132, *Stress ECHO* vilikuwa 35 na *Sparkle Traching ECHO* vilikuwa 732, *Transosophageal ECHO* vilikuwa 38, *X-Ray* vilikuwa 21,972 *Ultra Sound* vilikuwa 23,750, *ECG* vilikuwa 18,105, *Ultra Functional Test* vilikuwa 72 na *ABP* vilikuwa 1,528. Aidha, jumla ya **vipimo vya maabara** 405,258 vimefanyika kwa kutumia vifaa vya kisasa ikilinganishwa na vipimo 248,409 kipindi kama hiki mwaka 2024.

***125.*** ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali imeendelea kuratibu **mafunzo** ambapo katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, wataalam 62 wapo masomoni katika fani mbalimbali za ubingwa na ubingwa bobezi katika masuala ya moyo ndani na nje ya nchi. Taasisi imetumia jumla ya kiasi cha Shilingi 222,885,033 kutoka katika mapato yake ya ndani kuwalipia watumishi hao.

***126.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza ***Dkt. Samia Cardiac Outreach Program****,* Taasisi imeendelea kutoa **huduma za mkoba**, ambapo jumla ya wagonjwa 10,975 walifikiwa na hivyo kufanya jumla

ya wagonjwa waliopatiwa huduma tangu taasisi imeanza kutoa huduma za mkoba mwaka 2015 kufikia 46,788. Jumla ya wagonjwa 7,782 walipatiwa vipimo vya *ECHO* na *ECG* kupitia huduma hizo za mkoba na wagonjwa wapya 2,612 sawa na asilimia 33.5 waligundulika kuwa na magonjwa ya moyo.

***127. Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza dhana ya **Tiba Utalii** nchini, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete ilihudumia **jumla ya wagonjwa 518** kutoka nchi za Msumbiji, Comoro, Malawi, Zambia, Uganda, Kenya, Rwanda na Burundi. Aidha, Taasisi imehudumia wagonjwa kutoka mataifa mengine nje ya Bara la Afrika ikiwemo Norway, China, India, Poland na Marekani. Vilevile, kutokana na kuimarika kwa huduma za ubingwa za upasuaji wa moyo, Taasisi imezijengea uwezo nchi za Malawi, Rwanda na Zambia ili ziweze kutoa huduma hizo.

### Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI)

***128. Mheshimiwa Spika***, Taasisi ya Tiba ya Mifupa (MOI) katika kipindi cha mwezi Julai 2024 hadi Machi 2025 imetoa huduma kwa **jumla ya wagonjwa 168,483** ambapo wagonjwa waliolazwa ni 7,318 na wagonjwa wa nje ni 161,165 ikilinganishwa na wagonjwa 180,080 waliopatiwa huduma kwa kipindi hicho mwaka 2024. Katika kutekeleza dhana ya ubunifu na upanuzi wa huduma, Taasisi imeendelea kuhudumia wananchi kwa kuanzisha **huduma mpya** tatu (3) za kibobezi ambazo ni:- uchunguzi wa ubongo bila kufungua fuvu, upasuaji wa nyonga na magoti wa

marudio na huduma ya kutibu kiharusi. Uanzishwaji na uendelezaji wa huduma za matibabu ya kibingwa bobezi umefanikisha kupunguza rufaa za wagonjwa wa mifupa kwa asilimia 98 na ubongo kwa asilimia 97.

129. ***Mheshimiwa Spika***, huduma zingine za **ubingwa bobezi zilizoendelea kutolewa** na Taasisi ni pamoja na upasuaji wa nyonga, upandikizaji wa goti bandia, upasuaji wa vichwa vikubwa na mgongo wazi. Kupitia matibabu hayo yote ya huduma za ubingwa bobezi jumla ya wagonjwa 5,552 walihudumiwa kwa mafanikio makubwa na kuwezesha Serikali kuokoa Shilingi Bilioni 141 ambazo zingetumika iwapo wagonjwa hao wangepewa rufaa kwenda kutibiwa nje ya nchi.

130. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Taasisi ilitoa **msamaha** kwa wagonjwa 3,321 wasio na uwezo wa kumudu gharama za matibabu zenye thamani ya Shilingi 2,733,711,031.88 ikilinganishwa na gharama ya Shilingi 2,702,038,334 kwa wagonjwa 4,318 katika kipindi kama hiki mwaka 2024. Huduma zinazoongoza kutolewa misamaha ni pamoja na upasuaji na vipandikizi, mionzi, kulazwa, vipimo vya maabara pamoja na dawa.

131. ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza azma ya Serikali ya kutumia teknolojia ya kisasa kwenye utoaji wa huduma za afya, Taasisi imeanza kutoa huduma ya upasuaji wa ubongo na mishipa ya fahamu kwa

kutumia akili unde (Artificial Intelligence). Katika hatua ya kwanza **jumla ya wagonjwa 12** wamefanyiwa upasuaji kwa kutumia teknolojia hiyo. Hatua ya pili ni kuongeza wigo wa utoaji wa huduma kwa kufanya upanuzi wa vyumba vya kufanyia upasuaji ikiwa ni pamoja na kusimika mifumo ya kisasa ya kufanya upasuaji kwa kutumia roboti (Robotic Surgeries).

**132.** ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi imeendelea kutoa **huduma za uchunguzi** wa magonjwa mbalimbali ambapo vipimo 42,889 vya Radiolojia vilifanyika. Kati ya hivyo, vipimo vya MRI vilikuwa 7,133, CT scan vipimo 4,025, X-Ray vipimo 30,343 na Ultrasound vipimo 1,388. Aidha, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya **vipimo vya maabara** 88,779 vimefanyika kwa kutumia vifaa vya kisasa.

**133.** ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi ya Mifupa Muhimbili MOI imeendelea kuratibu **mafunzo** kwa wataalam ambapo katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, wataalam sita (6) wamepelekwa masomoni katika fani za ubingwa na ubingwa bobezi za upasuaji wa mifupa, ubongo na mishipa ya fahamu ndani na nje ya nchi.

**134.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza dhana ya **Tiba Utalii** nchini, Taasisi ilihudumia jumla ya **wagonjwa 203** kutoka nchi za Comoro, Msumbiji, Malawi, Zambia, Uganda, DRC na Rwanda. Aidha, Taasisi imehudumia wagonjwa kutoka mataifa mengine nje ya Bara la Afrika ikiwemo China na

Slovakia. Idadi hii imeongezeka kwa asilimia 68 ikilinganishwa na wagonjwa 121 waliohudumiwa katika kipindi kama hiki mwaka 2024. Hii inadhihirisha kuendelea kuimarika kwa ubingwa bobezi zinazotolewa na Taasisi ya Mifupa Muhimbili. Aidha, pamoja na kuimarisha huduma za tiba utalii, Taasisi imeendelea kutoa **huduma mkoba** katika maeneo mbalimbali nchini ambapo jumla ya wagonjwa 8,050 walipatiwa huduma na kati ya hao 6,162 walipatiwa huduma za kliniki na 1,888 walifanyiwa upasuaji.

***135.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha huduma na kupunguza msongamano wa wagonjwa, Taasisi inaendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa nne na ukarabati wa iliyokuwa Hospitali ya Tumaini kwa ajili ya kuhudumia wagonjwa wa nje. Aidha, katika kupunguza gharama za uendeshaji na ununuzi wa mitungi ya Oksijeni, Taasisi imekamilisha ujenzi wa kituo cha kuvuna hewa tiba ya oksijeni ambacho kwa sasa kinatumika.

## Taasisi ya Saratani Ocean Road

***136.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Taasisi ya Saratani Ocean Road ilihudumia **jumla ya wagonjwa 26,959** kati ya hao, wagonjwa wa nje ni 25,488 na waliolazwa 1,471. Huduma za ubingwa na ubingwa bobezi ambazo zimetolewa katika kipindi hiki ni pamoja na uchunguzi wa maabara, uchunguzi wa radiolojia, tiba mionzi nje,

tiba mionzi ndani, tiba kemia, tiba kinga na tiba nyuklia. Katika kipindi hicho, jumla ya wagonjwa 188 walitibiwa kwa tiba mionzi IMRT), wagonjwa 153 walitibiwa kwa tiba mionzi ya *3D Brachytherapy*, na wagonjwa 42 walitibiwa kwa tiba kinga.

***137.*** ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi imeendelea kutoa huduma za tiba mionzi (3D-CRT) ambapo kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya tiba mionzi 151,946 zimetolewa. Gharama ya matibabu haya ya kibobezi hapa nchini ni Shilingi 5,000,000 kwa mgonjwa mmoja ikilinganishwa na wastani wa Shilingi 12,000,000 kama mgonjwa akitibiwa nje ya nchi. Katika kuendelea kuimarisha ubora wa maisha kwa wagonjwa wa saratani, Taasisi imeendelea kutoa huduma za tiba shufaa ikiwemo dawa ya *Oral Morphine* kwa ajili ya kupunguza maumivu kwa wagonjwa 2,809 ikilinganishwa na wagonjwa 2,704 kwa mwaka 2024.

***138.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Taasisi ilitoa **misamaha kwa wagonjwa 3,868** wasioweza kumudu gharama za matibabu, yenye thamani ya Shilingi 3,286,270,154 ikilinganishwa na misamaha ya Shilingi 28,254,601,599.99 kwa wagonjwa 15,475 kwa kipindi hiki cha mwaka 2024. Huduma za misamaha zimepungua kutokana na wagonjwa wengi kutumia kadi za bima ya afya na pia kuweka utaratibu madhubuti kupitia Ofisi ya Ustawi wa Jamii katika kuchangia huduma. Huduma zinazoongoza kutolewa

misamaha ni tiba kemia, tiba mionzi, uchunguzi wa maabara, radiolojia na huduma za kulazwa.

**139.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 huduma za uchunguzi wa magonjwa mbalimbali zimeendelea kuimarika ambapo kwa upande wa radiolojia, vipimo 18,694 vilifanyika ikilinganishwa na vipimo 8,574 vilivyofanyika katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Kati ya vipimo hivyo, vipimo 7,128 ni vya X-Ray, 6,382 vya Ultrasound, 2,589 vya CT scan, 2,229 vya MRI na 366 vya mammograph. Kwa upande wa maabara jumla ya vipimo 171,930 vilifanyika ikilinganishwa na vipimo 158,607 vilivyofanyika katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Aidha, Taasisi imeendelea kushikilia ithibati ya kimataifa ya maabara kutoka Chombo cha Ithibati cha Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADCAS) iliyopatiwa tangu mwaka 2021. Hali ya upatikanaji wa dawa za saratani ni wastani wa asilimia 100.

**140.** ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi imekamilisha mradi wa PET/CT Scan na huduma zimeanza kutolewa, hadi sasa **jumla ya wagonjwa 231** wamefanyiwa uchunguzi kwa kutumia mashine hiyo. Aidha, mradi wa ujenzi wa Kituo cha Saratani Mbeya (ORCI Mbeya Cancer Centre) unaendelea ambapo kazi ya ujenzi wa ghorofa moja itakayokuwa na vyumba vya matibabu ya saratani, tiba kemia, tiba za dawa za nyuklia na kliniki za matibabu sasa umefikia asilimia 5. Kukamilika kwa mradi huo kutawezesha kuhudumia wagonjwa kutoka mikoa 11 na nchi jirani.

Vilevile, utekelezaji wa mradi wa Ujenzi wa Jengo la huduma jumuishi za saratani (Multi-purpose Oncology Hospital Building) kwa kutumia mapato ya ndani unaendelea na umefikia asilimia 35.

***141.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha huduma na kupunguza msongamano wa wagonjwa kusubiri huduma, Taasisi inaendelea na taratibu za ununuzi na usimikaji wa mashine nne (4) za kisasa za uchunguzi na tiba mionzi ya saratani ambazo ni *Linear Accelerator* kwa gharama ya Shilingi Billioni 8.08, mashine nyingine mbili (2) za *Cobalt - 60* kwa gharama ya Shilingi Billioni 4.4 na *C-Arm* kwa kushirikiana na Tume ya Kimataifa ya Nguvu za Atomiki kwa gharama ya Shilingi milioni 450.

***142.*** ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi imeendelea kusomesha wataalam wa kozi za ubingwa na ubingwa bobezi za muda mfupi, wataalam tisa (9) na za muda mrefu wataalam 11. Kozi hizo ni pamoja na *Radiology*, *Clinical Oncology*, *Haematology and Blood Transfusion*, *Women Imaging*, *Urology, Surgery, Gyanecology Oncology,* Famasia na *Medical Physicist*.

***143.*** ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi imehudumia jumla ya wateja 11,237 kupitia **huduma mkoba** katika mikoa sita (6) ya Dar es Salaam, Shinyanga, Tanga, Pwani, Simiyu, Dodoma na Zanzibar. Huduma zilizotolewa ni uchunguzi wa saratani ya matiti, mlango wa kizazi, ngozi, utumbo mpana na tezi dume.

**144.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza dhana ya **Tiba Utalii,** Taasisi imeendelea kuimarisha huduma ambapo kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Jumla ya wagonjwa 607 kutoka nje ya nchi walipatiwa huduma za uchunguzi na tiba ya saratani ikilinganishwa na wagonjwa 526 kwa kipindi kama hicho mwaka 2024. Wagonjwa hao walitoka katika nchi za Afrika ya Kusini, Malawi, Kenya, Comoro, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Msumbiji, Sudani ya Kusini, Zambia, Rwanda, Burundi na Uganda. Pia, Taasisi imehudumia raia wa kigeni waliotoka mataifa mengine nje ya Bara la Afrika ikiwemo Oman, Marekani, India, Pakistan na Bangladesh hali inayodhihirisha kuendelea kuaminiwa kwa Taasisi hii kwa wageni wanaotembelea au wanaoishi nchini.

**145.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha huduma kwa wagonjwa, **tafiti** mbalimbali za kimatibabu zimeendelea kufanyika ambapo kwa sasa Taasisi inafanya tafiti 15 kwa kushirikiana na Taasisi zingine ndani na nje ya nchi ikiwemo MUHAS, NIMR, *University of Zambia*, *University of California San Francisco* (UCSF) na *Lousiana State University* (LSU). Faida ya tafiti hizi ni kuongeza uelewa wa vyanzo vya magonjwa ya saratani, vihatarishi na matokeo ya matibabu ya saratani. Matokeo ya tafiti hizi yatakuwa na manufaa katika tiba ya saratani nchini. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya **machapisho ya kitafiti 22** yalifanyika katika majarida ya kimataifa.

146. ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi ya Saratani Ocean Road kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili iliendelea kutoa **mafunzo** kwa wanafunzi 170 katika fani za uchunguzi na Tiba ya Radiografia, Onkolojia na Uuguzi katika Onkolojia. Mafunzo hayo yameongeza idadi ya wataalam wa huduma za saratani nchini.

**Hospitali ya Benjamin Mkapa**

147. ***Mheshimiwa Spika*,** Hospitali imetoa huduma kwa **wagonjwa 209,080** kati ya hao, wagonjwa waliolazwa 10,158 na wagonjwa wa nje 198,922 ikilinganishwa na wagonjwa 191,528 katika kipindi kama hiki mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 9. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Taasisi ilitoa misamaha kwa wagonjwa 1,408 wasioweza kumudu gharama za matibabu, yenye thamani ya Shilingi 361,030,133 ikilinganishwa na Shilingi 279,943,046 kwa wagonjwa 1,463 katika kipindi kama hiki mwaka 2024. Huduma zinazoongoza kutolewa misamaha ni pamoja na uchujaji damu, vipimo vya maabara, wagonjwa mahututi, huduma za upasuaji na dawa.

148. ***Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 hospitali imeendelea kutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi ikiwemo; upandikizaji wa uloto kwa wagonjwa saba (7), upandikizaji figo kwa wagonjwa kumi (10), uvunjaji wa mawe kwenye mfumo wa mkojo kwa wagonjwa 75, upasuaji wa nyonga na magoti kwa wagonjwa 125, Upasuaji wa

ubongo na mishipa ya fahamu kwa wagonjwa 77 na upasuaji wa moyo kwa kutumia mtambo maalum wa *Cathlab* kwa wagonjwa 472.

***149. Mheshimiwa Spika*,** katika kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma za upandikizaji mimba, Hospitali ya Benjamin Mkapa inaendelea na maandalizi ya utoaji wa huduma hii, hadi sasa Wataalam watatu wanamalizia masomo yao ya kupata ujuzi zaidi kuhusu upandikizaji mimba katika vyuo vya nje ya nchi (India na Scotland). Aidha, ukarabati wa eneo maalum la kufanyia upandikizaji unaendelea na mpaka sasa utekelezaji umefikia asilimia 43.

***150. Mheshimiwa Spika*,** Hospitali imeendelea kutoa **huduma za uchunguzi** wa magonjwa mbalimbali ambapo vipimo 65,777 vya Radiolojia vilifanyika. Kati ya vipimo hivyo MRI vilikuwa 3,956, *CT scan* vipimo 3,857, *X-Ray* vipimo 22,682, Fluoroscopy 1239, Mammography 181 na *Ultrasound* vipimo 33,862. Aidha, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya vipimo vya maabara 330,320 vimefanyika kwa kutumia vifaa vya kisasa na hali ya upatikanaji wa dawa ni asilimia 98.

***151. Mheshimiwa Spika*,** katika kuongeza uwezo wa Taasisi kutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi kwa hadhi ya hospitali ya Kanda na Taifa, Hospitali imeendelea kuratibu **mafunzo** kwa wataalam ambapo katika kipindi cha Julai 2024 hadi

Machi 2025, jumla ya wataalam 55 wapo masomoni katika fani mbalimbali za ubingwa na ubingwa bobezi ndani na nje ya nchi.

***152.*** ***Mheshimiwa Spika*****,** Hospitali ilizipeleka huduma za ubingwa na ubingwa bobezi kwa utaratibu wa **huduma mkoba** katika mikoa mbalimbali, ambapo katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya wagonjwa 5,440 walifikiwa. Kati ya hao 3,509 walipatiwa huduma za Macho, 200 huduma za Mifupa na ajali, 223 huduma ya koo, masikio na pua, 149 huduma ya upasuaji wa mishipa ya fahamu na ubongo, 208 huduma za mfumo wa mkojo na uzazi kwa wanaume, 389 matibabu ya magonjwa ya ndani, 250 matibabu ya magonjwa ya moyo, 248 matibabu ya saratani, 166 matibabu ya meno na 98 walipatiwa matibabu ya figo.

***153.*** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Hospitali ya Benjamin Mkapa imefanya **tafiti** mbili (2) ambazo zipo katika mchakato wa kuchapishwa (publication). Aidha, Hospitali inatarajia kukamilisha tafiti nyingine nne katika maeneo ya magonjwa ya figo, damu, moyo na njia ya mkojo. Ukamilikaji wa tafiti hizo na matokeo yake utasaidia hospitali kufanya maamuzi ya uboreshaji wa huduma kwa wagonjwa.

**Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe**

***154.*** ***Mheshimiwa Spika*****,** Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe imeendelea kutoa huduma za matibabu ya afya ya akili kwa wananchi wa kawaida

na wagonjwa wa afya ya akili kwa mujibu wa sheria kwa ajili ya huduma za uchunguzi na matibabu ya afya ya akili pamoja na utoaji wa huduma za matibabu kwa waraibu wa aina mbalimbali ikiwemo waathirika wa dawa za kulevya. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, **jumla ya wagonjwa 75,409** walihudumiwa**,** kati yao 72,421 wagonjwa wa nje na 2,988 walilazwa. Aidha, wagonjwa 134,643 sawa na asilimia 89.1 ni wagonjwa wa Akili na wagonjwa 16,420 sawa na asilimia 10.9 ni wagonjwa wa kawaida.

***155.*** ***Mheshimiwa Spika***; Taasisi ilitoa **misamaha** kwa wagonjwa 4,606 wasioweza kumudu gharama za matibabu yenye thamani ya Shilingi 651,233,855 ambapo Shilingi 52,593,355 ni gharama ya matibabu na Shilingi 598,640,599 ni gharama ya malazi, chakula na mavazi ikilinganishwa na Shilingi 626,921,346 kwa wagonjwa 964 katika kipindi kama hiki mwaka 2024. Huduma zinazoongoza kutolewa misamaha ni pamoja na matibabu, chakula, mavazi na malazi.

***156.*** ***Mheshimiwa Spika;*** Hospitali imeendelea kutoa **huduma za uchunguzi** wa magonjwa mbalimbali ikiwemo uchunguzi wa magonjwa ya akili kati ya hizo, kipimo cha umeme wa Ubongo EEG kilifanyika kwa wagonjwa 56, *ECHO* 270, *ECG* 276, X-Ray 2,625 na *Ultrasound* 2,344. Aidha, katika kipindi hiki, jumla ya **vipimo vya maabara** 35,252 vimefanyika kwa kutumia vifaa vya kisasa na hali ya upatikanaji wa dawa ni asilimia 96.4.

***157. Mheshimiwa Spika***, katika kuongeza uwezo wa Hospitali kutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi kwa hadhi ya Taifa, Hospitali imeendelea kuratibu **mafunzo** kwa wataalam ambapo katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya wataalam 15 wapo masomoni katika fani mbalimbali za ubingwa na ubingwa bobezi ndani na nje ya nchi. Aidha, jumla ya **ajira za mkataba 79** zilitolewa na Hospitali ili kupunguza uhaba wa watumishi uliopo katika fani mbalimbali za utoaji huduma.

***158. Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 hospitali iliwafikia wananchi **125,606** kwa njia **huduma mkoba** uliolenga kutoa elimu ya afya ya akili, matibabu na msaada wa kisaikolojia kwenye mikoa mbalimbali ikiwemo Dodoma, Kigoma, Ruvuma na Singida. Jumla ya wananchi **524** walibainika kuwa na magonjwa na changamoto za Afya ya akili na walipatiwa huduma za matibabu.

***159. Mheshimiwa Spika***, Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha North Carolina, Chuo Kikuu cha Miami, Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo Kikuu cha Afya Sayansi Shirikishi Muhimbili, KCMC na KCMUCo inaendelea na tafiti kubwa nne (4), ambazo ni umuhimu wa elimu ya afya akili kwa wagonjwa na familia zinazohudumiwa wagonjwa wa afya ya akili, matumizi ya akili mnemba katika afya ya akili, mtazamo wa masuala ya afya akili kwa watumishi wa afya na watu wa tiba asili, na

utafiti wa ugonjwa unaoathiri kumbukumbu kwa wazee (Dementia). Matokeo ya tafiti hizi yanatarajiwa kuchangia kuboresha utoaji wa huduma za afya ya akili nchini.

### Hospitali ya Magonjwa Ambukizi - Kibong'oto

**160.** ***Mheshimiwa Spika,*** Hospitali ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto inatoa matibabu ya magonjwa ambukizi kama Kifua Kikuu na Kifua Kikuu Sugu pamoja *na* utaalam wa kimatibabu kwa mikoa na halmashauri kwa njia ya teknolojia ya masafa (MDRTB -ECHO). Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, jumla ya wagonjwa 14,552 walihudumiwa ikilinganishwa na wagonjwa 16,174 katika kipindi kama hiki mwaka 2024. Kati ya wagonjwa hao, wa nje 13,947 na waliolazwa 605. Aidha, kati ya wagonjwa 14,552 waliohudumiwa, wagonjwa 418 waligundulika kuwa na Kifua kikuu, kati yao 367 Kifua kikuu cha kawaida na 51 Kifua kikuu sugu. Wagonjwa 51 wa Kifua kikuu sugu walitokana na rufaa kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara na Zanzibar ambao hulazwa kwa muda wa wastani wa miezi 6 au zaidi wakipatiwa matibabu, chakula, chakula dawa kwa wenye utapiamlo mkali na mahitaji mengine muhimu ya kijamii. Vilevile, kupitia teknolojia ya masafa Hospitali ilihudumia wagonjwa wa Kifua Kikuu Sugu 39 kutoka Mikoa mbalimbali nchini pasipo kulazimika kupatiwa rufaa.

**161.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Hospitali ilitoa **misamaha** kwa

wagonjwa 1,468 wasioweza kumudu gharama za matibabu yenye thamani ya Shilingi 21,892,630 ikilinganishwa na Shilingi 58,382,803 kwa wagonjwa 3,712 katika kipindi kama hiki mwaka 2024. Huduma zilizoongoza kutolewa misamaha ni dawa, huduma za maabara pamoja na huduma za uchunguzi kwa kutumia mionzi.

**162.** ***Mheshimiwa Spika,*** Hospitali imeendelea kutoa **huduma za uchunguzi** wa magonjwa mbalimbali ambapo katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya vipimo 3,682 vya Radiolojia vilifanyika. Kati ya hivyo, vipimo 2,864 vya X-Ray, 784 vya Ultrasound na 34 vya CT Scan. Vilevile, vipimo vya maabara 17,763 vimefanyika kwa kutumia vifaa vya kisasa. Aidha,hali ya upatikanaji wa dawa za Kifua Kikuu na kufubaza virusi vya UKIMWI ni asilimia 100 na asilimia 90 kwa aina nyingine za dawa.

**163.** ***Mheshimiwa Spika,*** Hospitali katika kuboresha huduma za afya imeendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa tatu (3) kwa ajili ya huduma za radiolojia ambapo usimikaji wa mashine ya CT Scan umekamilika na huduma kuanza kutolewa. Aidha, hospitali imekamilisha usimikaji wa kichomea taka cha kisasa, usimikaji wa mtambo na kuanza uzalishaji wa hewa tiba pamoja na upanuzi na ukarabati wa majengo ya utawala.

**164.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza uwezo wa Hospitali kutoa huduma za ubingwa na ubingwa

bobezi kwa hadhi ya Taifa, Hospitali imeendelea kuratibu **mafunzo** kwa wataalam ambapo katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya wataalam 44 wapo masomoni katika fani mbalimbali za ubingwa na ubingwa bobezi ndani na nje ya nchi wakiwemo wanaofadhiliwa na Samia *Health specialization scholarship program*

165. ***Mheshimiwa Spika,*** Hospitali ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto imeendelea kufanya **tafiti** mbalimbali kwa lengo la kuboresha tiba na ugunduzi. Tafiti hizo ni pamoja na utafiti wa kupunguza muda wa matibabu ya kifua kikuu cha kawaida kutoka miezi sita (6) hadi minne (4) na utafiti wa kuboresha matibabu ya wagonjwa wa UKIMWI wenye maambukizi ya Kifua Kikuu ili kuona uwezekano wa kupunguza vifo katika kundi hili. Utafiti huu unafanyika kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Mbarara nchini Uganda na Chuo Kikuu cha Virginia nchini Marekani.

## Hospitali ya Rufaa ya Kanda Bugando

166. ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali ya Rufaa Kanda Bugando hutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi katika Mikoa nane (8) ya Kanda ya Ziwa yenye jumla ya wakazi wapatao milioni 22. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Hospitali imetoa huduma kwa **jumla ya wagonjwa 286,718**. Kati ya hao, waliolazwa 27,016 na wa nje ni 259,702 ikilinganishwa na wagonjwa 365,261 katika kipindi

kama hiki mwaka 2024. Hospitali ilitoa **misamaha** kwa wagonjwa 22,397 wasio na uwezo wa kumudu gharama za matibabu yenye thamani ya Shilingi 3,305,676,941 ikilinganishwa na Shilingi 3,619,939,055 kwa wagonjwa 22,277 katika kipindi kama hiki mwaka 2024. Huduma zinazoongoza kutolewa misamaha ni pamoja na mionzi tiba, magonjwa ya afya ya akili, matibabu ya watoto wachanga, mama wajawazito, uchujaji wa damu na huduma kwa wazee wasiojiweza.

***167.*** ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali imeendelea kutoa huduma za Upasuaji wa ubingwa bobezi kwenye maeneo ya kubadilisha nyonga na magoti, upasuaji wa kinywa na meno, upasuaji wa watoto wenye mdomo sungura (cleft lip/palate), upasuaji wa macho, upasuaji wa koo, pua na masikio, upasuaji wa kifua na moyo, upasuaji wa ubongo, mishipa ya fahamu na uti wa mgongo, upasuaji wa mfumo wa mkojo, upasuaji sanifu, upasuaji Maalumu wa watoto, upasuaji wa matundu madogo na huduma ya viungo tiba (saidizi) na vifaa tiba saidizi (orthopedic – rosthetics and orthotics unit). Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya wagonjwa 10,907 walifanyiwa upasuaji kati yao 10,626 walifanyiwa upasuaji mkubwa na 281 upasuaji mdogo. Aidha, katika kuendelea kutoa huduma za saratani, jumla ya wagonjwa 23,712 walihudumiwa na kati ya hao, wagonjwa 20,551 ni wa nje na 3,161 walilazwa.

***168.*** ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali imeendelea kutoa **huduma za uchunguzi** wa magonjwa mbalimbali

ambapo katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya vipimo 57,406 vya radiolojia vilifanyika. Kati ya hivyo 2,729 MRI, 7,136 CT-Scan, 22,602 X-Ray, 23,749 Ultrasound, 112 Mammography, 814 Fluoroscopy na Interventional radiology vipimo 264. Katika kipindi hiki, jumla ya **vipimo vya maabara** 713,196 vimefanyika kwa kutumia vifaa vya kisasa.

**169.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuongeza uwezo wa Hospitali kutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi kwa hadhi ya Kanda, Hospitali imeendelea kuratibu **mafunzo** kwa wataalam ambapo katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya wataalam 61 wapo masomoni katika fani mbalimbali za ubingwa na ubingwa bobezi ndani na nje ya nchi wakiwemo wanaofadhiliwa na Samia *Health Specialization Scholarship Program*. Pia, katika kipindi hicho Hospitali imepokea watumishi wapya 35 kutoka Serikali Kuu ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma.

**170.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuboresha huduma na kupunguza msongamano wa wagonjwa kusubiri huduma, Hospitali inaendelea na taratibu za ununuzi wa Mashine Tiba ya Mionzi (Linear Accelerator) kwa ajili ya matibabu ya Saratani yenye thamani ya Shilingi 1,763,940,285 kwa ufadhili wa Serikali na mapato ya ndani. Mashine hii itasaidia kuongeza idadi ya wagonjwa watakaohudumiwa kwa siku kutoka 82 hadi 164. Aidha, Hospitali inaendelea na ununuzi wa mashine ya *C-Arm* kwa ajili ya

*Interventional Radiology* yenye thamani ya Shilingi 407,000,000.

171. ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali imeendelea kutoa **huduma mkoba** kwa vituo 38 katika wilaya za Magu, Bariadi, Buchosa, Misungwi na Biharamulo. Katika zoezi hilo, **jumla ya wagonjwa 2,517** walipatiwa huduma na kati yao 328 walifanyiwa Upasuaji. Aidha, Katika kutekeleza dhana ya **Tiba Utalii** nchini, Hospitali ilihudumia jumla ya wagonjwa 85 kutoka nchi za Kenya, Uganda, Rwanda na Zambia. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 Hospitali imefanya **tafiti** 182 katika maeneo mbalimbali ya afya. Tafiti hizo zimekuwa na mchango mkubwa katika kutengeneza miongozo mbalimbali ya matibabu hapa nchini ikiwemo miongozo ya usugu wa Dawa za *Antibiotic*. Vilevile, Hospitali inaendelea na utafiti wa jani la mgomba katika kuwezesha matibabu ya vidonda vya kuungua na moto.

### Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya

172. ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali imeendelea kutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi kwa wananchi wa mikoa saba (7) ya Nyanda za Juu Kusini ambayo ni Mbeya, Iringa, Ruvuma, Njombe, Songwe, Rukwa na Katavi. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 Hospitali imetoa huduma kwa **jumla ya wagonjwa 307,253** ikilinganishwa na wagonjwa 263,011 sawa na ongezeko la asilimia 17 katika kipindi kama hiki mwaka 2024. Kati yao, wagonjwa wa kulazwa ni 36,433 na wagonjwa wa nje (OPD) ni 270,820. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi

Machi 2025 hospitali ilitoa **misamaha** kwa wagonjwa 32,411 wasio na uwezo yenye thamani ya Shilingi 809,499,200 ikilinganishwa na Shilingi 603,730,000 kwa wagonjwa 17,700 katika kipindi kama hiki mwaka 2024.

173. ***Mheshimiwa Spika*,** Hospitali imetoa huduma katika fani za upasuaji wa moyo wagonjwa 226, ubongo na mishipa ya fahamu 11,122 na mfumo wa chakula na ini 7,302, mfumo wa upumuaji 6,359 pamoja na upasuaji wa watoto wachanga kwa wagonjwa 455. Aidha, **huduma nyingine za ubingwa bobezi** zilizoendelea kutolewa ni upasuaji, masikio, pua na koo, saratani, upasuaji wa mifupa, magonjwa ya wanawake, uzazi na watoto, ajali na dharura (EMD), magonjwa ya ndani na ngozi. Kwa huduma za watoto Hospitali imetoa huduma za watoto wachanga wagonjwa 2,216 ikilingalishwa na Watoto wachanga 1,872 katika kipindi kama hiki mwaka 2024. Katika mwaka huu wa fedha huduma za wagonjwa mahututi zilitolewa kwa wagonjwa 1,131 ukilingalisha wagonjwa 904 katika kipindi kama hiki mwaka 2024.

174. ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali imeendelea kutoa **huduma za uchunguzi** wa magonjwa mbalimbali na jumla ya vipimo 51,603 vya Radiolojia vilifanyika. Vipimo hivyo ni pamoja na; MRI vipimo 502, CT Scan 3,089, X-Ray 13,123, Fluoroscopy 11,234 na Ultrasound 23,655. Aidha, katika kipindi hiki jumla ya vipimo vya **maabara** 191,808 vimefanyika kwa kutumia vifaa vya kisasa. Vilevile, kwa sasa hali ya **upatikanaji wa dawa** ni asilimia 91.5.

***175.*** ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali imeendelea **kuratibu mafunzo** kwa wataalam na katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla wataalam 58 wapo masomo katika fani mbalimbali za ubingwa na ubingwa bobezi ndani na nje ya nchi. Aidha, jumla ya **ajira za mkataba 543** zilitolewa na Hospitali ili kupunguza upungufu wa watumishi.

***176.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza dhana ya **Tiba Utalii** nchini, Hospitali ilihudumia jumla ya wagonjwa 177 katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025. Wagonjwa waliohudumiwa ni kutoka nchi za Malawi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Zambia na Msumbiji. Taasisi imehudumia wagonjwa kutoka mataifa mengine nje ya Bara la Afrika ikiwemo China.

**Hospitali ya Rufaa ya Kanda – KCMC**

***177.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Hospitali ilihudumia **jumla ya wagonjwa 187,731**. Kati ya hao wagonjwa wa nje (OPD) ni 173,193 na wagonjwa wa kulazwa ni 14,538 ikilinganishwa na wagonjwa 340,455 katika kipindi kama hiki mwaka 2024. Aidha, Hospitali imeendelea kutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi ikiwemo ubadilishaji wa nyonga wagonjwa 78 na upasuaji kwa njia ya tundu dogo kwenye mfumo wa chakula kwa wagonjwa 231. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 hospitali ilitoa **misamaha** kwa wagonjwa 4,002 wasio na uwezo wa kumudu gharama za matibabu yenye thamani ya Shilingi 2,102,960,145 ikilinganishwa na Shilingi

19,189,800,400 kwa wagonjwa 6,084 katika kipindi kama hiki mwaka 2024.

***178.*** ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali imeedelea kutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi ambazo ni; ugumba na endokrinolojia wagonjwa 1,716, upandikizaji wa kornea wagonjwa 110, upasuaji wa saratani wagonjwa 713, matibabu ya saratani wagonjwa 9,165, upasuaji wa njia ya mkojo wagonjwa 743, matibabu ya ngozi wagonjwa 11,236, na matibabu ya macho wagonjwa 28,337. Huduma zingine zilizotolewa ni matibabu ya njia ya mkojo na kibofu wagonjwa 7,505, upasuaji wa kinywa na uso wagonjwa 131, upandikizaji wa taya wagonjwa 42, viungo bandia wagonjwa 333, viungo saidizi 847, na upasuaji wa retina wagonjwa 509. Huduma hizi zimewezesha wananchi wa mikoa ya Kaskazini kuzipata kwa haraka, urahisi na kuondoa ulazimu wa kuzifuata mbali.

***179.*** ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali imeendelea kutoa **huduma za uchunguzi** ambapo wagonjwa 1,664 walifanyiwa kipimo cha MRI, CT-Scan wagonjwa 4,004, ultrasound wagonjwa 13,276, X-Ray wagonjwa 23,138 na maabara ilifanya vipimo 199,807. Aidha, hali ya upatikanaji wa dawa katika Hospitali ni asilimia 99 ukilinganisha asilimia 98.5 kwa 2024.

***180.*** ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali imeendele kutoa mafunzo kwa watumishi na katika kipindi hiki, jumla ya wataalam 281 wapo masomoni katika fani

mbalimbali za kibingwa ndani na nje ya nchi. Aidha, katika kukabiliana na upungufu wa Watumishi, Hospitali imeajiri jumla ya watumishi 470 wa mikataba.

***181.*** ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali imeendelea kuimarisha huduma kwa kuendelea na upanuzi wa miundombinu kwa ujenzi wa vyumba 11 vya upasuaji ambavyo vimefikia asilimia 78, jengo la mionzi (bunker) uliofikia asilimia 95.5 ikifadhiliwa na Serikali kwa Shilingi Bilioni 4, mabweni ya wagonjwa na ndugu wa wagonjwa wa saratani umefikia asilimia 88 na maabara ya umahiri uliofikia asilimia 80. Vilevile, Hospitali imendelea kuboresha huduma za mama na mtoto kwa kukarabati na kuboresha miundombinu ya wodi ya wazazi ambapo ukarabati huu umekamilika kwa asilimia 100. Ukamilishaji wa miradi hii itasaidia kupunguza msongamano wa wagonjwa, kupunguza muda wa kupata huduma na uanzishaji wa huduma za mionzi tiba ya magonjwa ya saratani.

***182.*** ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali imeendelea kutoa **huduma za mkoba**, na jumla ya wagonjwa 4,618 walipatiwa huduma. Kati yao wagonjwa 2,788 walipatiwa huduma katika Siku ya maadhimisho ya Figo, Macho na Usikivu Duniani na Wagonjwa 1,830 walipatiwa huduma za saratani, VVU/UKIMWI na Ngozi.

***183.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuendeleza dhana ya **Tiba Utalii** nchini, Hospitali ilipokea jumla ya

wagonjwa 579 ikilinganishwa na wagonjwa 384 kwa kipindi kama hiki mwaka 2024 kutoka katika nchi za Kenya, Uganda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Comoro. Aidha, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Hospitali iliwapatia huduma za matibabu raia wa kigeni 51 kutoka nchi mbalimbali waliofika nchini kwa shughuli anuai ikiwemo utalii kutoka Marekani, Uingereza na Canada.

***184.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya **tafiti 35** zimefanyika katika maeneo ya magonjwa ya kuambukiza, usimamizi wa matibabu ya dharura, uchunguzi wa vinasaba vya magonjwa kama VVU na uchunguzi wa magonjwa yasiyoambukiza kama Kisukari na shinikizo la damu. Tafiti hizo hufanyika kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo *Duke University, London School of Hygine and Tropical Medicine, Radbound University* na *Philips University of Murburg*.

**Hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato**

***185.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato inahudumia Mikoa ya Kagera, Kigoma, Geita na Shinyanga na nchi ya jirani ya Burundi. Hospitali inatoa huduma za kibingwa katika fani za afya ya uzazi na magonjwa ya akinamama, upasuaji, radiolojia, dawa za ganzi na usingizi na magonjwa ya watoto. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 Hospitali imetoa huduma kwa **jumla ya wagonjwa 30,553**, wagonjwa wa nje 28,759 na wa kulazwa ni 1,794 ikilinganishwa na wagonjwa 40,370 katika kipindi kama hiki 2024. Wagonjwa waliopata huduma

za kibingwa ni 29,737 kati yao 6,226 magonjwa ya afya ya uzazi, 9,409 magonjwa ya Watoto, 3,222 huduma ya upasuaji na 10,880 magonjwa ya ndani. Aidha, hospitali inashirikiana na Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete ili kutoa huduma za kibingwa na kibingwa bobezi za moyo kupitia kliniki ya kila mwezi ambapo jumla ya wagonjwa 3,521 wamenufaika na huduma hiyo.

***186.*** ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali imeanzisha huduma mpya nne (4) katika kipindi hiki ambazo ni kliniki ya ubingwa na ubingwa bobezi ya mifupa, ubongo na mishipa ya fahamu iliyohudumia wagonjwa 2,598, ambao kati yao, mifupa ni 1,795, mishipa ya fahamu ni 795, na upasuaji mkubwa wa mifupa 36 na wagonjwa 12 upasuaji mkubwa wa ubongo. Huduma nyingine mpya zilizoanzishwa ni pamoja na kuanzisha huduma ya benki ya damu, upimaji wa wingi wa Virusi vya UKIMWI na Kliniki ya Selimundu.

***187.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, hospitali ilitoa **misamaha** kwa wagonjwa 586 yenye thamani ya Shilingi 121,201,313 ikilinganishwa na wagonjwa 314 yenye thamani ya Shilingi 94,679,090 katika kipindi kama hiki mwaka 2024.

***188.*** ***Mheshimiwa Spika***, huduma za uchunguzi wa magonjwa zimeendelea kutolewa na katika kipindi hiki vipimo 12,397 vya radiolojia vilifanyika. Kati ya hivyo vipimo vya *MRI* vilikuwa 279, *CT Scan* 351, *X-Ray* 2,565, *Dental X-Ray* 133 na *Ultrasound* 2,635,

*ECHO* 3,102 na *ECG* 3,342. Aidha, katika kipindi hiki, jumla ya vipimo vya maabara 40,745 vimefanyika kwa kutumia mashine za kisasa na hali ya upatikanaji wa dawa imefikia asilimia 97.

***189.*** ***Mheshimiwa Spika***, Hospitali imeendelea kuratibu mafunzo kwa watumishi na hadi kufikia Machi 2025, jumla ya madaktari 20 wapo masomoni katika fani mbalimbali za ubingwa na ubingwa bobezi ndani na nje ya nchi. Kati ya wataalam hao 20, watumishi saba (7) wanasomeshwa kutokana na mapato ya ndani. Sambamba na hili Hospitali kupitia mapato ya ndani imeajiri watumishi 30 wa mkataba.

***190.*** ***Mheshimiwa Spika***, huduma za mkoba zimeendelea kutolewa na katika kipindi hiki huduma hizo zimefanyika katika Hospitali ya Wilaya ya Muleba ambapo wagonjwa 1,600 walipata huduma za kibingwa. Aidha, wagonjwa 695 walipatiwa huduma za afya ya uzazi, 327 huduma za watoto, 208 huduma za upasuaji na 370 huduma za magonjwa ya ndani. Vilevile, wagonjwa 21 walifanyiwa upasuaji, 13 upasuaji mdogo na 8 upasuaji mkubwa.

***191.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza dhana ya **Tiba Utalii**, Hospitali ilihudumia jumla ya wagonjwa 15 kutoka nchi za Uganda na Burundi. Aidha, katika kuboresha huduma za Hospitali kupitia tafiti, Hospitali imefanya tafiti sita (6) zinazohusu uboreshaji wa huduma. Tafiti hizo zipo katika hatua

mbalimbali ambapo tafiti moja imeshachapishwa na nyingine zipo katika hatua mbalimbali za uchapishaji.

## Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini – Mtwara

**192.** ***Mheshimiwa Spika,*** Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini – Mtwara inahudumia wananchi wa mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma pamoja na wananchi wa nchi za nchi jirani kama Comoro, Msumbiji na Malawi. Wizara imeendelea kuiwezesha Hospitali kuwa na uwezo zaidi wa kutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi ambapo Hospitali imeendelea kuimarika na kuwa na uwezo wa kutoa huduma za kibingwa katika fani za Afya ya uzazi na magonjwa ya akina mama, upasuaji, upasuaji wa mifupa, magonjwa ya ndani, radiolojia na huduma ya ubobezi ya magonjwa ya moyo. Katika kipindi hiki hospitali imehudumia jumla ya wagonjwa 31,297. Kati yao, wagonjwa wa nje ni 29,239 na wa kulazwa ni 2,058 ikilinganishwa na wagonjwa 22,122 katika kipindi kama hiki mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 41.

**193.** ***Mheshimiwa Spika,*** Hospitali imeanzisha kitengo maalum kwa ajili ya huduma za lishe, huduma hii itasaidia katika matibabu lishe kwa wagonjwa na hivyo kuboresha matokeo ya huduma za tiba. Aidha, Hospitali Inaendelea kukamilisha maandalizi ya huduma ya uchujaji damu (dialysis) baada ya mapokezi ya mashine tisa (9) na mafunzo ya watumishi kukamilika. Huduma hii itaongeza wigo wa huduma za kuchuja damu kutoka Hospitali moja ya

umma kwa Kanda ya kusini na kufikia Hospitali mbili (2) zinazotoa huduma hizo.

***194.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki, Hospitali ilitoa huduma za kibingwa kwa wagonjwa 7,507 na kati yao; wagonjwa 492 walifanyiwa upasuaji, 1,517 walipatiwa matibabu ya magonjwa ya moyo, 2,693 walipatiwa matibabu ya mifupa, 1376 walipatiwa huduma za dharura, 834 walipatiwa matibabu ya magonjwa ya akinamama na uzazi na 595 walipatiwa huduma za magonjwa ya ndani. Pia, huduma za Mkoba kwa ajili ya matibabu ya mifupa na meno ziliendelea kutolewa ambapo wagonjwa 476 walipatiwa matibabu ya meno na wagonjwa 416 walipatiwa huduma ya matibabu ya mifupa.

***195.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki Hospitali ilitoa misamaha kwa wagonjwa 365 wasio na uwezo wa kumudu gharama za matibabu yenye thamani ya Shilingi 14,037,559 ikilinganishwa na Shilingi 14,091,153 kwa wagonjwa 241 katika kipindi kama hiki mwaka 2024.

***196.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Hospitali imeendelea kutoa huduma za uchunguzi wa kibingwa ambapo katika kipindi hiki, wagonjwa 152 walifanyiwa kipimo cha MRI, wagonjwa 410 walifanyiwa kipimo cha CT-Scan, wagonjwa 2,279 walifanyiwa kipimo cha ultra-sound na wagonjwa 2,082 walifanyiwa kipimo cha X-ray. Kwa upande wa **maabara** jumla ya vipimo 31,220 vilifanyika. Aidha, hali ya upatikanaji wa damu

salama katika Hospitali ni asilimia 100 na upatikanaji wa dawa ni asilimia 95.

197. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Hospitali imeendelea kuratibu mafunzo kwa watumishi 21 ambao wapo masomoni kwa mafunzo ya ubingwa na ubingwa bobezi katika fani mbalimbali. Vilevile, Hospitali imepokea watumishi 58 wa ajira mpya kutoka Serikali Kuu na pia imeajiri watumishi 53 kwa mapato ya fedha za ndani kwa mkataba ili kuongeza nguvu ya rasilimali kwa lengo la kuboresha huduma kwa wagonjwa.

198. ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kuimarisha diplomasia ya nchi kupitia **tiba utalii**, hospitali ilitoa huduma kwa jumla ya wagonjwa 271 kutoka nchi za Comoro, Malawi na Msumbiji. Aidha, Hospitali imefanikiwa kuongeza vyumba sita (6) vya wodi ya watu maalum ambavyo vinaweza kutumika kwa wateja wanaohitaji huduma za kipekee kwa malipo ya ziada.

199. ***Mheshimiwa Spika,*** Hospitali imeendelea kufanya tafiti tatu, ambazo zinahusu; (1) tathmini ya ufuasi wa matumizi ya dawa na viashiria vya dharura za shinikizo la damu, (2) uelewa wa watoa huduma kuhusu usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa (UVIDA), na (3) uelewa wa vihatarishi vya maambukizi ya virusi vya Homa ya Ini B (HBV).

**Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Mashariki – CCBRT**

***200. Mheshimiwa Spika***, Hospitali imeendelea kutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi , na kipindi hiki wagonjwa 88,808 walihudumiwa ikilinganishwa na wagonjwa 86,211 katika kipindi kama hiki mwaka 2024. Waliohudumiwa katika kipindi hiki, wagonjwa wa nje ni 84,982 na wa kulazwa ni 3,826. Aidha, wagonjwa 9,557 walipata huduma na kati yao walikuwa na ulemavu wa macho, mdomo sungura, miguu kifundo, mtindio wa ubongo, ulemavu mwingine wa viungo na fistula kwa wanawake. Katika kipindi hiki, jumla ya wajawazito waliojifungua walikuwa 921.

***201. Mheshimiwa Spika***, Hospitali imetoa **huduma mpya nne (4)** ambazo ni upasuaji rekebishi wagonjwa (35), upasuaji kwa njia ya matundu madogo (14); kutoa uvimbe kwenye mayai ya uzazi wagonjwa (23), kufunga mirija ya uzazi kama njia ya uzazi wa mpango wagonjwa (9), upasuaji wa ndani ya kizazi kwa njia ya kamera wagonjwa (18) na huduma ya uchunguzi kwa njia ya matundu madogo wagonjwa (61), na kuweka lensi kwenye mboni 246. Hospitali pia imetoa huduma ya ziada ya Upasuaji wa makengeza kwa watoto 58.

***202. Mheshimiwa Spika***, Hospitali iliendelea kutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi za upasuaji kwa wagonjwa 6,667 walinufaika. Kati yao, wagonjwa 5,289 walifanyiwa upasuaji wa macho,

322 fistula ya uzazi, 880 upasuaji wa mifupa, 90 upasuaji wa mdomo sungura, na 354 wenye miguu kifundo. Pia, hospitali ilitoa huduma za utengemao kwa wahitaji 3,100. Aidha, huduma zingine zilizotolewa ni pamoja na huduma ya kuchuja damu kwa wagonjwa 151 na kutoa viungo saidizi kwa wahitaji 663. Vilevile, katika kipindi hiki hospitali ilitoa misamaha kwa wagonjwa 6,150 yenye thamani ya Shilingi 3,248,719,944.46 ikilinganishwa na wagonjwa 4,552 waliogharimu Shilingi 6,695,986,236 kwa katika kipindi kama hiki mwaka 2024.

***203. Mheshimiwa Spika***, katika kipindi hiki Hospitali imeimarisha huduma za **uchunguzi za maabara** ambapo vipimo 74,346 vilifanyika. Katika kipindi hicho, wagonjwa 268 walifanyiwa kipimo cha CT - Scan, 4,063 *ultra-sound*, 1,387 *Echocardiology* na 6,644 *X-Ray*. Sambamba na hilo, Hospitali imetoa ufadhili kwa mtaalam mmoja (1) aliyepo masomoni kwa kozi za ubingwa na ubingwa bobezi wa masuala ya obiti na upasuaji rekebishi wa jicho. ***Aidha,*** Hospitali imeendelea kutoa **huduma za mkoba** kwa wagonjwa 10,433. Huduma hizo ni pamoja na utengemao kwa wateja 1615.

***204. Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza dhana ya Tiba Utalii hospitali imehudumia wagonjwa 591 ikilinganishwa na wagonjwa 135 kwa kipindi kama hiki mwaka 2024. Huduma za matibabu zilizotolewa zilihusisha tiba ya macho, vifaa saidizi vya macho, mifupa na Fistula ya uzazi kwa wageni kutoka

Burundi, Comoro, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Misri, Eritrea, Ethiopia, Ghana, Kenya, Malawi, Msumbiji, Rwanda, Somalia na Sudan. Aidha, hospitali imehudumia wagonjwa kutoka mataifa mengine nje ya Bara la Afrika ikiwemo Ireland ya Kaskazini, China, India, Indonesia na Iran.

**Hospitali za Rufaa za Mikoa**

***205.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki Hospitali 28 za Rufaa za Mikoa zimeendelea kuimarishwa ili kutoa huduma zenye hadhi ya ubingwa hususani katika fani nane za kipaumbele ambazo ni huduma za magonjwa ya ndani, magonjwa ya watoto, upasuaji, upasuaji wa mifupa, radiolojia, dawa za usingizi na ganzi, huduma za dharura na afya ya uzazi na magonjwa ya akina mama. Katika kipindi hiki Hospitali za Rufaa za Mikoa zimetoa huduma kwa wagonjwa 2,628,784 ambapo kati ya wagonjwa hao wa kulazwa ni 220,494 na wa nje ni 2,408,290 ikilinganishwa na wagonjwa 2,309,964 waliohudumiwa kipindi kama hiki mwaka 2024.

***206.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 Hospitali za Rufaa za Mikoa zilitoa misamaha kwa wagonjwa 134,145 yenye thamani ya Shilingi 2,630,043,203 ikilinganishwa na Shilingi 2,920,786,230 kwa wagonjwa 302,999 katika kipindi kama hiki mwaka 2024.

***207.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Hospitali za Rufaa za Mikoa zimetoa **huduma mkoba**, jumla ya wagonjwa 68,058 walihudumiwa na kati yao 5,121 walifanyiwa upasuaji

ikilinganishwa na wagonjwa 35,281 waliohudumiwa na 2,356 waliofanyiwa upasuaji kipindi kama hiki mwaka 2024. Huduma mkoba zilizotolewa zilikuwa za magonjwa ya akinamama na afya ya uzazi, magonjwa ya ndani, watoto, afya ya akili, upasuaji, upasuaji wa mifupa, magonjwa ya njia ya mkojo, afya ya kinywa na meno, masikio, pua na koo, macho, ngozi, utoaji wa dawa za usingizi na ganzi na radiolojia. Uanzishwaji wa huduma mpya na utoaji wa huduma mkoba uliwawezesha wananchi kupata huduma kwa haraka katika Mikoa yao, kupunguza gharama za matibabu na kupunguza msongamano katika Hospitali za Rufaa za Kanda, Maalum na Taifa.

***208.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki, jumla ya vipimo 395,971 vilifanyika. Vipimo hivyo vimejumuisha CT scan 24,370, *Ultra Sound* 184,768 na *X-ray* 186,833. Aidha, jumla vya vipimo 1,920,148 vya maabara vilifanyika. Upatikanaji wa dawa kwa Hospitali za Rufaa za Mikoa umeongezeka kutoka asilimia 94 mwaka 2024 na kufikia asilimia 96 mwaka 2025.

***209.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika dhana ya kuendeleza **Tiba Utalii** nchini, Hospitali za Rufaa za Mikoa na hasa zilizopo pembezoni mwa mipaka ya nchi, zilihudumia wagonjwa 275 kutoka nchi jirani za Malawi, Ethiopia, Zambia, Somalia, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo, Burundi, Kenya, Uganda na Msumbiji.

210. ***Mheshimiwa Spika,*** Hospitali zimeendelea kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za afya kwa kujenga majengo mapya, ukarabati wa majengo pamoja na ununuzi wa vifaa tiba na mitambo. Baadhi ya vifaa tiba na mitambo iliyonunuliwa ni 3D-CBCT (CT- Scan Maalum za kinywa na meno), mashine za mionzi, meza za upasuaji, mashine za kutoa dawa za usingizi na ganzi, mashine za *ultra sound*, mitambo ya kisasa ya kuchomea taka, mashine za kufulia, mashine za huduma ya *endoscope*, mitambo ya kuzalisha hewa tiba ya oksijeni na magari ya wagonjwa na utawala.

211. ***Mheshimiwa Spika,*** idadi ya madaktari bingwa wanaopatikana Hospitali za Rufaa za Mikoa imeongezeka kufikia 402 hadi Machi 2025 ikilinganishwa na 328 kipindi kama hiki mwaka 2024. Hii imesababisha kuongezeka kwa hospitali zinazotoa huduma za kibingwa kwa fani 8 zinazohitajika kufikia 15 ukilinganisha na 8 za kipindi kama hicho mwaka 2024. Hospitali zimeendelea kuratibu mafunzo ambapo katika kipindi hiki, watumishi 563 walikwenda masomoni katika fani mbalimbali, kati yao 146 sawa na asilimia 25 walifadhiliwa na hospitali kwa kutumia mapato ya ndani. Kwa upande wa tafiti, jumla ya tafiti 98 zimefanyika na tafiti hizo zimejikita katika maeneo ya magonjwa ya ndani, magonjwa ya mama na mtoto, maabara, magonjwa ya dharura na lishe.

## Mapambano Dhidi ya Magonjwa ya Kuambukiza

### Mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI, Homa ya Ini na Magonjwa ya Ngono

**212.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa afua mbalimbali zenye lengo la kuzuia maambukizi mapya na kutoa huduma za tiba kwa magonjwa ya VVU/UKIMWI, Magonjwa ya Ngono na Homa ya Ini. Afua hizo ni pamoja na; kuhamasisha wananchi kupima na kutambua hali zao za maambukizi ya VVU; kutoa huduma za ushauri nasaha; upimaji; matunzo na huduma za dawa kwa wenye maambukizi ya VVU/UKIMWI; huduma ya kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto; kuhamasisha wananchi kwenda kwenye vituo vya kutolea huduma za afya kupima na kupata chanjo ya kujikinga na maambukizi ya Homa ya Ini; kutoa elimu kwa jamii na kuhamasisha wananchi, hususan wajawazito kupima maambukizi ya magonjwa ya ngono na kupata matibabu sahihi.

**213.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi kufikia Machi 2025, takwimu zinaonesha kuwa jumla ya watu 1,530,227 walikuwa wanatambua hali zao za maambukizi ikiwa ni sawa na asilimia 90 ya watu 1,700,000 wanaokadiriwa kuishi na VVU nchini (95 ya kwanza). Watu 1,500,212 kati ya waliopima na kutambua hali zao za maambukizi ya VVU walikuwa wameanza kutumia dawa za kufubaza VVU, sawa na asiilimia 98 (95 ya pili). Aidha, jumla ya vipimo 874,944 vya kujua wingi wa VVU (Viral Load) kwa

wagonjwa walioanza kutumia dawa vilifanyika, ambapo vipimo vya wagonjwa 858,272 sawa na asilimia 98 vilionesha kuwa virusi vya UKIMWI vimefubazwa (95 ya tatu). **Jedwali Na. 5** linaonesha ufafanuzi huo.

**Jedwali Na. 5. Mafanikio kuelekea kufikisha malengo ya 95-95-95.**

| Na. | Kiashiria | Machi 2024 | Machi 2025 | Hali ya 95-95-95 |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Wanaokadiriwa kuwa na maambukizi (People Living with HIV/AIDS - PLHIV) | 1,700,000 | 1,700,000 | |
| | Wanaotambua hali zao za Maambukizi | 1,515,838 | 1,530,227 | 95 ya kwanza |
| | Asilimia ya wanaotambua hali zao (on care) | 89 | 90 | |
| 2 | Wenye maambukizi na wameanza dawa | 1,493,532 | 1,500,212 | 95 ya pili |
| | Asilimia ya walioanza dawa (on ART) | 98.5 | 98 | |
| 3 | Idadi ya waliopimwa makali ya VVU (VL test) | 974,405 | 874,944 | |
| | Idadi ya makali yaliyofubazwa | 964,917 | 858,272 | 95 ya tatu |
| | Asilimia ya waliofubazwa makali (VL<1000) | 98 | 98 | |

***214. Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa **huduma kwa WAVIU** zinasogezwa karibu zaidi na jamii, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo, imekuwa ikifanya jitihada kuhakikisha kila kituo cha kutolea huduma za afya nchini kinakuwa na uwezo wa kutoa huduma kwa watu wanaoishi na maambukizi ya VVU na UKIMWI. Hadi kufikia Machi 2025, Jumla ya vituo vinavyotoa huduma ya Tiba na Matunzo (CTC) vimefikia 7,994 sawa na asilimia 78 ya vituo 10,263 vinavyotoa

huduma za afya nchini. Lengo ni kufikia zaidi ya asilimia 95 ya vituo vyote nchini vinavyotoa huduma za afya ifikapo mwaka 2030.

**_215. Mheshimiwa Spika,_** Serikali imevijengea uwezo vituo vya kutolea huduma za afya ngazi ya msingi ili viweze kufanya uchunguzi wa awali na kutoa rufaa kwa wanaobainika kuwa na Virusi vya **Ugonjwa wa Homa ya Ini**. Wagonjwa wanaopewa rufaa hupata huduma za tiba na matunzo katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, Kanda na Taifa. Aidha, Utafiti uliofanyika mwaka 2022/23 (THIS 2022/23) ulionesha kuwa ushamiri wa ugonjwa wa Virusi vya Homa ya Ini aina ya B nchini ni asilimia 3.5 na asilimia 0.2 aina ya C, ushamiri umepungua ikilinganishwa na utafiti kama huu uliofanyika mwaka 2016/17 ambapo ushamiri wa ugonjwa Virusi vya homa ya ini aina ya B ulikuwa asilimia 4.1 na asilimia 1.0 aina ya C. Katika tafiti hii matokeo yalionesha kuwa idadi kubwa ya walioathirika ni watumiaji na wajidunga wa dawa za kulevya. Wizara inatekeleza Mpango Mkakati jumuishi kwa ajili ya afua ya Homa ya Ini kwenye vituo vya kutolea huduma za Afya nchini kote ili kuhakikisha huduma inawafikia wananchi kwa karibu zaidi.

**_216. Mheshimiwa Spika,_** Wizara inaendelea kuhakikisha **upatikanaji wa dawa kinga kwa makundi yaliyo katika hatari zaidi ya kuambukizwa au kuambukiza VVU,** hadi kufikia Machi 2025 jumla ya wateja 47,307 walipatiwa huduma ya dawa kinga. Makundi lengwa ni wanaume na vijana wa kike na

wakiume walio katika hatari zaidi ya maambukizi. Makundi hayo yanajumuisha wachimbaji madini, madereva wa masafa marefu, wavuvi, wajidunga, wanawake wanaoendesha maisha kwa kujihusisha na ngono na wateja wao, na vijana wa kike wasio na ajira wala kipato rasmi.

217. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kutekeleza mikakati mahususi hususan kwenye mikoa ya Iringa, Njombe na Mbeya ambayo ina kiwango cha juu cha maambukuzi ya VVU. Baadhi ya mikakati hiyo ni pamoja na kuimarisha afua ya tohara kwa wanaume, utoaji wa elimu ya kinga na matibabu na kufikisha huduma wezeshi za kiuchumi kwa vijana balehe kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu.

218. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza afua mbalimbali ili kuhakikisha **mama wajawazito wanapimwa maambukizi ya VVU** wanapohudhuria kliniki na hata baada ya kujifungua. Lengo likiwa ni kuhakikisha mtoto aliyeko tumboni anakingwa dhidi ya maambukizi ya VVU kutoka kwa mama. Huduma hizi zinaenda sambamba na kupima na kutibu maambukizi ya Kaswende na kukinga virusi vya Homa ya Ini aina ‘B’ kwa mama na mtoto. Aidha takwimu zinaonesha kwamba katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya **wajawazito 2,127,548 walihudhuria kliniki,** wajawazito **2,089,252** sawa na asilimia 98.2 walipimwa maambukizi ya VVU ikilinganishwa na asilimia 97.4 ya wajawazito waliopimwa VVU katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Kati ya waliopimwa asilimia 2.6

walikuwa na maambukizi ya VVU. Aidha, asilimia 94.6 ya wajawazito waliobainika kuwa na maambukizi walianzishiwa matibabu ili kumkinga mtoto aliye tumboni asipate maambukizi.

***219.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 watoto waliozaliwa na kinamama wenye maambukizi ya VVU na kuwekwa katika uangalizi maalum kwa muda wa miezi 24 walikuwa 21,081 na kati yao watoto 235 sawa na asilimia 1.1 walibainika kuwa wameambukizwa VVU na hivyo kuwekwa katika mpango wa matibabu. Wizara inaendelea kuhakikisha kuwa watoto wote wanaozaliwa na mama wenye maambukizi wanazaliwa wakiwa hawana maambukizi na wanaishi hadi kufikia miezi 24 bila ya kuwa na maambukizi ya VVU kwa kutoa dawa za kuzuia maambukizi ya VVU, kutoa elimu ya unyonyeshaji sahihi na kufanya uchunguzi mapema.

***220.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sera ya Afya kwa kuhakikisha vituo vinatoa **huduma bora za kliniki kwa kina mama wajawazito,** huduma hizo zikiwa ni pamoja kutoa elimu ya afya kuhusu viashiria vya hatari na lishe na kuwafanyia vipimo mbalimbali vya msingi ikiwemo vipimo vya uchunguzi wa VVU na magonjwa ya ngono pamoja na kaswende. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya wajawazito **1,742,625** walifanyiwa kipimo cha kaswende ambapo wajawazito 7,787 sawa na asilimia 0.45 waligundulika kuwa na maambukizi ya kaswende na

kupatiwa matibabu. Hii ni pungufu ya asilimia 0.19 ikilinganishwa na asilimia 0.64 ya wajawazito waliokutwa na maambukizi ya kaswende katika kipindi kama hicho mwaka 2024 (**Jedwali Na. 6**).

***Jedwali Na. 6. Ulinganifu wa Viashiria vya Huduma za Kuzuia Maambukizi ya VVU na Kaswende kutoka kwa Mama kwenda kwa Mtoto kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025.***

| Na. | Viashiria | Julai 2023-Machi 2024 | Julai 2024-Machi 2025 |
|---|---|---|---|
| 1 | Idadi ya wajawazito waliohudhuria Kliniki | 1,973,955 | **2,127,548** |
| 2 | Idadi wajawazito waliopima VVU kipimo cha kwanza | 1,891,963 | 1,986,614 |
| 3 | Asilimia ya waliopata uchauri na kupima VVU ANC | 97.8 | 97.3 |
| 4 | Idadi ya wajawazito waliokutwa na maambukizi ya VVU | 53,454 | 55,363 |
| 5 | Asilimia ya waliokutwa na maambukizi | 2.8 | 2.7 |
| 6 | Asilimia ya wajawazito walioanza Dawa kuzuia maambukizi kwa mtoto | 95.8 | 89.7 |
| 7 | Jumla ya watoto waliozaliwa | 1,636,931 | **1,708,556** |
| 8 | Watoto waliowekwa katika ufuatiliaji wa VVU kwa miezi 24 | 45,514 | 42,218 |
| 9 | Watoto waliokutwa na VVU baada ya miezi 24 | 1,779 | 1,663 |
| 10 | Asilimia waliokutwa na maambukizi ya VVU baada ya miezi 24 | 3.9 | 3.9 |
| 11 | Wajawazito waliopima kaswende | 1,772,993 | 1,742,625 |
| 12 | Wajawazito waliogundulika na kaswende | 11,419 | 7,787 |
| 13 | Asilimia ya wajawazito waliokutwa na kaswende | 0.64 | 0.45 |

***Chanzo: DHIS2 2025***

## Mapambano dhidi ya Kifua Kikuu na Ukoma

**221.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha huduma za Kifua Kikuu kwa kuhakikisha wananchi wanapata huduma za uchunguzi, upimaji, na matibabu dhidi ya Kifua Kikuu. Kwa mujibu wa taarifa za Shirika la Afya Duniani ya Mwaka 2024, imeonesha kwamba Tanzania ni miongoni mwa nchi tatu (3) kati ya nchi zenye wagonjwa wengi wa Kifua Kikuu kukaribia lengo la kupunguza visa vipya vya Kifua Kikuu kwa asilimia 50 na kuwa kati ya nchi 13 zinazokaribia kufikia lengo la kupunguza vifo vitokanavyo na Kifua Kikuu kwa asilimia 75 ifikapo mwaka 2025. Nchi yetu imefanikiwa kupunguza visa vipya vya Kifua Kikuu kwa asilimia 40 na kupunguza idadi ya vifo vitokanavyo na Kifua Kikuu kwa asilimia 68.

**222.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Wizara imenunua na kusambaza mashine 75 za ***GeneXpert*** na ***Truenat*** 110 kwa ajili ya kuimarisha huduma za upimaji kwa kutumia teknolojia ya vinasaba. Mashine hizo zimesambazwa katika vituo vya kutolea huduma za afya 165. Hii inafanya nchi kuwa na mashine za *GeneXpert* 417 na Truenat 157, na hivyo kufanya jumla ya mashine kufikia 573. Hii imeongeza uibuaji wa wagonjwa wenye vimelea vya Kifua Kikuu. Katika kipindi hicho, Wizara imefanikiwa kuibua jumla ya wagonjwa 56,002 wa Kifua Kikuu sawa na asilimia 76 ya lengo la kuibua visa 73,408. Aidha, wagonjwa 236 wa Kifua

Kikuu sugu waliibuliwa sawa na asilimia 65 ya lengo la kuibua wagonjwa 362.

***223.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutoa **huduma mkoba** na **kliniki tembezi** zenye uwezo wa kutoa huduma za uchunguzi na ugunduzi kwa magonjwa ya Kifua Kikuu na magonjwa mengine ya mfumo wa njia ya hewa katika maeneo yenye makundi hatarishi kuambukizwa ugonjwa wa Kifua Kikuu. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla wananchi 14,827 walifikiwa, 6,810 walichunguzwa Kifua Kikuu, 3,079 walihisiwa kuwa na Kifua Kikuu, 1,500 walipimwa kwa kutumia mashine aina ya Gene-Xpert na wagonjwa 579 wa Kifua Kikuu wameibuliwa kupitia huduma za Mkoba za kliniki tembezi.

***224.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya visa 1,067 vya Ukoma viliibuliwa nchini, ambapo mikoa iliyoibua visa vingi zaidi ni pamoja na Morogoro, Lindi, Dar es Salaam, Mtwara, Tanga na Unguja. Kiwango cha maambukizi kimeshuka kutoka wagonjwa 20 kwa kila watu 10,000 kwa mwaka 1979 hadi mgonjwa 1 kwa kila watu 10,000 kwa mwaka 2024. Hii ilichangiwa na uwepo wa mikakati ya kutoa elimu juu ya ugonjwa wa Ukoma na kushirikisha jamii katika uibuaji wa ugonjwa huu. Aidha, Visa vya ugonjwa wa Ukoma nchini vimepungua kutoka wagonjwa 35,400 mnamo mwaka 1979 hadi 1,346 kwa mwaka 2024 sawa na punguzo la asilimia 96.

225. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imejipanga kuendelea kutoa elimu na hamasa kwa jamii kuhusu ugonjwa wa ukoma na pia inaendelea kujenga uwezo kwa watumishi wa afya ili waweze kuwa na uelewa wa ugonjwa huo ikiwa ni sehemu ya mikakati ya kukabiliana na changamoto hii. Serikali inaendelea kutoa hamasa kwa mikoa, halmashauri na vituo viweze kuweka katika mipango yao afua za Ukoma zinazolenga kutokomeza ugonjwa huo.

**Mapambano dhidi ya Malaria**

226. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha **Mapambano dhidi ya Malaria**, Wizara imeendelea kuhakikisha Vipimo pamoja na dawa za kutibu malaria zinapatikana wakati wote katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 Wizara ilinunua na kusambaza dozi 1,364,220 za dawa mseto ya malaria, vichupa 3,289,685 vya dawa ya sindano ya Artesunate na vitepe 9,644,925 vya vipimo vya MRDT. Mikakati hii imeimarisha hali ya upatikanaji wa dawa na vitendanishi vya malaria katika vituo vya kutolea huduma za Afya nchini na kufikia wastani wa asilimia 90. Upatikanaji wa vipimo na dawa za tiba ya malaria katika vituo vya kutolea huduma za Afya kwa wakati wote kunachangia kupunguza kiwango cha maambukizi ya malaria katika jamii, ambayo imesaidia kupunguza idadi ya wagonjwa wa malaria na kupungua kwa vifo vinavyotokana na ugonjwa wa malaria. Mathalan, vifo vinavyotokana na ugonjwa wa malaria vimepungua kwa asilimia 39 kutoka vifo 2,460 mwaka 2020 mpaka vifo 1503, mwaka 2024

vilivyoripotiwa kutoka katika vituo vya kutolea huduma za afya. Mafanikio hayo yametokana na kutekeleza afua za kinga za matumizi ya vyandarua vyenye dawa, udhibiti wa mazalia ya mbu kwa kufanya usafi wa mazingira, matumizi ya tiba kinga na matumizi ya viuadudu vya kibaiolojia, kuwepo kwa huduma za upimaji na matibabu ya malaria kwenye vituo vya kutolea huduma za afya na uelimishaji wa jamii dhidi ya matumizi sahihi ya afua za kinga, vipimo na matibabu kwa wakati.

***227. Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kutekeleza afua mbalimbali ambazo zimekuwa na lengo la kuhakikisha malaria inatokomea kabisa kufikia mwaka 2030. Mojawapo ya afua hizo ni pamoja na kugawa vyandarua vyenye dawa kupitia makundi Maalum kama wanafunzi wa shule za msingi, akinamama wajawazito na Watoto chini ya mwaka mmoja. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya vyandarua 6,220,340 vilisambazwa ambapo vyandarua 3,635,890 vilisambazwa kupitia njia ya kampeni (Targeted Mass Campaign) kwenye Halmashauri 12 za Mikoa ya Mwanza na Geita, vyandarua 2,469,375 vimesambazwa kwa wajawazito na watoto wenye umri chini ya mwaka mmoja kupitia vituo vya kutolea huduma za afya na vyandarua 115,075 vilisambazwa kupitia wanafunzi wa shule za msingi kwenye Halmashauri tatu (3) za Mkoa wa Tabora ambazo ni Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua, Halmashauri ya Wilaya ya Nzega na Halmashauri ya Mji wa Nzega. Halmashauri hizi zimechaguliwa miongoni mwa halmashauri 8 za

Mkoa wa Tabora kwa kuonekana kuwa na kiwango kikubwa cha visa vya maambukizi ya malaria kwa mama wajawazito kwa taarifa za mwaka 2023.

***228. Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za Serikali kuharakisha kutokomeza malaria ifikapo 2030, Wizara imeendelea kutekeleza afua ya kuangamiza viluilui wa mbu kwa kutumia viuadudu vinavyozalishwa na kiwanda cha ndani cha kuzalisha viuadudu vya kibaiolojia (Biolarvicides) cha *Tanzania Biotech Products Limited (TBPL)* kilichopo Kibaha Mkoani Pwani ambapo Wizara imetenga jumla ya Shilingi Bilioni 10 kwa ajili ya kununua Lita 819,333 za viuadudu kutoka kiwandani humo. Aidha, hadi kufikia Machi 2025, tayari Serikali imetoa jumla ya Shilingi Bilioni 5.5 kwa ajili ya kununua Lita 458,333, na tayari lita 208,333 zimesambazwa kwenye halmashauri 57 zenye kiwango cha juu cha maambukizi ya malaria kwa awamu ya kwanza. Awamu ya pili ya usambazaji itafuatia kwa kusambaza kwenye Halmashauri 127 zilizobaki na kuweza kufikia na kuzewezesha halmashauri zote 184 kutekeleza afua hiyo.

### *Magonjwa ya Milipuko na Huduma za Afya Mipakani*

***229. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia, kuratibu na kutekeleza afua za ufuatiliaji na udhibiti wa magonjwa ya kuambukiza, milipuko na huduma za afya mipakani. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi

Machi, 2025, Wizara imeendelea **kukabiliana na milipuko ya magonjwa** ikiwemo Kipindupindu, Marburg na Mpox na magonjwa mengine ya milipuko.

***230. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia, kuratibu na kutekeleza afua za ufuatiliaji na udhibiti wa magonjwa ya kuambukiza, milipuko na huduma za afya mipakani. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, **Wizara imeendelea kukabiliana na milipuko ya magonjwa ikiwemo Kipindupindu, Marburg, Mpox** na magonjwa mengine. Aidha, Wizara imefuatilia mwenendo wa mlipuko wa ugonjwa wa Kipindupindu ambapo jumla ya visa 6,940 vilitolewa taarifa kutoka Mikoa 24 nchini isipokuwa Kilimanjaro na Njombe. Hadi kufikia Machi 2025, ugonjwa huo ulikuwa umedhibitiwa katika Mikoa yote 26.

***231. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kufanya ufuatiliaji wa magonjwa yanayoenezwa kwa njia ya hewa yakiwemo UVIKO 19 na mafua makali yanayosababishwa na virusi vya Influenza kupitia vituo 27 vya ufuatiliaji (Sentinel Sites) vilivyopo nchini ambapo hadi kufikia Machi 2025 jumla ya sampuli 2,532 zilipimwa kati ya hizo 190 sawa na asilimia 7.5 zilithibitika kuwa na UVIKO 19. Aidha, sampuli 209 sawa na asilimia 8.3 zilithibitika kuwa na Virusi vya *Influenza*. Vilevile, Wizara imeendelea kufuatilia mwenendo wa mlipuko wa ugonjwa wa Surua nchini katika Mikoa ya Morogoro, Dar es Salaam, Ruvuma, Kagera, Kigoma na Dodoma, ambapo jumla ya visa

63 vilitolewa taarifa na wagonjwa walipata matibabu na kupona.

***232. Mheshimiwa Spika,*** mnamo tarehe 20 Januari 2025, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan alitangaza kuwepo kwa **mlipuko wa ugonjwa wa Marburg** uliotokea katika Wilaya ya Biharamulo mkoani Kagera, baada ya wagonjwa wawili (2) kuthibitika kuwa na maambukizi ya vimelea vya ugonjwa huo. Kufuatia uwepo wa mlipuko huo, Wizara kupitia Kamati ya Kitaalamu ya Udhibiti wa Milipuko ya ngazi ya Taifa ikishirikiana na Uongozi wa Mkoa na Timu ya wataalam zilitekeleza afua za kukabiliana na udhibiti wa mlipuko huo na **hadi kufikia tarehe 13, Machi 2025 tulifanikiwa kuudhibiti na kutangaza kuisha kwa mlipuko ndani ya siku 54.** Aidha, Wizara inaendelea kufuatilia tetesi za magonjwa ya milipuko nchini na kuhakikisha milipuko inadhibitiwa kikamilifu.

***233. Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa **uboreshaji wa miundombinu** hususan katika eneo la dharura, uimarishaji umeendelea katika vituo vya Operesheni za Dharura na Majanga ngazi za Mikoa (Regional Public Health Emergency Operation Centers) na kufikisha Mikoa 20 kati ya 26 nchini. Vituo hivi vimeimarisha uwezo wa Mikoa kuratibu afua za udhibiti wa magonjwa na kuchakata taarifa za tetesi za matukio ya dharura. Taarifa hizi ni sehemu muhimu katika kupanga mikakati na kufanya

maamuzi ya kudhibiti magonjwa hayo katika Mikoa husika.

**Huduma za Afya Mipakani**

***234. Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kudhibiti kuingia nchini kwa magonjwa hatari yanayoambukiza ambapo udhibiti huu unafanyika katika mipaka yote nchini. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi, 2025, **Wizara ilifanya uchunguzi wa awali (Screening) kwa wasafiri 1,175,710** walioingia nchini kutoka nchi zenye mlipuko au uwezekano wa kuwa na magonjwa ya mlipuko. Wasafiri wote hawakuthibitika kuwa na vimelea vya magonjwa ya mlipuko. Vilevile, kati ya wasafiri 389,653 waliotoka katika nchi zinazosadikiwa kuwa na ugonjwa wa homa ya manjano, **wasafiri 8,884** hawakuwa na uthibitisho wa kuchanjwa homa ya manjano, hivyo walipatiwa chanjo hiyo hapa nchini.

***235. Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha udhibiti wa magonjwa mipakani, Wizara imejengea uwezo wataalam na kuwapa magari ya kubebea wahisiwa wa magonjwa ya kuambukiza katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro, viwanja vya ndege vya Songwe na Mwanza pamoja na mipaka ya Holili, Namanga, Tunduma na Mutukula.

***236. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha julai 2024 hadi Machi 2025, Wizara imeajiri watumishi 201 katika ofisi za afya mipakani na hivyo kuongeza idadi

ya watumishi kutoka watumishi 321 hadi 522 kwa ajili ya kuimarisha utekelezaji wa afua mbalimbali za kudhibiti magonjwa katika maeneo ya mipakani. Aidha, kufuatia ongezeko hilo, Wizara imeanzisha ofisi mpya za Afya mipakani na katika maeneo ya kimkakati ambayo ni Bandari za Pangani, Kagunga na Bagamoyo, Mipaka ya Kilambo, Mkunya, Mkenda na Kyaka, Kiwanja cha Ndege Songea na Vituo vya Treni ya Mwendokasi (SGR) vya Dodoma, Morogoro na Dar es Salaam.

**237.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa lengo la kuimarisha udhibiti wa magonjwa ya mlipuko, Wizara imefanya utambuzi wa maeneo muhimu yanayowakutanisha wakazi wa mipakani pamoja na njia kuu wanazotumia na mienendo ya watu wanaoingia na kutoka nchini kupitia mipaka rasmi na isiyo rasmi kwa kushirikiana na nchi za Uganda na Kenya (Joint Population Connectivity Across Borders - PoPCAB). Aidha, Wizara imefanya tathmini ya athari za kiafya (Strategic Risk Assessment) na uandaaji wa mipango ya kukabiliana na dharura (Public Health Contingency Plan) katika mipaka kupitia zoezi la pamoja na nchi jirani za Burundi na Kenya. Matokeo ya tathmini zote hizo yameonesha kwamba mipaka yetu ni salama kwa viwango vinavyokubalika Kitaifa na Kimataifa.

**238.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Wizara imeratibu mafunzo ya ana kwa ana ya matibabu ya magonjwa ya milipuko ya Kipindupindu, Mpox na Marburg kwa watoa huduma

2,581 katika Mikoa ya Mwanza, Geita, Kigoma, Kagera, Dar es Salaam, Morogoro, Katavi, Mbeya, Songwe, Singida, Simiyu, Dodoma na Tabora. Vilevile, jumla ya watoa huduma 62 wamepata mafunzo ya usimamizi na uendeshaji wa vituo vya operesheni za dharura na maafa katika Mikoa ya Tabora, Manyara, Ruvuma, Mbeya, Rukwa na Kigoma.

***‘Naomba kuwahakikishia wananchi kuwa, mipaka yetu ipo salama na Serikali imejipanga kukabiliana na magonjwa ya mlipuko na ya kuambukiza kutoka nchi za jirani’.***

**Utoaji wa Huduma za Kinga**

**Huduma za Chanjo**

239. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia na kuimarisha utoaji wa huduma za kinga ikiwemo kuhakikisha huduma za chanjo na vifaa vya kutolea chanjo vinapatikana muda wote kulingana na mahitaji. Lengo ni kuhakikisha kuwa watoto wote wenye umri chini ya mwaka mmoja, chini ya miaka mitano, wajawazito, wasichana wenye umri wa miaka 9 hadi 14, wasafiri na makundi mengine yaliyo katika hatari ya magonjwa yanayozuilika kwa chanjo wanapata huduma hizo kwa wakati. Chanjo hizo zimekuwa zikitolewa katika vituo vya kutolea huduma za afya na ngazi ya jamii kupitia huduma mkoba na huduma tembezi.

240. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha mnyororo baridi wa huduma za chanjo, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imejenga maghala tisa (9) ya kuhifadhia chanjo pamoja na kununua magari 96 ambapo kati ya hayo, *Pick up Double Cabin ni* 68, malori 28 na pikipiki 300 kwa ajili ya kutoa huduma za chanjo nchini. Makabidhiano ya magari hayo na pikipiki yalifanywa na Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 1 Desemba 2024. Aidha, uimarishaji huo umesaidia kupunguza gharama za uendeshaji kutoka Shilingi Bilioni 18 hadi Shilingi Bilioni 1.8 mwaka 2024 pamoja na kuimarisha upatikanaji wa chanjo kwa wakati.

241. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuhakikisha **chanjo za watoto** za kuwakinga na magonjwa 13 yanayozuilika kwa chanjo zinazopatikana bila malipo kulingana na mahitaji. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025 Wizara imeratibu ununuzi wa chanjo za Rota; dozi 6,312,125 kwa ajili ya kukinga ugonjwa wa kuhara kwa watoto; PCV - 13 dozi 2,366,400 kwa ajili ya kukinga watoto dhidi ya ugonjwa wa Nimonia; chanjo za Surua Rubella; dozi 4,200,000 kwa ajili ya kukinga watoto dhidi ya ugonjwa wa Surua na Rubella; bOPV dozi 8,034,300 kwa ajili ya kukinga ugonjwa wa kupooza (Polio), Pentavalent dozi 3,034,300 kwa ajili ya kukinga Donda Koo, Kifaduro, Pepopunda, Homa ya Ini, na Mafua ya Influenza, *Tetanus Diphtheria* dozi 1,400,000 kwa ajili ya

kukinga ugonjwa wa Pepo Punda, BCG dozi 3,200,000 za kukinga watoto dhidi ya ugonjwa wa Kifua Kikuu na IPV dozi 2,304,200 kwa ajili ya kukinga ugonjwa wa kupooza (Polio).

**242.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 kulikuwa na jumla ya dozi za chanjo 13,416,045 nchi nzima katika maghala ya kuhifadhia chanjo. Kwa mgawanyo wa ROTA dozi 982,125, (MR) dozi 3,139,500, (PCV-13) dozi 4,583,200, (IPV) dozi 440,250, (PENTA) dozi 2,689,060, (Td) dozi 789,320, (bOPV) dozi 291,000, (BCG) dozi 96,000 na HPV dozi 396,590 baada ya kufanya usambazaji kwenye mikoa nchi nzima, hali hii inaonesha kuwa upatikanaji wa chanjo nchini ni wa kutosheleza.

**243.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutoa **huduma za chanjo kupitia katika vituo vya kutolea huduma za afya** na katika huduma Mkoba na tembezi ili kuhakikisha watoto wote wanaohitaji huduma ya chanjo, wanafikiwa na huduma hiyo. Wizara iliweka lengo la kuchanja jumla ya watoto 3,114,061 ambapo hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya watoto 2,995,318 sawa na asilimia 96 walichanjwa chanjo ya Penta-3 ambayo hutumika kama kipimo kikuu cha utoaji wa chanjo nchini kwa watoto wa chini ya mwaka mmoja.

**244.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa **Chanjo za kukinga ugonjwa wa Polio,** jumla ya watoto 2,896,495 sawa na asilimia 93 walipatiwa chanjo ya

matone (OPV3) na watoto 3,025,922 sawa na asilimia 97 walipatiwa chanjo ya sindano (IPV). Aidha, watoto 3,094,604 sawa na asilimia 99 walipatiwa chanjo ya Surua Rubella dozi ya kwanza na Watoto 2,903,356 sawa na asilimia 93 walipatiwa chanjo ya Surua Rubella dozi ya pili. Vilevile, watoto 3,761,937 sawa na asilimia 114 walichanjwa chanjo ya BCG kwa ajili ya kukinga kifua kikuu. Kwa wastani hali ya utoaji wa chanjo nchini ni nzuri na inaendelea kuimarika kulingana na malengo yaliyowekwa.

***245. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuwalinda **wasichana wenye umri wa miaka 9 hadi 14 dhidi ya Saratani ya mlango** wa kizazi kwa kununua na kusambaza chanjo ya *Human Pappiloma Virus* (HPV) dozi 4,763,180. Hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya wasichana wapatao 4,989,818 walipatiwa chanjo ya HPV sawa na asilimia 112 ya walengwa, ili kuwakinga dhidi ya saratani ya mlango wa kizazi. Aidha, katika maghala ya chanjo kulikuwa na chanjo za HPV dose 659,470.

## Huduma za Lishe

***246. Mheshimiwa Spika,*** Lishe bora ni muhimu kwa uhai, ukuaji na maendeleo ya binadamu kiakili na kimwili na hivyo huchangia katika kuongeza tija katika uzalishaji mali kwa kaya na kuimarisha uchumi wa Taifa kwa ujumla. Katika kuhakikisha hilo linafanikiwa, Wizara imeendelea kutekeleza Mpango Jumuishi wa pili wa Kitaifa wa Lishe (National Multisectoral Nutrition Action Plan (2021/22 – 2025/26). Kupitia Mpango huo Wizara imekuwa

ikitekeleza afua za lishe zilizothibishwa kuwa na matokeo makubwa ili kukabiliana na matatizo ya utapiamlo wa lishe duni na ule wa lishe ya kuzidi. Baadhi ya afua hizo ni pamoja na utoaji wa matone ya Vitamini A, kinga na matibabu ya utapiamlo mkali, uongezwaji wa virutubishi vya madini na vitamini kwenye vyakula na utoaji elimu kwa jamii kuhusiana na masuala ya lishe kwa ujumla wake.

**247.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inatambua kuwa maziwa ya mama ni hitaji muhimu la mtoto pindi anapozaliwa hadi anapotimiza umri wa miaka miwili (2) au zaidi huku akiendelea kupewa vyakula mchanganyiko vya nyongeza kutoka katika makundi yote ya vyakula ili kupata virutubishi vyote muhimu kwa afya na ukuaji wake. Katika kutekeleza hilo, Wizara, imeendelea kusimamia miongozo inayosisitiza **unyonyeshaji sahihi wa Watoto**, ambapo katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 **jumla ya Watoto 1,145,739 walinyonyeshwa maziwa ya mama pekee** ndani ya saa moja baada ya kuzaliwa, ambayo ni sawa na asilimia 93 ya lengo, ikilinganishwa na asilimia 92 ya kipindi kama hicho mwaka 2024. Aidha, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya watoto 1,536,286 wamenyonyeshwa maziwa ya mama pekee sawa na asilimia 93 ya lengo. Ili kuhakikisha hali ya unyonyeshaji maziwa ya mama pekee inaongezeka, Wizara iliratibu maadhimisho ya Wiki ya Unyonyeshaji Kitaifa Agosti 2024, ambayo yaliambatana na mkutano wa Maafisa Utumishi na Maafisa Sheria kwa lengo la kuhamasisha

utekelezaji wa haki za uzazi mahala pa kazi ikiwemo kuweka mazingira wezeshi kwa wanawake kunyonyesha watoto wakiwa katika shughuli za kiuchumi au maeneo ya ajira.

***248. Mheshimiwa Spika,*** huduma ya **utoaji wa matone ya Vitamini A** kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano (5) hufanyika katika vituo vya kutolea huduma za afya kwa utaratibu wa kawaida ambapo mtoto akitimiza umri wa miezi sita (6) hupewa matone ya Vitamini A na huendelea kupatiwa matone hayo kila baada ya miezi sita (6) hadi atakapotimiza umri wa miaka mitano (5). Aidha, Wizara imeendelea kutekeleza Kampeni ya Kitaifa ya utoaji wa matone ya Vitamini A kwa watoto walio chini ya miaka mitano. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, malengo ya kampeni yalikuwa ni kutoa matone ya Vitamin A kwa watoto 9,468,207 wenye umri wa kati ya miezi 6 mpaka miezi 59 nchi nzima. Jumla ya watoto 9,456,378 walipatiwa matone ya vitamin A ambayo ni sawa na asilimia 99.8 ya lengo.

***249. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu na wadau mbalimbali, imeendelea kuhamasisha na kuelimisha makundi mbalimbali katika jamii kuhusu masuala ya lishe na mtindo bora wa maisha kupitia majukwaa mbalimbali ikiwemo maadhimisho ya **Siku ya Lishe Kitaifa** yaliyofanyika mwezi Oktoba 2024 katika Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara yakiwa na kaulimbiu isemayo **"Mchongo ni Afya Yako, Zingatia Unachokula"**. Lengo kuu la maadhimisho hayo lilikuwa ni kutoa

elimu ya lishe kwa jamii. Kupitia maadhimisho hayo, jumla ya Watalaam wa afya na Lishe nchini wapatao 200 walijengewa uwezo kuhusu masuala ya ulaji unaofaa na mitindo bora ya maisha. Wakati wa maadhimisho hayo, jumla ya vipindi 208 vya masuala ya lishe viliandaliwa na kurushwa kwenye vyombo mbalimbali vya habari vikiwemo redio, runinga, magazeti na mitandao ya kijamii katika ngazi zote nchini.

***250.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuhamasisha wananchi **kutumia vyakula ambavyo vimeongezwa virutubishi muhimu** kwa maendeleo ya ukuaji wa afya ya watoto ili kuboresha afya zao na kuwakinga na maradhi mbalimbali yanayoweza kuzuilika kwa kula lishe bora yenye virutubisho vya madini na vitamini, iodini kwenye chumvi na vitamin A kwenye mafuta ya kula. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya mashine 230 za kunyunyizia virutubishi (Dosifiers) kwenye vyakula zimefungwa katika Mikoa 26 nchini na hivyo kufikia jumla ya mashine 1,402 ukilinganisha na machine 1,172 zilizokuwepo katika kipindi kama hiki mwaka 2024. Aidha, kufuatia uwepo wa mazingira wezeshi ya uzalishaji wa virutubishi, jumla ya kilo 65,946 za virutubishi zimezalishwa na kusambazwa nchini.

**Afya Mazingira na Usafi**

***251.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na wadau pamoja na Mikoa na Halmashauri imeendelea kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa afua mbalimbali zilizopo katika mradi wa Afya Mazingira

na Usafi: *Sustainable Rural Water Supply and Sanitation* (SRWSS) 2020-2026, unaotekelezwa katika Halmashauri za Wilaya 137. Lengo la Mradi ni kuvifikia vituo 2,636 vya kutolea huduma za afya ifikapo 2025, ambapo hadi kufikia Machi 2025 jumla ya vituo 2,740 vya kutolea huduma za afya vimefikiwa.

***252.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Afua zilizotekelezwa ni pamoja na kuwezesha ujenzi na matumizi ya vyoo bora, uwekaji wa vifaa vya kunawa mikono, udhibiti wa taka, usafishaji wa maeneo ya makazi, maeneo ya biashara na maeneo ya umma ili kuikinga jamii dhidi ya magonjwa mbalimbali kama vile Kipindupindu, Kuhara Damu, Dengue, Malaria na magonjwa mengine ya kuambukiza. Katika kuboresha suala la usimamizi wa mradi huo ngazi ya mikoa, Wizara imenunua na kusambaza jumla ya magari 21 na pikipiki 410.

***253.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza Kampeni ya ***FANYA KWELI USIBAKI NYUMA-MTU NI AFYA inayohamasisha*** ujenzi na matumizi ya Vyoo bora, kuzingatia kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni katika nyakati maalum, hedhi Salama, usafishaji wa maeneo ya makazi na kazi (Mita tano Usafi Wangu, Usafi Wangu Mita Tano, udhibiti wa utupaji ovyo wa taka, lishe Bora, mazoezi ya mwili, nishati Safi na maji salama ya kunywa). Utekelezaji wa Kampeni hii umesaidia kuongeza idadi ya kaya zenye vyoo bora kutoka kaya 8,277,206 mwezi Machi, 2024 na kufikia kaya

8,504,503 mwezi Machi, 2025 sawa na asilimia 78.4 ya lengo. Aidha, kaya zenye vifaa vya kunawia mikono kwa maji tiririka na sabuni zimeongezeka kutoka asilimia 41.4 hadi asilimia 45.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2024.

### Udhibiti wa Magonjwa Yaliyokuwa Hayapewi Kipaumbele (NTDs)

***254.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutoa kipaumbele katika kutekeleza afua za kutokomeza magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele ambayo ni Matende, Mabusha, Vikope, Trakoma, Usubi, Kichocho na Minyoo ya Tumbo. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Wizara imetoa kingatiba dhidi ya ugonjwa wa matende na mabusha kwa jumla ya watu 530,034 sawa na asilimia 96.5 ya walengwa katika Halmashauri tano (5) za Mtama, Mikindani, Kinondoni, Pangani na Lindi. Aidha, jumla ya wananchi 1,603,419 sawa na asilimia 81.5 ya walengwa walipata kingatiba dhidi ya ugonjwa wa Trakoma katika Halmashauri saba (7) za Longido, Monduli, Ngorongoro, Kiteto, Mpwapwa, Simanjiro na Kalambo zenye maambukizi ya juu ya ugonjwa huo. Vilevile, Wizara ilitoa kingatiba kwa wananchi 5,456,029 dhidi ya ugonjwa wa Usubi sawa na asilimia 85 ya walengwa katika Halmashauri 24 za mikoa ya Ruvuma, Iringa, Njombe na Morogoro. Wizara imetoa **kingatiba ya kudhibiti ugonjwa wa kichocho kwa watoto** 7,134,762 sawa na asilimia 76 na kingatiba dhidi ya ugonjwa wa minyoo ya

tumbo kwa Watoto 9,167,116 sawa na asilimia 83 ya walengwa.

**255.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutoa huduma za tiba kwa kufanya upasuaji wa mabusha na vikope. Huduma za upasuaji wa mabusha zilitolewa kwa njia ya kambi katika Hospitali za Wilaya ya Bagamoyo, Masasi Mji, Kisarawe, Handeni DC, Korogwe DC na Korogwe TC ambapo jumla ya wagonjwa 1,084 walipata huduma hiyo ikilinganishwa na wagonjwa 617 kipindi kama hiki mwaka 2024.

**256.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imewajengea uwezo watumishi katika vituo 40 vya kutolea huduma za afya juu ya kutoa huduma za matibabu ya matende. Aidha, Wizara imewajengea uwezo Wahudumu wa Afya ngazi ya Jamii 200 katika kuibua wagonjwa wa Matende na Mabusha katika Halmashauri za Bagamoyo, Masasi na Masasi Mji. Pia, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Wizara ilitoa huduma za upasuaji mdogo wa usawazishaji wa Vikope kwa wagonjwa 1,772 katika Halmashauri za Wilaya 13. Lengo la upasuaji huo ni kuzuia wananchi walioathirika na ugonjwa wa vikope kupata ulemavu wa kutoona.

**Elimu ya Afya kwa Umma na Huduma za Afya Ngazi ya Jamii**

257. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo imeendelea kutoa elimu kwa jamii, ili kuhakikisha jamii inakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu njia mbalimbali za kujikinga na magonjwa yanayoambukiza na yale yasiyoambukiza. Hii inaenda pamoja na utoaji wa elimu kuhusu masuala ya lishe, mazoezi, magonjwa ya mlipuko, chanjo, afya ya uzazi, mama na mtoto.

258. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha hilo linafanikiwa, Wizara inatekeleza Mpango Jumuishi wa Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii ambapo kupitia mpango huo jumla ya wahudumu wa afya ngazi ya jamii 12,832 katika Mikoa 12 ya Pwani, Mbeya, Kagera, Njombe, Songwe, Lindi, Geita, Kigoma, Tabora, Dodoma, Tanga na Ruvuma wamechaguliwa kuingia katika mafunzo maalum yanayohusiana na utoaji huduma katika ngazi ya jamii, pamoja na elimu. Hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya wahudumu wa afya ngazi ya jamii 3,706 wamehitimu mafunzo hayo na wengine 4,309 wanaoendelea na mafunzo katika vyuo 45 nchini.

259. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Wadau imeanzisha programu ya elimu na hamasa ya matumizi ya huduma ya m-mama. Programu hiyo inakusudia kuiwezesha jamii kuwasaidia wajawazito, waliojifungua ndani ya siku 42 au watoto wachanga ndani ya siku 28 wenye changamoto ya dharura za

kiafya kupata huduma ya usafiri na matibabu kwa haraka. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, wanahabari 200 wamejengewa uwezo, vipindi 30 vya redio na runinga vimeandaliwa na kurushwa, vipeperushi mbalimbali vimeandaliwa na kusambazwa pamoja na uhamasishaji kupitia mitandao ya kijamii.

**260.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeandaa na kusambaza vielelezo vya kuelimisha na kuhamasisha jamii kuhusu elimu ya afya kwa Umma kulingana na kalenda ya matukio ya afya ya kitaifa na kimataifa. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya picha mjongeo 920 na vipeperushi vya mtandaoni 1,440 vimesambazwa kupitia mitandao mbalimbali ya kijamii. Aidha, katika kipindi hicho, jumla ya matangazo ya redio 12 yamerushwa mara 22,680 kupitia vituo vya redio vinane (8), matangazo mafupi ya redio 10, vipindi vya redio 44, vipindi vya runinga 26, picha mjongeo 48 ambazo zimesambazwa kupitia mitandao ya kijamii na vipeperushi vya mtandaoni aina 26 vimeandaliwa na kusambazwa.

**261.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeandaa na kusambaza vielelezo vya kuelimisha na kuhamasisha jamii kuhusu tishio la ugonjwa wa *Mpox* na *Marburg*. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, jumla ya vielelezo vilivyoandaliwa na kusambazwa ni mabango nakala 84,000, matangazo nane (8) ya redio yamerushwa mara 5,760, picha mjongeo 16 zimesambazwa kupitia mitandao ya

kijamii sambamba na kuandaa kanzidata ya kidijitali ya kuhifadhi vielelezo vya uelimishaji na uhamasishaji jamii kuhusu masuala ya afya.

262. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha ushirikishwaji wa jamii katika kujikinga na kukabiliana na magonjwa ya mlipuko ikiwemo kuwajengea uwezo viongozi 70 wa dini na waandishi wa habari 150 kuhusu utoaji wa elimu ya kujikinga na magonjwa ya mlipuko nchini. Wizara pia inaendesha kituo cha kupokea simu na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu masuala ya afya (Afya Call Center) ambapo wananchi hupatiwa majibu ya maswali, ufafanuzi na hoja mbalimbali zinazoibuliwa katika jamii. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, jumla ya wananchi 527,284 walipiga simu na katika simu hizo, simu 416,577 sawa na asilimia 79 zilipokelewa na kupatiwa huduma. Miongoni mwa masuala yaliyoulizwa kwa wingi ni magonjwa ya mlipuko asilimia 41, magonjwa ya kuambukiza asilimia 12, bima ya afya asilimia 21, magonjwa yasiyoambukiza asilimia 9, afya ya uzazi asilimia 7, lishe asilimia 4, afya ya akili asilimia 2 pamoja na matumizi sahihi ya dawa asilimia 4.

263. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo kwa kipindi tajwa imefanya uhamasishaji na uelimishaji kupitia njia mbalimbali ikiwemo kampeni na kutembelea Shule za Msingi na Sekondari katika mikoa 19. Jumla ya wanafunzi 198,000 wameelimishwa kuhusu lishe, magonjwa ya milipuko, afya ya uzazi, chanjo dhidi ya HPV na

kuhamasisha tabia zinazozingatia kanuni za afya na mitindo bora ya maisha.

### Huduma za Dawa, Vifaa, Vifaa Tiba na Vitendanishi

***264.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutoa kipaumbele katika upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi vya maabara vyenye ubora, ufanisi na vilivyo salama kwenye vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Wizara kupitia Bohari ya Dawa (MSD) imeendelea kuzalisha, kununua, kutunza na kusambaza aina mbalimbali za dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi.

***265.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha upatikanaji wa bidhaa za afya, Serikali imeendelea kutoa fedha za ruzuku kwenye vituo kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa za afya kupitia Bohari ya Dawa (MSD). Katika Kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya Shilingi Bilioni 183.2 sawa na asilimia 91.6, zimetolewa kati ya Shilingi Bilioni 200 ya bajeti ya fedha za ruzuku. Aidha katika kuimarisha hali ya upatikanaji wa bidhaa za afya katika Bohari ya Dawa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali imefanikiwa kutoa kiasi cha Shilingi Bilioni 50 kama mtaji wa kuboresha upatikanaji wa dawa nchini. Vilevile, vituo vya kutolea huduma za afya vimeweza kuchangia kiasi cha Shilingi Bilioni 126.6 kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa za afya. Katika kukabiliana na mabadiliko ya ufadhili na kisiasa kutoka kwa wadau, Serikali imetoa kiasi cha Shilingi Bilioni 93.5 kwa ajili ya ununuzi wa

dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI na vitendanishi vya maabara na hivyo kufikia jumla ya Shilingi Bilioni 370.1.

***266.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vya kuzalisha dawa, vifaa tiba na vitendanishi nchini kununua maji tiba kutoka viwanda vya ndani ya nchi, kutoa msamaha wa kodi kwa vifungashio vya bidhaa za afya na Sheria mpya ya Ununuzi wa Umma kuruhusu wazalishaji kulipwa malipo ya awali ya hadi asilimia 30 baada ya kusaini mkataba wa ununuzi.

***267.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuendeleza viwanda vya dawa nchini, Jumla ya Shilingi Bilioni 10 zimetolewa na kuelekezwa kiwanda cha viuadudu kilichopo Kibaha mkoa wa Pwani. Fedha hizo zimewezesha ununuzi wa lita 833,333.3 ambazo zinaendelea kusambazwa katika Halmashauri zote nchini. Aidha, upatikanaji wa fedha hizo zimeboresha uhusiano wetu na nchi ya Cuba na kupelekea kukamilika kwa makubaliano ya uhaulishaji wa teknolojia (Technology Transfer).

***'Nitoe wito kwa Halmashauri zote zilizopokea na zinazoendelea kupokea viuadudu hivyo kutekeleza afua za unyunyuziaji katika maeneo yote yenye mazalia ya Mbu'.***

***268.*** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia upatikanaji wa fedha hizo, hali ya upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi aina 382 nchini imeimarika kufikia

wastani wa asilimia 86.2 katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 79 kwa kipindi kama hicho mwaka 2024. Hali ya upatikanaji wa dawa kwenye Zahanati asilimia 77, Vituo vya Afya asilimia 78, Hospitali za Wilaya asilimia 79, Hospitali za Rufaa za Mikoa asilimia 98 na Hospitali za Kanda, Maalum na Taifa asilimia 99. Aidha, upatikanaji wa dawa muhimu za kipaumbele 382 katika Bohari ya Dawa (MSD) umefikia asilimia 68 katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 61 katika kipindi kama hicho Mwaka 2024.

**269.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kufanya ufuatiliaji wa bidhaa za afya katika vituo vyote vya umma vya kutolea huduma za afya nchini kwa lengo la kuhakikisha dawa na bidhaa nyingine za afya zinawafikia walengwa. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya vituo 90 vya kutolea huduma za afya katika mikoa 14 vilifikiwa na zoezi hilo. Aidha, katika kipindi hicho, Wizara iliweza kuwajengea uwezo watumishi 3,220 kutoka vituo 1,579 ili waweze kuimarisha usimamizi,upatikanaji na utolewaji huduma za dawa na bidhaa nyinginezo za afya kwa wananchi. Vituo ambavyo watumishi wake walijengewa uwezo, ni vile ambavyo vilikuwa vimebainika kuwa na upungufu kutokana na taarifa za usimamizi shirikishi, usimamizi wa ubora wa mnyororo wa ugavi pamoja na taarifa za mfumo wa kuagiza na kutoa taarifa za bidhaa za afya.

270. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea na utekelezaji wa kampeni ya Kitaifa ya kujenga uelewa kwa jamii juu ya athari za **Usugu wa Vimelea vya Magonjwa dhidi ya Dawa.** Kampeni hii inaitwa **Holelaholela Itakukosti** ambayo imetekelezwa kwa kutumia majukwaa na njia mbalimbali za mawasiliano na kufikia jamii na rika mbalimbali. Aidha, kampeni hii imetajwa kuwa kampeni ya kipekee ya mfano wa kuigwa barani Afrika kwa mujibu wa taarifa ya *African CDC AMR Landmark report, August 2024. S*ambamba na hili, Tanzania imeshinda tuzo ya Afrika ya wanahabari kinara katika kampeni ya usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa (UVIDA) kupitia kampeni ya "Holela-holela Itakukosti".

271. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 Wizara imetoa mafunzo ya ufuatiliaji wa UVIDA katika hospitali za umma 23, Binafsi sita (6) na Mashirika ya dini nne (4). Mafunzo hayo yamewezesha kuongezeka kwa upatikanaji wa takwimu zinazohusu usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa na kuweza kutolewa taarifa kwenye mifumo ya kimataifa. Aidha, kufuatia jitihada zinazofanywa na Wizara, zimewezesha nchi kutambulika na Shirika la Afya Duniani (WHO) na kushika nafasi ya kwanza barani Afrika kwa kupata asilimia 80.3 kwenye eneo la ufuatiliaji wa matumizi ya dawa za *antimicrobials*. Vilevile, katika uimarishaji wa mfumo wa upimaji wa sampuli za UVIDA, Wizara imeongeza idadi ya upimaji kutoka sampuli 7,920

hadi 43,907 sawa na asilima 81.9 kwa kipindi cha mwaka 2020 hadi 2023.

**272.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha udhibiti wa wizi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi, Serikali imeendelea kutumia mifumo ya TEHAMA katika kusimamia uagizaji, utunzaji na matumizi kuanzia ngazi ya Bohari ya Dawa (MSD) hadi vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Sambamba na hilo Serikali imeweka alama ya utambuzi ya "GOT" (*Government of Tanzania)* kwenye bidhaa za afya ili kuzuia usambazaji usio halali. Aidha, Serikali inaendelea kufanya ufuatiliaji, usimamizi na kujenga uwezo kwa timu za ngazi ya Mkoa na Halmashauri ili kuongeza uwazi, uwajibikaji na matumizi sahihi.

### Huduma za Uchunguzi wa Magonjwa

**273.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha huduma za uchunguzi wa magonjwa na matengenezo ya vifaa tiba katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini, kwa kuwekeza kwenye maeneo makuu matatu ya maabara, radiolojia na matengenezo ya vifaa tiba.

**274.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Wizara imeongeza **maabara 883 na kufanya jumla ya maabara kufikia 11,665** ikilinganishwa na maabara 10,782 kipindi kama hicho mwaka 2024. Kati ya maabara hizo, 7,383 ni za Serikali na 4,282 ni za binafsi. Aidha, katika kipindi

cha Julai 2024 hadi Machi 2025 maabara 14 zilipata Ithibati na kufikia 89 kutoka maabara 75 kwa mwaka 2024. Kati ya maabara hizo, ngazi ya Taifa (03), Maalum (06), Kanda (05), Mikoa (31), Halmashauri (15), Binafsi (23) na sita (6) ni za Mpango wa Taifa wa Damu Salama ambapo vipimo vinavyofanyika katika maabara hizi vinaaminika na kukubalika duniani kote. Vilevile, kwa kuwa ubora wa huduma unaenda sambamba na usalama dhidi ya vimelea vya magonjwa, jumla ya makabati maalum 15 ya usalama wa vimelea yamenunuliwa na kusimikwa katika maabara ngazi ya Halmashauri ambazo hazikuwa na makabati hayo, ili kuimarisha usalama wa watoa huduma dhidi ya vimelea vya magonjwa ya kuambukiza.

***275. Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha **huduma za radiolojia** nchini, Wizara imefanikisha kusimika Mashine za *Digital X-ray* katika Hospitali za Rufaa za Mikoa ya Tabora - Kitete, Kigoma - Maweni na huduma tayari zimeanza kutolewa. Aidha, usimikaji wa *PET CT Scan* katika Taasisi ya Saratani *Ocean Road* umekamilika na huduma za uchunguzi wa viashiria vya awali vya ugonjwa wa saratani tayari zimeanza kutolewa na hivyo kufikia jumla ya CT scan 45, MRI 13, *Digital X-ray* 491 na *Ultrasound* 970 katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Vilevile, Serikali imenunua na kusimika mashine 68 za *X-ray* za kidijitali zenye thamani ya Shilingi Bilioni 13.5 na kuzisimika katika hospitali na vituo vya Afya ngazi ya msingi katika mikoa ya Kigoma, Dodoma, Njombe, Katavi, Shinyanga, Tabora, Pwani, Tanga,

Ruvuma, Lindi, Mwanza, Morogoro, Iringa, Mbeya, Kilimanjaro, Dar es Salaam, Arusha, Singida na Geita.

***276.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki, Wizara imefanikiwa kusimika **mitambo 25 ya kuzalisha hewa tiba ya oksijeni** nchini. Aidha, imefanyika tathmini ya mahitaji ya kupata chanzo mbadala cha kuzalisha na kusambaza hewa tiba ya oxygen katika mfumo wa kimiminika (Liquid Oxygen) kwa vituo 28. Awamu ya kwanza ya usimikaji wa matenki ya kuhifadhi hewa tiba ya Oksijeni katika mfumo wa kimiminika umeanza katika Hospitali ya Taifa Muhimbili – Upanga, Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI), Hospitali za Rufaa za Mikoa za Temeke na Mwananyamala.

***277.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha uwekezaji uliofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita kwenye kuboresha huduma za uchunguzi nchini, Serikali imeajiri **wahandisi na mafundi Sanifu wa Vifaa tiba wapatao 81 na kufanya Idadi ya wataalam hao kufikia 490** katika ngazi zote za utoaji wa huduma za Afya. Jumla ya wataalam 40 wamejengewa uwezo katika maeneo mbalimbali ya usimikaji, matengenezo kinga na ukarabati wa vifaa tiba ndani ya nchi na nje ya nchi. Aidha, jumla ya watoa huduma za afya 16 kutoka vituo mbalimbali vya kutolea huduma za afya nchini wamepatiwa mafunzo ya matumizi na utunzaji wa mfumo wa kielektroniki wa kutolea taarifa za utendaji kazi wa vifaa tiba.

**278.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeanzisha na kuimarisha karakana sita (6) zilizopo Hospitali za Bugando (Kanda ya Ziwa Victoria), Mbeya (Kanda ya Nyanda za Juu Kusini), Mtwara (Kanda ya Kusini), Hospitali ya Taifa Muhimbili (Kanda ya Mashariki), Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe (Kanda ya Kati) na Hospitali ya KCMC (Kanda ya Kaskazini) kwa ajili ya ukarabati na matengenezo kinga ya mashine na mitambo ilisimikwa nchini. Vituo hivyo pia vinatoa mafunzo kwa wataalam wa ufundi wa vifaa na vifaa tiba katika usimamizi na matengenezo kinga kwa vifaa tiba vyote. Aidha, Wizara imeendelea kuhuisha na kutoa miongozo mbalimbali ya kusimamia ubora wa mashine na mitambo hiyo. Vilevile, Wizara inaendelea kusimamia mfumo wa kieletroniki wa usimamizi wa vifaa tiba na miundombinu (MEIMIS) ili kuwezesha ufuatiliajia wa karibu na matengenezo kinga kwa wakati.

**Mpango wa Taifa Wa Damu Salama**

**279.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Wizara imeendelea kuhakikisha uwepo wa damu salama ya kutosha nchini ambapo**jumla ya chupa za damu 418,609 zilikusanywa nchini** ambazo ni sawa na asilimia 94.5 ya lengo la kukusanya chupa za damu 442,972 ikilinganishwa na malengo ya kukusanya chupa za damu 442,764 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Makusanyo hayo yametokana na jitihada za pamoja kati ya Mpango wa Taifa wa Damu Salama

(NBTS), Wadau mbalimbali, Madhehebu ya Dini, Timu za Ukusanyaji Damu za Halmashauri pamoja na Timu za Hospitali za Rufaa za Mikoa katika ukusanyaji wa damu salama nchini.

***280.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki, Wizara imeanza taratibu za kuhakikisha vituo vya vya Damu Salama Kanda ya Kati Dodoma, Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali ya Benjamini Mkapa, Hospitali za Rufaa za Mikoa ya Iringa, Njombe na Kigoma vinaanza mchakato wa kutambuliwa na kupata cheti cha ithibati katika utoaji huduma za damu salama kwa viwango vya Kitaifa na Kimataifa.

**Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii**

***281.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2024 mpaka Machi 2025, Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii imefanikiwa **kupima jumla ya Sampuli 60,224 za magonjwa mbalimbali ya mlipuko pamoja na upimaji wa anuai za magonjwa hayo**. Sampuli hizo zinahusisha uchunguzi wa magonjwa yakiwemo Mpox, Marburg, mafua makali, Kipindupindu, Surua, *Rubella*, Kimeta, *Dengue*, kichaa cha mbwa (Rabies), matende, *Rotavirus, Human Papiloma*, wingi wa Virusi vya UKIMWI, utambuzi wa maambukizi ya VVU kwa watoto wachanga.

***282.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara **imesimika mashine kwa ajili ya upimaji wa ugonjwa wa Saratani ya Shingo ya Kizazi "Alinity - M"** ambapo baada ya usimikaji zoezi rasmi la uchunguzi wa ugonjwa huo

umeanza kufanyika kupitia Maabara ya Taifa. Aidha, Maabara ya Taifa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuboresha huduma za Maabara nchini kwa kununua mashine za kisasa aina ya *Next Generation Sequencers* sambamba na mashine kubwa aina ya *Illumina Nextseq 1000* kwa ajili ya kuchakata sampuli nyingi na kwa kiwango cha juu kwa mara moja.

***283.*** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara katika kuhakikisha inakabiliana na magonjwa ya mlipuko nchini, imeimarisha huduma za uchunguzi kwa kuwa na **mashine mbili (2)** za **iSeq 100** kwa ajili ya maabara jongezi (BSL-3 Mobile Laboratories) inayoweza kutumika mahali popote inapotokea mlipuko wa magonjwa. Maabara jongezi hiyo ndiyo iliyotumika kuthibitisha uwepo wa virusi vya ugonjwa wa *Marburg* katika milipuko ya mwaka 2023 na 2025 mkoani Kagera. Aidha, maabara hii imeendelea kutumika katika kubaini anuai za vinasaba vya vimelea vya magonjwa ya mlipuko ambayo ilisaidia wataalam wa afya kufanya jitihada za kutokomeza ugonjwa huo kwa muda mfupi.

***284.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Maabara ya Taifa imefanyiwa ukaguzi na kupata Ithibati ISO:15189:2022 kwa ajili ya usimamizi wa ubora wa vipimo wa Kitaifa na Kimataifa na ISO:17043:2010 kwa ajili ya kutengeneza na kusambaza sampuli za kuhakiki ubora wa huduma za maabara nchini. Katika kipindi cha Julai 2024 mpaka Machi, 2025 maabara imefanikiwa kuandaa na kutuma sampuli za uhakiki

ubora wa vipimo kwa vituo 600 nchi nzima kwa ajili ya kuhakiki ubora wa vipimo mbalimbali vinavyotolewa na Maabara nchini. Zoezi hilo linalenga kuendelea kupata na kudumisha ubora wa huduma za maabara katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini.

### Huduma za Uuguzi na Ukunga

***285.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inatambua kuwa huduma za Uuguzi na Ukunga ni mhimili muhimu katika utoaji wa huduma za afya hapa nchini kwani asilimia 80 ya huduma za Afya zinatolewa na Wauguzi na Wakunga. Hivyo basi, Wizara imeendelea kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora kwa kuwajengea uwezo watoa huduma ili kuweza kutoa huduma zenye staha kwa **kuzingatia utu, heshima na mawasiliano madhubuti**. Hadi kufikia Machi 2025, **jumla ya madawati 400** ya Huduma kwa Mteja yameanzishwa katika vituo vya kutolea huduma kwa ngazi zote ili kusaidia wananchi kupata huduma kwa urahisi ikiwa ni pamoja na kufanyia kazi changamoto mbalimbali wakati wa utoaji huduma. Aidha, watoa huduma 12,000 wamejengewa uwezo juu ya utoaji huduma staha ukilinganisha na watumishi 6,544 waliojengewa uwezo kwa mwaka 2024. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 83.

***286.*** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza uwajibikaji wa watoa huduma katika kuimarisha ubora wa huduma, Wizara imezindua rasmi Kauli Mbiu ya Ubora wa

Huduma katika Sekta ya Afya inayosema,”**HUDUMA BORA WAJIBU WANGU”.** Kauli Mbiu hii ilizinduliwa rasmi katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Wauguzi Viongozi wa ngazi zote pamoja na taasisi za mafunzo uliofanyika kuanzia tarehe 18 hadi 20 Machi 2025 . Kauli mbiu hii ambayo itawekwa kwenye mageti na milango ya vituo vyote vya kutolea huduma inalenga kuimarisha uwajibikaji kwa watoa huduma kutoa huduma bora.

***287. Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ubora wa utoaji huduma, Wizara imeendelea kufanya ukaguzi wa kimatibabu katika vituo vya kutolea huduma. Kwa kipindi hiki, Wizara imefanya ukaguzi wa kimatibabu kwa huduma za Uuguzi na Ukunga katika Hospitali 126 za Halmashauri. Matokeo ya ukaguzi huo yanaonesha kiwango cha ubora wa huduma za Uuguzi kimeongezeka kutoka asilimia 66 mwaka 2024 hadi asilimia 69 mwaka 2025 na huduma za Ukunga kutoka asilimia 75 mwaka 2024 kufikia asilimia 78 mwaka 2025. Ongezeko hili limechangiwa na kujengea uwezo Wauguzi na Wakunga 8,954 katika kutekeleza mipango kazi ya kushughulikia mapungufu yanayobainika pamoja na kuimarisha usimamizi wa huduma vituoni.

***288. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuboresha upatikanaji wa huduma za ushauri nasaha, upimaji wa VVU, kuanzisha dawa za kufubaza makali ya VVU kwa wakati katika ngazi zote za kutolea huduma na kutoa rufaa kwa wakati kwa kuwatumia Wauguzi na Wakunga. Kwa kipindi hiki idadi ya Wauguzi na

Wakunga waliopatiwa mafunzo ya kutoa huduma za VVU imeongezeka kutoka 3,769 mwaka 2024 hadi 5,056 Machi 2025, lengo ni kuendelea kusogeza huduma hizo kwa wagonjwa waliopo maeneo yenye upungufu wa matabibu. Aidha, programu hii imechangia kuongeza kasi ya upimaji wa VVU na uanzishwaji wa dawa pamoja na kuongezeka kwa huduma za kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto. Hadi kufikia Machi 2025 jumla ya vituo vipya 1,025 vya dawa za kupunguza makali ya VVU vinavyosimamiwa na Wauguzi vimeanzishwa katika maeneo yenye upungufu wa madaktari.

289. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kuboresha vyumba vya kujifungulia ili kuweza kutoa **huduma za mama mwambata (Birth Companionship)** ambapo mama anaruhusiwa kukaa na msindikizaji aliyemchagua wakati wa kujifungua. Jumla ya vituo vya kutolea huduma 2,202 vimejengewa uwezo ambapo kwa sasa vituo 847 vinatoa huduma ya mama mwambata ikilinganishwa na vituo 42 kwa mwaka 2024 kipindi kama hiki. Sambamba na hili Wizara imewajengea uwezo watoa huduma 5,958 ikilinganishwa na watoa huduma 1,285 katika kipindi kama hiki mwaka 2024 juu ya matumizi sahihi ya chati uchungu ili kuendana na mapendekezo ya Shirika la Afya Duniani ya kuimarisha ubora wa huduma wakati wa kujifungua. Aidha, jumla ya Wakunga 181 katika Halmashauri za Kahama Mji, Ushetu, Kishapu, Shinyanga Vijijini, Ilala Jiji,

Kinondoni na Temeke walijengewa uwezo kutoa huduma za dharura kwa mama wakati wa kujifungua (Midwifery Emergency Skills Training).

**290.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kusimamia ubora wa huduma kwa wagonjwa wa ndani katika **vitengo vya wagonjwa mahututi na dharura (ICU na EMD)**, Wizara ilitoa mafunzo kuhusu matibabu ya hewa tiba ya Oksijeni kwa Wauguzi na Wakunga 760 kutoka Hospitali 16 za Rufaa za Mikoa ili kuimarisha huduma za wagonjwa mahututi. Aidha, Wizara imewajengea uwezo Wauguzi viongozi wa Mikoa na Halmashauri zote pamoja na Wauguzi Wafawidhi wa Hospitali za Rufaa za Mikoa kufanya usimamizi shirikishi wa ndani kwa kutumia mfumo wa Usimamizi Shirikishi (AfyaSS) sambamba na miongozo ya kutoa huduma za Uuguzi. Jumla ya viongozi 302 waliweza kujengewa uwezo ili kuongeza ufanisi, tija na ubora wa huduma katika vituo wanavyosimamia sambamba na kuongeza usimamizi wa matumizi ya miongozo ya kutolea huduma za Uuguzi kama inavyoelekezwa na Shirika la Afya Duniani.

### Uhakiki Ubora wa Huduma za Afya

**291.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jukumu la kuhakikisha na kufuatilia utoaji wa huduma bora za afya katika ngazi zote nchini. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara iliendelea kuimarisha Timu za Uimarishaji Ubora (Quality Improvement Teams) kwa kuwajengea uwezo watoa huduma 510 kutoka Timu za Uendeshaji Huduma za Afya za Mikoa,

Halmashauri na vituo vya afya katika Halmashauri 35 za Mikoa ya Mtwara, Singida, Lindi, Manyara na Shinyanga. Kwa upande wa huduma kwa wateja, Wizara imeendelea kusimamia vituo vya kutolea huduma katika ngazi zote kwa kuhakikisha vituo vinaweka mazingira rafiki ya huduma kwa wateja. Mazingira hayo ni pamoja na kuboresha mifumo ya kupokea malalamiko, watoa huduma kuzingatia maadili ya kazi na kuhakikisha usalama wa huduma kwa mteja.

***292.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ubora wa huduma za kimatibabu, kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Wizara imefanya ukaguzi wa kimatibabu (Clinical Audit) katika hospitali za rufaa za mikoa 28, hususan kwenye huduma za mama na mtoto pamoja na huduma za dharura. Matokeo ya ukaguzi huo yalionesha kuwa miongozo ilifuatwa kwa asilimia 67 katika huduma za mama na mtoto na asilimia 64 katika huduma za dharura. Sambamba na hilo, Wizara ilitoa mafunzo ya ukaguzi kwa watoa huduma 288 ambapo 163 walipata mafunzo ya ana kwa ana na 125 kwa njia ya mtandao. Aidha, Wizara imeboresha nyenzo za ukaguzi na kuwajengea uwezo watoa huduma ili waendelee kufanya ukaguzi kwa ufanisi na kupanua wigo wa ukaguzi hadi vituo vya afya vya ngazi ya msingi ambako wananchi wengi hupatiwa huduma.

***293.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha huduma zinazotolewa kwenye vituo zinakidhi viwango vya Kitaifa na Kimataifa, Serikali inaendelea na mchakato wa kuanzisha taasisi maalum ya kutoa ithibati kwa vituo

vya kutolea huduma za afya nchini. Lengo kuu la kuanzisha taasisi hii ni kuhakikisha huduma zinazotolewa zinazingatia viwango vya kitaifa na kimataifa kwa kuweka viwango, kufanya tathmini huru, na kutoa ithibati kwa vituo vitakavyokidhi vigezo. Pia, uanzishwaji wa taasisi hii utapunguza gharama kubwa zinazolipwa kwa taasisi za nje na kusaidia vituo vitakavyopewa ithibati kutoa huduma bora, salama na zenye kuheshimu haki na utu.

***294. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza afua za kukinga na kudhibiti maambukizi (Infection Prevention and Control) pamoja na kuhakikisha usalama wa huduma kwa wateja. Katika muktadha huo, jumla ya watoa huduma 3,304 wamepatiwa mafunzo ambapo 1,852 walihudhuria mafunzo darasani na 1,452 walipata mafunzo kwa njia ya mtandao katika mikoa ya Mara, Dar es Salaam, Kigoma, Shinyanga, Singida, Simiyu, Mwanza, Geita, Kagera, Morogoro, Mbeya na Katavi. Mafunzo hayo yalilenga kuwajengea uwezo watoa huduma ili waweze kukinga na kudhibiti maambukizi katika vituo vya kutolea huduma za afya, kukabiliana na magonjwa ya kuambukiza na ya milipuko kama Marburg, Kipindupindu, Mpox, pamoja na maambukizi yanayotokana na huduma za afya (Healthcare Associated Infections).

***295. Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha ufuatiliaji wa maambukizi yanayohusiana na huduma za afya, Wizara imetoa mafunzo kwa watoa huduma 317

kutoka vituo 53 vilivyopo katika mikoa sita (Lindi, Dar es Salaam, Mtwara, Arusha, Manyara na Kilimanjaro). Viashiria vya ufuatiliaji vimeingizwa kwenye mfumo wa kidijitali wa DHIS2 ili kurahisisha ukusanyaji na ufuatiliaji wa taarifa hizo. Vilevile, Wizara inaendelea kuwajengea uwezo watoa huduma waliopo kwenye ngazi ya afya ya msingi ili waweze kuanza kutoa taarifa za magonjwa husika katika mifumo ya kutolea taarifa.

***296. Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha **usimamizi shirikishi** kwenye vituo vya kutolea huduma za afya nchini, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea na utekelezaji wa matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa *Afya Supportive Supervision System* (AfyaSS) ambapo mfumo huo umeweza kutumika katika ngazi zote za kutolea huduma za afya nchini. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi 2025, jumla ya simamizi shirikishi 14,186 kati ya 25,147 sawa na asilimia 56.4 zilifanyika kupitia mfumo huo. Aidha, hadi kufikia Machi, 2025 jumla ya watoa huduma 13,134 wamefundishwa na kusajiliwa katika mfumo huo. Mfumo huo umesaidia kuongeza ufanisi wa usimamizi shirikishi kwa kusaidia kutunza kumbukumbu, kuongeza uwajibikaji na kupunguza gharama za matumizi ya karatasi.

### Rasilimali Watu Katika Sekta ya Afya

***297. Mheshimiwa Spika,*** utoaji wa huduma bora kwa wananchi unategemea uwepo wa watoa huduma za

afya wenye ujuzi na weledi wa kazi. Lengo hilo litawezekana iwapo vyuo vya afya vitaendelea kuzalisha wataalam wenye ujuzi na weledi, kuwaendeleza wataalam waliopo pamoja na kuajiri watumishi wa kutosha katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini.

***298.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Serikali **imeajiri jumla ya watumishi 13,564** katika Sekta ya Afya na kufanya **jumla ya watumishi katika Sekta ya Afya kufikia 177,711**. Ongezeko hili la watumishi **limepunguza upungufu wa watumishi wa Sekta ya Afya kutoka asilimia 64 hadi kufikia asilimia 55 ya mahitaji** ya watumishi wote 391,950 wanaohitajika katika Sekta ya Afya. Kati ya watumishi waliopo, watumishi 136,739 sawa na asilimia 77 wapo katika ngazi ya afya ya msingi na watumishi 33,765 sawa na asilimia 19 wanafanya kazi katika ngazi ya Hospitali za Rufaa za Mikoa, hospitali za Rufaa za Kanda, Hospitali Maalum za Rufaa na Hospitali ya Taifa na asilimia 4 ya watumishi wapo katika Mashirika na Taasisi. Pamoja na juhudi hizi Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo katika Sekta ya Afya imeendelea kutoa ajira za mikataba ili kukabiliana na upungufu wa watumishi uliopo. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya wataalam 8,146 waliajiriwa kupitia utaratibu huu kwa ajili ya kufanya kazi kwenye vituo vya kutolea huduma.

***299.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo itaendelea kuweka mazingira

mazuri na yenye kuvutia kwa watumishi wa Sekta ya Afya ili kuwabakiza watumishi katika maeneo yao ya kazi. Wizara inaendelea kuwakumbusha waajiri mbalimbali kuweka mazingira mazuri yatakayowavutia na kuwabakiza watumishi wa Sekta ya Afya kama vile kujenga nyumba za makazi karibu na maeneo ya kutolea huduma, kununua vyombo vya usafiri kwa ajili ya kuwahudumia watumishi, kuendelea kutoa posho ya masaa ya ziada na posho za kuitwa kazini (Oncall Allowance), kutoa mikopo kwa watumishi wa afya na kuwaendeleza watumishi hao ili wabaki katika maeneo yao kwa lengo la kutoa huduma bora kwa wananchi.

**300.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha uwepo wa wataalam wa kutosha, kwa uwiano sahihi na wanaotoa huduma zilizo bora za afya kwa wananchi, Wizara imeendelea kusimamia vyuo vyote vya mafunzo vya kada zaa kati vinavyomilikiwa na Serikali, taasisi za dini na watu binafsi ili kuhakikisha vinazalisha wataalam wenye ujuzi na weledi. Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi ilifanya uchaguzi wa wanafunzi 33,353 sawa na asilimia 36 ya waombaji 92,820 waliotuma maombi ya kujiunga na vyuo vya afya ngazi ya kati. Kati yao wanafunzi 3,209 sawa na asilimia 10 walichaguliwa kujiunga na vyuo vya Serikali na wanafunzi 30,144 sawa na asilimia 90 walichaguliwa kujiunga na vyuo vinavyomilikiwa na watu binafsi na taasisi za dini katika programu za Sayansi Shirikishi za Afya, Uuguzi na Ukunga. Aidha, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla

ya watalaam 17,850 wamehitimu katika fani mbalimbali za kada za kati za Afya ikilinganishwa na wataalam 15,475 katika kipindi hicho kwa mwaka 2024. Wahitimu ngazi ya shahada kwa kipindi hicho ni 5,415 ikilinganishwa na wataalam 2,891 katika kipindi hicho kwa mwaka 2023. Vilevile, wahitimu wa ngazi ya Shahada ya Uzamili wameongezeka kutoka 540 mwaka 2023 hadi kufikia 889 mwaka 2024.

**301.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea na kuratibu uendeshaji wa mafunzo ya muda mfupi ya Wahudumu wa Afya ngazi ya Jamii ambapo katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya washiriki 3,631 wamepatiwa mafunzo hayo. Pamoja na mafunzo hayo, Wizara imeanzisha mitaala ya kada zenye uhaba mkubwa nchini ikiwa ni pamoja na Mtaala wa Stashahada ya Saikolojia Tiba (Clinical Psychology) ambao upo kwenye hatua za mwisho za ukamilishwaji. Mitaala hii imeanzishwa ili kuzalisha wataalam wa kutosha kukabiliana na changamoto za matibabu ya afya ya akili na utengemao kuanzia kwenye ngazi ya msingi. Vilevile, Wizara imehuisha mitaala ya Stashahada ya Optometria na Utunzaji Kumbukumbu na Taarifa za Afya (Health Record and Information Technology) baada ya iliyokuwepo kuisha muda wa matumizi.

**302.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia ufadhili wa masomo wa ***Samia Health Super-specialization Program*** umewezesha ufadhili wa masomo kwa **watalaam wapya wa Sekta ya Afya 544** na kufanya jumla ya wataalam wanaofadhiliwa kusomea fani za

ubingwa na ubingwa bobezi katika fani mbalimbali ndani na nje ya nchi kufikia 1,420. Kati ya wataalam wapya waliopata ufadhili, 517 wamepata ufadhili wa kusoma vyuo vikuu vya ndani na watalaam 27 wamepata ufadhili wa kusoma nje ya nchi. Vilevile, Watumishi 47 wamepata ufadhili wa mafunzo kwa mfumo wa seti unaowezesha huduma mpya za ubingwa na ubingwa bobezi kuanza kutolewa zikiwa na wataalam wote wanaohitajika kwa ajili ya utoaji wa huduma hizo. Aidha, kutokana na **kuongezeka kwa kiwango cha fedha ya ufadhili kutoka Shilingi Bilioni 10.95 mwaka 2023/2024 hadi kufikia Bilioni 14** mwaka 2024/2025, idadi ya wanufaika wa ufadhili imeendelea kuongezeka hadi kufikia wataalam 1,420 mwaka 2024/2025.

***303.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea na utekelezaji wa mpango wa kuwajengea uwezo wataalam wa Sekta ya Afya ili waweze kutoa huduma zinazokubalika kitaifa na kimataifa sambamba na kuimarisha matumizi ya Mfumo wa Kitaifa wa Mafunzo kwa Njia ya Mtandao kwa Sekta ya Afya (*National e-Learning Platform for Health).* Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, **jumla ya moduli 42 za mafunzo mbalimbali ya afya ziliongezwa kwenye mfumo na kufanya jumla ya moduli zilizopo katika mfumo kufikia 298.** Katika kipindi hicho watumishi wapya waliosajiliwa kwenye mfumo huo ni 9,751 na kufanya jumla ya watumishi wote kufikia 129,663. Wizara kwa kushirikiana na mabaraza ya kitaaluma itaendelea kusimamia utekelezaji wa mpango wa kuwaendeleza wataalam

wa Sekta ya Afya ili waendelee kuwa na weledi unaokubalika katika kutoa huduma za afya nchini.

***304.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Wizara imewajengea uwezo wakufunzi 92 wa vyuo vya afya vya kada za kati nchini kwa kuwapatia mafunzo ya mbinu za ufundishaji na upimaji wa wanafunzi *(Teaching Methodology and Students Assessment).* Pia, katika kuweka mfumo madhubuti wa kudhibiti ubora wa mafunzo, Wizara imehuisha miongozo mbalimbali ya mafunzo ikiwemo Mwongozo wa Mitihani ya Kitaifa ya Kada za Kati za Afya, Mwongozo wa Ulinzi na Usalama wa Mitihani ya Kitaifa ya Muhula wa Pili na Mwongozo wa Matumizi ya Hospitali za Mafunzo (Clinical Placement Guide).

***305.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imetoa mafunzo ya Viashiria vya Mahitaji ya Watumishi kwa kulingana na kazi yaani ***Workload Indicators of Staffing Needs (WISN)*** kwa wakufunzi 128 kutoka kwenye Mikoa yote nchini. Mafunzo hayo, yamezingatia maboresho ya kidigitali yaliyofanyika ili kurahisisha kukusanya na kuchakata taarifa za viashiria vya kazi zilizofanyika kwenye kituo kwa ajili ya kupima uzito wa kazi kwenye vituo na kutoa taarifa ya uhitaji wa watumishi kulingana na uzito wa kazi zilizopo. Mafunzo hayo yatawezesha kuendelea kupanga mipango ya mahitaji ya watumishi yenye uhalisia kwa kuzingatia uzito wa kazi na sio kuzingatia hadhi au ukubwa wa kituo bila kujali idadi ya wagonjwa, huduma

zinazotolewa na uzito wa kazi kwa watumishi waliopo kwenye kituo husika.

### Matumizi ya TEHAMA

***306. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imesimika Mfumo wa Afya eHMS katika Hospitali za Rufaa za Mikoa 28 na kuunganisha na mifumo mingine ikiwemo mfumo wa Taarifa za Utoaji wa Huduma za Afya (DHIS2), mfumo wa kukusanya mapato Serikalini (GePG), Bohari ya Dawa (MSD), Wakala ya Usajili wa Ufilisi na Udhamini (RITA) na mifumo ya Bima za afya, ikiwemo mfumo wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF). Aidha, Mfumo huo pia umeunganishwa na Mifumo ya kutolea huduma za afya katika Hospitali ya Taifa, Hospitali Maalum na Hospitali za Rufaa za Kanda (MNH, JKCI, MOI, BMH, BMC, ORCI) na mfumo wa kutolea huduma za afya ngazi ya msingi (GOTHOMIS).

***307. Mheshimiwa Spika,*** Mfumo jumuishi wa kukusanya na kuhifadhi taarifa za afua mbalimbali za afya ngazi ya jamii (Unified Community System - UCS) umeboreshwa. Hadi sasa mfumo huo umesimikwa katika jumla ya mikoa 26 ikiwemo Arusha (vituo vya afya 108), Dar es Salaam (vituo vya afya 52), Dodoma (vituo vya afya 105), Geita (vituo vya afya 90), Kagera (vituo vya afya 120), Kigoma (kituo cha afya 75), Kilimanjaro (vituo vya afya 62), Lindi (vituo vya afya 102), Manyara (vituo vya afya 52), Mbeya (vituo vya afya 172), Morogoro (vituo vya afya 79), Mwanza (vituo vya afya 178), Njombe (vituo vya afya

79), Pwani (vituo vya afya 129), Shinyanga (vituo vya afya 128), Singida (vituo vya afya 62), Tabora (vituo vya afya 174) na Tanga (vituo vya afya 130).

***308. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imekamilisha ufungaji wa huduma za Tiba Mtandao katika hospitali ya Rufaa Mkoa wa Songwe na kufanya hospitali zinazotumia Huduma ya Tiba Mtandao kuwa 25 (Hospitali za Rufaa ya ngazi ya Mkoa 18, Hospitali za Rufaa ngazi ya Kanda tatu (3), Hospitali Maalum tatu (-3), Hospitali ngazi ya Taifa moja (1). Matumizi ya mfumo huu yatasaidia katika kuimarisha utoaji wa huduma za afya nchini.

**Ufuatiliaji na Tathmini**

***309. Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na Tathmini, Wizara imeunda timu ya wataalam 126 wa Ufuatiliaji na Tathmini kutoka katika Idara, Vitengo, Programu, Mabazara na bodi, Taasisi na Hospitali zilizo chini ya Wizara. Utekelezaji huu umefanyika kwa kuzingatia agizo lililotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu juu ya kuimarisha utekelezaji wa majukumu ya ufuatiliaji na tathmini. Lengo la timu hiyo ni kuimarisha utendaji kazi wa Ufuatiliaji na Tathmini kwa Taasisi zilizo chini ya Wizara. Aidha, kwa kutambua umuhimu wa kuwa na *champions* ambao wamebobea katika eneo ya tathmini na ufuatiliaji, Wizara imeandaa mwongozo wa mafunzo ambao utatumika kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa

wataalam hao 126 kuwa na ujuzi wa kutosha katika kutekeleza majukumu yao haswa katika eneo la afya.

***310. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Wizara imekamilisha kuandaa machapisho manne (4) ya Takwimu na kuyasambaza katika Idara na Vitengo kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya takwimu ikiwemo jarida la Takwimu za hali ya utoaji wa huduma za Afya nchini kwa kipindi cha Januari hadi Juni 2024, *Annual Health Sector Performance Profile 2023, Health Statistical Table and Figure 2023 na National Health Facility Atlas 2023.* Taarifa hizi zinapatikana katika Tovuti ya Wizara na Tovuti ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS). Taarifa zinazopatikana katika majarida na machapisho hayo inawezesha Wizara, wadau na jamii kufahamu kuhusu mwenendo wa utoaji huduma za afya na kutumia taarifa hizo katika kutoa ushauri na kufanya maamuzi yenye ushahidi wa kisayansi katika kutatua changamoto za Sekta ya Afya.

***311. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa taarifa na takwimu za utoaji huduma za afya nchini ambapo katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, imeandaa na kusambaza nyenzo 314,413 za ukusanyaji taarifa (MTUHA tools) katika vituo vyote vya kutolea huduma nchini. Nyenzo hizo ni pamoja na Rejesta, Fomu za Muoanisho na Fomu za Taarifa za kila mwezi, ambazo zimeshajumuishwa katika mifumo ya kidijitali ya ukusanyaji taarifa. Zana hizo zitasaidia

kuimarisha upatikanaji wa takwimu katika vituo vya kutolea huduma za afya.

## Ugharamiaji wa Huduma za Afya

***312. Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Wizara ya Afya imeendelea kutekeleza Mikakati mbalimbali ili kuwezesha wananchi kupata huduma za afya kwa kuzingatia Sera ya Afya ya Mwaka 2007. Mikakati hiyo ni pamoja na kuwezesha upatikanaji wa rasimali fedha kwa ajili ya kugharamia huduma za afya nchini na kuimarisha mfumo wa Bima ya Afya kwa kutunga Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, Sura 161 yenye lengo la kuhakikisha wananchi wanapata huduma za afya bila kikwazo cha fedha pindi wanapohitaji huduma hiyo.

***313. Mheshimiwa Spika*****,** kufuatia tangazo la **Serikali Na. 700A la mwaka 2024** la kuanza utekelezaji wa **Sheria ya Bima ya Afya kwa wote** kwa awamu**,** Wizara kwa kushirikiana na wadau inaendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu dhana na umuhimu wa bima ya afya kabla ya kuanza kutekelezwa kwa takwa la ulazima wa bima ya afya kwa wote. Uelimishaji wa wananchi unahusisha viongozi wa ngazi zote ikiwemo ngazi za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa lengo la kuwa na uwajibikaji wa pamoja. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi zinazohusika na utekelezaji wa Sheria hii inaendelea kuimarisha mifumo itakayosaidia kuongeza ufanisi katika kuandikisha wanachama na uchakataji wa

madai. Taasisi hizo ni pamoja na Ofisi ya Rais TAMISEMI, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, mfuko wa kugharamia kaya maskini (TASAF), Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa Tanzania (NIDA) na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA).

***314.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2024/25 kiasi cha **Shilingi Trilioni 2.54** kilitengwa kwa ajili ya kugharamia vipaumbele mbalimbali katika Sekta ya Afya ikiwemo ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya kutolea huduma za afya katika ngazi zote, ununuzi wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi ikilinganishwa na kiasi cha Shilingi Trilioni 2.46 kilichotengwa mwaka 2023/24. Aidha, Serikali imeendelea kuwezesha upatikanaji wa bidhaa za afya katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini ambapo hadi kufikia Machi 2025, kiasi cha Shilingi Bilioni 243.5 kimetolewa kwa ajili ya ununuzi, ugomboaji, utunzaji na usambazaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi.

***315.*** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika kukabiliana na athari zitokanazo na mabadiliko ya Sera za Kimataifa katika ufadhili wa Sekta ya Afya, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu imefanya tathmini ya namna ya kukabiliana na changamoto ya athari hizo kwa kutenga kiasi cha Shilingi Bilioni 202 kwa ajili ya kutumika katika kipindi cha mwezi Machi hadi Juni, 2025. Kati ya fedha hizo, kiasi cha Shilingi Bilioni 93

tayari zimetolewa kwa ajili ya ununuzi wa dawa za ARVs, bidhaa za Kifua Kikuu na Malaria. Aidha, Serikali imeongeza bajeti ya dawa kwa Wizara hadi kufikia Shilingi Bilioni 300 kwa mwaka 2025/26 kutoka Shilingi Bilioni 200 za mwaka 2024/25. Ongezeko hili litawezesha ununuzi wa dawa za ARVs pamoja na dawa nyingine muhimu.

***'Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa, Serikali imejipanga katika kuhakikisha dawa hizo muhimu zinapatikana kwa walengwa katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya kama kawaida'***.

**Miradi ya Maendeleo**

***316. Mheshimiwa Spika*****,** katika kuboresha huduma za afya nchini, Wizara imeendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo hususan ujenzi wa miundombinu ya kutolea huduma za Afya katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, Hospitali za Rufaa za Kanda, Hospitali Maalumu na Hospitali ya Taifa pamoja na vyuo vya Afya na utekelezaji wa miradi hiyo upo katika hatua mbalimbali.

***317. Mheshimiwa Spika,*** Miradi 11 imefikia zaidi ya asilimia 80 ya utekelezaji ikiwemo; ujenzi wa jengo la huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu; ujenzi wa awamu ya pili wa jengo la wodi za wagonjwa, jengo la huduma za Radiolojia katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda-Chato; jengo la kutolea huduma za wagonjwa

wa nje awamu ya kwanza na jengo la Damu Salama katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kigoma-Maweni; jengo la wagonjwa wa nje katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Lindi na Mtwara, ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mara awamu ya nne; ujenzi wa miundombinu ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi, ujenzi wa jengo la huduma za afya ya uzazi katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kilimanjaro-Mawenzi, ujenzi wa jengo la Radiologia katika Hospitali ya Magonjwa ambukizi ya Kibong'oto na ujenzi wa jengo la kutolea huduma za wagonjwa wa nje awamu ya pili katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma - Songea**.**

***318. Mheshimiwa Spika,*** Miradi mitatu (3) inayoendelea na utekelezaji imefikia wastani wa asilimia 60 ambayo ni ujenzi wa jengo la huduma za afya ya mama na mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tabora-Kitete, ujenzi wa jengo la huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe na ujenzi wa jengo la damu salama katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Rukwa.

***319. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza miradi mitano (5) ambayo utekelezaji wake umefikia wastani wa asilimia 40, ikiwemo ujenzi wa jengo la magonjwa hatarishi ya kuambukiza katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida; ujenzi wa jengo la afya ya mama na mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita, ujenzi wa kituo cha umahiri kwa ajili ya matibabu ya magonjwa hatarishi na milipuko

Kisopwa, ujenzi wa jengo la tiba mionzi katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Benjamin Mkapa na ujenzi wa majengo ya Hospitali ya Kanda Chato.

**320. *Mheshimiwa Spika,*** miradi (52) utekelezaji wake upo katika hatua za awali kwa wastani wa asilimia 20; Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa Hospitali ya mama na Mtoto Nala-Dodoma, Ujenzi wa Hospitali ya Kanda ya Magharibi-Kigoma, Ujenzi wa jengo la utawala katika ya Hospitali ya magonjwa ambukizi Kibong'oto, Uhuishaji wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje katika Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI), ujenzi wa kituo cha mionzi kwa ajili ya matibabu ya Saratani – Mbeya, ujenzi wa jengo la huduma ya afya ya mama na mtoto katika Hospitali za Rufaa za Mikoa ya Shinyanga, Tanga, Kagera na Morogoro ni ***kama inavyoonekena katika Kiambatisho Namba 2.***

## Utekelezaji wa Majukumu ya Taasisi zilizo Chini ya Wizara

### Bohari ya Dawa (MSD)

**321. *Mheshimiwa Spika,*** Bohari ya Dawa (MSD) ni Taasisi iliyoanzishwa mwaka 1993 kwa mujibu wa Sheria ya Bohari ya Dawa Na.13 iliyofanyiwa marekebisho mbalimbali na ina majukumu ya msingi manne (4); Uzalishaji, Ununuzi, Utunzaji na Usambazaji wa bidhaa za afya kwenda kwenye vituo vya umma vya kutolea huduma za afya na vile vilivyoidhinishwa na Wizara. Hadi kufikia mwezi

Machi 2025, idadi ya vituo vya kutolea huduma za afya vinavyohudumiwa na Bohari ya Dawa vimeongezeka na kufikia 8,619 kutoka vituo 8,276 vilivyorekodiwa Juni 30, 2024 sawa na ongezeko la vituo 343. Ongezeko hili limetokea kwenye mikoa yote inayohudumiwa na Bohari ya Dawa kupitia kanda 10 zilizopo katika mikoa ya Dodoma, Dar es Salaam, Mtwara, Mwanza, Tabora, Kilimanjaro, Tanga, Kagera, Mbeya na Iringa.

**322.** ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya upatikanaji wa bidhaa za afya imeendelea kuimarika kwa kuzingatia upatikanaji wa bidhaa za afya ashiria 382 na bidhaa za Mradi Misonge 73. Hivyo, kwa mwaka wa fedha 2024/25, upimaji wa hali ya upatikanaji wa bidhaa za afya ashiria umeendelea kuzingatia bidhaa za afya 382. Lengo likiwa ni kuimarisha upatikanaji wa bidhaa za afya ambazo ni muhimu zaidi kwenye utoaji wa huduma za afya katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini.

**323.** ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya upatikanaji wa bidhaa za afya kwenye maghala ya Bohari ya Dawa pekee umeendelea kuwa wa kuridhisha. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 upatikanaji wa bidhaa za afya ashiria 382 kwenye maghala ya Bohari ya Dawa umefikia asilimia 68 kwa kiwango kinachokidhi mahitaji ya mwezi mmoja ikilinganishwa na asilimia 61 kipindi kama hicho mwaka 2024. Aidha, upatikanaji wa bidhaa za dawa pekee umeendelea kuwa asilimia 68 kwa mwezi Machi 2025 kwa

kiwango kinachokidhi mwezi mmoja. Upatikanaji huu wa bidhaa za afya umeendelea kuimarika mwaka hadi mwaka licha ya kuwepo kwa changamoto ya uwezo mdogo wa uzalishaji wa bidhaa za afya nchini na migogoro mbalimbali inayoathiri mnyororo wa ugavi duniani na hivyo kuhitajika kwa muda mrefu kati ya uagizaji na mapokezi ya bidhaa za afya.

***324. Mheshimiwa Spika,*** hali ya upatikanaji wa bidhaa za afya za Miradi Misonge – "Vertical Programs" umeendelea kuimarika ambapo hadi kufikia Machi 2025, upatikanaji wa bidhaa hizi umefikia asilimia 92.5 kutoka asilimia 82 iliyofikiwa mwezi Machi 2024 . Bidhaa hizi za Miradi Misonge zinahusu magonjwa ya UKIMWI, Malaria, Kifua Kikuu, Ukoma na Afua nyinginezo ambazo zimekuwa zikipatikana kupitia Serikali na Wadau mbalimbali. Sambamba na hili, Utimizaji wa mahitaji ya vituo vya kutolea huduma za afya umeendelea kuwa wastani wa asilimia 79 hadi kufikia mwezi Machi 2025, sawa na kiwango kilichoripotiwa mwezi Julai 2024. Utimizaji huu unahusu mahitaji yaliyoombwa kupitia Bohari ya Dawa pekee.

***'Nichukue fursa hii kulihakikishia Bunge lako tukufu kuwa dawa za miradi misonge zitaendelea kupatikana kama kawaida katika vituo vya kutolea huduma za afya'.***

***325. Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hilo, Bohari ya Dawa imeendelea kufanya ununuzi na usambazaji wa vifaa tiba vinavyohitajika katika vituo vya kutolea

huduma za afya kuanzia ngazi ya msingi hadi vituo vinavyotoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi nchini. Vifaa hivyo ni pamoja na mashine za kuchuja damu (dialysis), vifaa tiba vya utoaji wa huduma ya kinywa na meno kama vile viti vya meno vya kisasa pamoja na mashine maalum za mionzi kwa utoaji wa huduma za kinywa na meno 'dental x-ray', mashine za usingizi, 'Ultrasound' na 'Digital X-Ray'. Uwepo wa mitambo hii umeimarisha utambuzi wa magonjwa kwa usahihi na kutolewa kwa tiba sahihi. Vilevile, Bohari ya Dawa imeendelea kusambaza bidhaa za afya kwa lengo la kuokoa maisha ya mama na mtoto, majenereta kwa ajili ya kuhakikisha huduma hazikwami pale ambapo kunatokea changamoto za umeme, mashine za kufulia na majokofu ya kuhifadhia miili.

***326. Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Bohari ya Dawa inatekeleza mpango maalum wa kuongeza upatikanaji wa huduma za uchujaji damu ikiwa ni sehemu ya matibabu ya figo, hivyo kupunguza gharama za huduma hiyo. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi 2025 idadi ya mashine imeongezeka na kufikia mashine 137 kutoka mashine 60 na hivyo kuongeza hospitali zilizopokea mashine hizi kupitia Bohari ya Dawa kutoka hospitali 7 na kufikia hospitali 15. Uwekezaji huu umegharimu kiasi cha Shilingi Bilioni 7.7. Katika hospitali hizi, hospitali 11 zimeanza kutoa huduma na hospitali 4 zipo katika hatua za mwisho za matengenezo. Baadhi ya hospitali zinazotoa huduma hizi ni pamoja na Hospitali za Rufaa za Mikoa za Amana,

Mwananyamala, Temeke, Morogoro, Katavi, Tumbi, Chato, Sekou Toure pamoja na hospitali ya Chuo Kikuu cha Dodoma. Aidha, Mkakati huu wa usambazaji wa mashine za uchujaji wa damu unalenga kupunguza gharama na adha zilizopo kwa sasa.

***327. Mheshimiwa Spika,*** Bohari ya Dawa imesambaza jumla ya *kits* 144 ya bidhaa za *hemodialysis* kwa ajili ya vipindi 100 kila kimoja kwa hospitali zinazotoa huduma za uchujaji wa damu. Usambazaji huu utawezesha utoaji wa huduma kwa vipindi 14,400. Katika kuhakikisha huduma hizi hazikwami, Bohari ya Dawa imeagiza na inatarajia kupokea shehena nyingine ya *kits* 504 ifikapo mwezi Juni 2025, ili kuhakikisha upatikanaji endelevu wa huduma za uchujaji damu.

***328. Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Bohari ya Dawa imeendelea kuhakikisha bidhaa za afya ya kinywa na meno zinapatikana katika vituo vya kutolea huduma za afya. Thamani ya bidhaa hizo zilizosambazwa imeendelea kuongezeka kutoka Shilingi milioni 598.19 kwa mwaka 2022/23 na kuweza kufikia Shilingi Bilioni 9.46 mwaka 2024/25. Hali ya upatikanaji wa bidhaa za meno ashiria imeendelea kuimarika ambapo hadi kufikia Machi 2025 imefikia 88% ikilinganishwa na 75% katika kipindi kama hichi kwa mwaka 2024 na hivyo kuwezesha vituo vya kutolea huduma za afya kuweza kutoa huduma hizi kwa ubora na ufanisi zaidi.

**329.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha bidhaa za afya zinapatikana wakati wote kwenye vituo vya kutolea huduma za afya, Serikali kupitia Bohari ya Dawa imeendelea kufanikisha usambazaji wa bidhaa za afya nchi nzima kwa mizunguko sita kutoka mizunguko minne. Aidha, katika kipindi cha mwezi Julai 2024 hadi mwezi Machi 2025, Bohari ya Dawa ilifanikiwa kusambaza bidhaa za afya kwa kuzingatia muda uliopangwa kwa wastani wa asilimia 98 ikiwa ni ongezeko la asilimia 6 kutoka asilimia 92 katika kipindi kama hiki mwaka 2023/2024.

**330.** ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na jukumu la ununuzi wa bidhaa za afya, sambamba na fedha ya Serikali inayopelekwa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ambapo mwaka huu wa fedha kiasi cha Shilingi Bilioni 200 kilitengwa na mpaka sasa MSD imeshapokea kiasi cha Shilingi Bilioni 183.2 sawa na asilimia 91.6. Hata hivyo, Bohari ya Dawa hukusanya fedha (*cash collection)* kutoka vituo vya kutolea huduma za afya ambazo hupatikana kupitia vyanzo vingine vya vituo hivyo. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 kiasi cha Shilingi Bilioni 126.64 zilikusanywa sawa na asilimia 64 ya lengo la kukusanya Shilingi Bilioni 198.40. Aidha, kiasi hiki kimeongezeka kwa asilimia 110 ikilinganishwa na kiasi cha Shilingi Bilioni 60.3 kilichokusanywa kipindi kama hiki kwa mwaka wa fedha uliopita.

**331.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na maboresho yanayoendelea kufanywa na Serikali, mapato ya

Bohari ya Dawa yameendelea kuongezeka. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Bohari ya Dawa imepata mapato ya Shilingi Bilioni 438.14 sawa na asilimia 108 ya lengo la kusambaza bidhaa za afya zenye thamani ya Shilingi Bilioni 389.94. Mapato haya ni ongezeko la Shilingi Bilioni 90.68 kutoka Shilingi Bilioni 347.46 sawa na asilimia 26 ikilinganishwa na kipindi kama hiki mwaka 2023/2024. Ongezeko hili limesababishwa na maboresho ya kiutendaji na usimamizi wa mnyororo wa ugavi, ununuzi na usambazaji wa bidhaa za afya kupitia bajeti ya vituo vya kutolea huduma inayotengwa kupitia Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais-TAMISEMI, kuimarika kwa makusanyo kwenye vituo vya kutolea huduma za afya na utunzaji na usambazaji wa bidhaa za afya za Miradi Msonge. Aidha, mapato mengine yaliyokusanywa kwa kipindi hiki cha mwezi Julai 2024 hadi Machi 2025 ni kiasi cha Shilingi Bilioni 16.37 sawa na asilimia 108 ya lengo la Shilingi Bilioni 15.07 kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

***332.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha upatikanaji wa bidhaa za afya, Bohari ya Dawa inaendelea na mkakati wake wa kuhakikisha uwepo wa Mikataba ya Muda Mrefu - *Framework Agreements,* kutoa kipaumbele kwa wazalishaji wa ndani, kuanzisha na kutekeleza mkakati wa kununua moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji au wazabuni walioidhinishwa na wazalishaji husika, na kusimamia utendaji wa wazabuni kwa kuzingatia mikataba iliyopo.

**333. *Mheshimiwa Spika,*** ufanisi unaopatikana Bohari ya Dawa ni matokeo ya Serikali kuwekeza kwenye maboresho na kuhakikisha Taasisi hii nyeti inatekeleza majukumu yake kikamilifu ikiwemo kuipatia MSD kiasi cha Shilingi Bilioni 100. Aidha, katika kuhakikisha utendaji wa Bohari ya Dawa unaimarika, kuanzia mwaka wa fedha 2025/26, Serikali imeamua kutenga fedha kwa ajili ya kulipia gharama za bidhaa za Miradi Msonge ambazo zinahusu utunzaji na usambazaji wa bidhaa za afya kwa ajili ya magonjwa ya UKIMWI, Malaria, Kifua Kikuu, Ukoma na bidhaa za mama na mtoto.

**334. *Mheshimiwa Spika,*** kutokana na ongezeko la watu, na uwekezaji mkubwa wa Serikali katika Sekta ya Afya umesababisha ongezeko la mahitaji ya maghala ya kuhifadhia bidhaa za afya ili kuimarisha mnyororo wa ugavi. Serikali imejenga maghala ya kisasa yenye viwango vya kimataifa katika Mikoa ya Dodoma na Mtwara ambapo yameshakamilika na yataanza rasmi kutumika mwezi Juni,2025.

**335. *Mheshimiwa Spika,*** Maghala haya mapya yatapunguza gharama za usambazaji ambapo ghala lililopo Dodoma litakuwa linapokea bidhaa zake kupitia reli ya kisasa kituo cha Dodoma kutoka Bandari ya Dar es Salaam na kuwezesha bidhaa hizo kusambazwa moja kwa moja kwenda kwenye Kanda nyingine nchini. Aidha, Bohari ya Dawa inaendelea kutekeleza ujenzi wa maghala kwa awamu ambapo awamu ya pili itahusu ujenzi wa ghala la Mwanza na Chato, Mkoa wa Geita, ambapo Serikali imeweza

kutoa kiasi cha Shilingi Bilioni 24.6 na hatua za kuwezesha kuanzishwa kwa ujenzi wa ghala la Dar es Salaam zinaendelea. Awamu ya tatu itatekelezwa katika Mikoa ya Arusha na Ruvuma.

***336. Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kuongeza upatikanaji wa bidhaa za afya nchini, Bohari ya Dawa imeanzisha Kampuni Tanzu inayoitwa "MSD Medipharm Manufacturing Company Limited" ambayo ina jukumu kubwa la kufanya uzalishaji wa bidhaa za afya. Kampuni hii, ina uwezo wa kufanya uwekezaji kwa kushirikiana na Sekta binafsi kwa mfumo wa uwekezaji wa pamoja yaani *Joint Venture Investment* na kuiwezesha Serikali kunufaika na faida inayopatikana moja kwa moja.

***337. Mheshimiwa Spika,*** Kampuni hii kwa sasa inamiliki Kiwanda cha Barakoa cha MSD Medipharm ambacho kina takribani miaka minne (4) toka kuanzishwa kwake na kinazalisha barakoa za kawaida (Surgical mask) na barakoa maalum (N95) kwa ajili ya kujikinga na maambukizo ya njia ya hewa katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini pamoja na Kiwanda cha Glovu kilichopo Makambako Mkoa wa Njombe.

***338. Mheshimiwa Spika***, kuanzia Julai 2024 hadi Mwezi Machi 2025, kiwanda kimeweza kuzalisha jumla ya Barakoa 1,119,778 sawa na asilimia 124 ya lengo, na kufanya mauzo ya jumla ya Shilingi 588,930,035.00 sawa na asilimia 130.9 ya malengo ya kiwanda, na ikilinganishwa na barakoa 732,800

zilizozalishwa kipindi kama hiki kwa mwaka wa fedha 2023/24 na kufanya mauzo ya Shilingi 366,400,000.00. Vilevile, hadi kufikia mwezi Machi 2025, Kiwanda cha Glavu(Gloves) Idofi kimeweza kuzalisha na kuuza jumla ya glavu milioni 5.6 zenye thamani ya Shilingi Bilioni 1.9 sawa na asilimia 50 ya matarajio ya uzalishaji kwa mwaka wa kwanza wa kiwanda.

***339. Mheshimiwa Spika***, Kampuni hii inatekeleza mradi mkubwa wa viwanda vya dawa na vifaa tiba katika eneo la viwanda la MSD, Zegereni Mkoa wa Pwani, mradi unaotekelezwa kwa kushirikiana na wabia wenza kutoka sehemu mbalimbali duniani. Aidha, MSD kupitia Kampuni hii inaendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa kiwanda cha kuchakata na kuzalisha bidhaa za afya zitokanazo na malighafi ya pamba ambao unalenga kutumia pamba inayolimwa nchini na kuchangia sio tu kupunguza uagizaji wa bidhaa hizi kutoka nje ya nchi bali pia kutoa soko la uhakika kwa wakulima wa zao la pamba nchini na ajira kwa vijana.

***340. Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Bohari ya Dawa imeendelea kuongeza ununuzi wa bidhaa za afya kutoka kwa wazalishaji wa ndani ambapo katika kipindi cha mwezi Julai 2024 hadi Machi 2025, bidhaa za afya zenye thamani ya Shilingi Bilioni 56.7 zimenunuliwa kutoka kwa wazalishaji wa ndani ikilinganishwa na Shilingi Bilioni 16.93 zilizonunuliwa katika kipindi kama hichi kwa mwaka wa fedha 2023/24 ikiwa ni ongezeko la Shilingi Bilioni 39.77.

Aidha, MSD imeendelea kununua maji tiba kwa asilimia 100 kutoka kwa wazalishaji wa ndani. Dhamira hii itasaidia kuongeza uzalishaji na kuvutia wawekezaji ambapo matumizi ya fedha za kigeni yatapungua na ajira zitatengenezwa nchini.

***341.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 Serikali imewezesha Bohari ya Dawa kuanza usimikaji wa mfumo wa TEHAMA ambao utakuwa na thamani ya Shilingi Bilioni 4. Mfumo huu unatarajiwa kuongeza ufanisi katika mnyororo wa ugavi, kuboresha matumizi ya takwimu na upashanaji taarifa. Katika jitihada za kuhakikisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA yanaimarishwa, hadi sasa, matumizi ya TEHAMA kwa Bohari ya Dawa yamefikia kiwango cha asilimia 95 ambapo sehemu kubwa ya michakato inafanyika katika mfumo wa Epicor 10 – ERP na kupelekea MSD kutambulika na Mamlaka ya Serikali Mtandao kwa kiwango cha *Level 4* katika matumizi ya Tehama*.*

***342.*** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi 2025 miongoni mwa mifumo iliyotengenezwa ili kuimarisha utendaji ni mfumo wa usimamizi na ufuatiliaji wa magari (Real time Fleet Management System), mfumo wa ununuzi wa bidhaa za afya kwa nchi za SADC kwa njia ya kielektroniki (Electronic SADC Pool Procurement - eSPPS), Mfumo wa *“Proof of Delivery”* unaotumika kusainisha vituo baada ya kufikishwa mzigo vituoni na kupokelewa na mfumo wa kuhudumia wateja, (Customer Portal) ambao hutumika na vituo vya kutolea huduma za afya

kutambua bidhaa za afya zilizopo MSD, gharama yake na hatua zilizofikiwa katika uchakataji wa maombi ya wateja yalipofikia.

**Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)**

343. ***Mheshimiwa Spika,*** Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ni Taasisi ya Umma iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria Sura ya 395 kwa lengo la kusimamia upatikanaji wa huduma za matibabu kwa watumishi wa Umma na wategemezi wao kupitia bima ya afya. Sheria ya Mfuko imekuwa ikifanyiwa marekebisho mara kwa mara ili kuwezesha kupanua wigo wa walengwa kwa kuingiza makundi mbalimbali. Kufuatia marekebisho ya Sheria ya Bima ya Afya, Mfuko unajumuisha watumishi katika Sekta ya Umma, wafanyakazi kutoka katika Sekta Binafsi na makundi mbalimbali ya jamii katika Sekta isiyo rasmi. Majukumu ya Kisheria ya Mfuko ni pamoja na kuandikisha wanachama, kukusanya michango na kuitunza, kusajili watoa huduma na kufanya malipo kwa watoa huduma za afya. Majukumu mengine ni kuwekeza fedha za ziada katika vitega uchumi mbalimbali ili kujiongezea uwezo wa kifedha unaowezesha kutoa huduma, kufanya kaguzi kwa waajiri na watoa huduma ili kuhakikisha wanazingatia miongozo iliyopo, kufanya tathmini ya uhai wa Mfuko na kutoa elimu kwa Umma.

344. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Mfuko umesajili wanachama wapya 462,408 sawa na asilimia 78 ya lengo la kusajili wanachama wapya 593,654. Kulinganisha na

wanachama 337,834 waliosajiliwa kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Idadi ya wanachama waliosajiliwa imewezesha Mfuko kuwa na wanachama wachangiaji 1,255,813 wenye jumla ya wanufaika 5,161,281 sawa na **asilimia 8.1** ya Watanzania wote. Mfuko unaendelea kubuni na kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuongeza wanachama ikiwemo kutoa elimu mijini na vijijini ili kuhakikisha wanachama wengi wanajiunga na kunufaika na huduma za bima ya afya.

***345.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi husika, Mfuko umekusanya mapato jumla ya Shilingi Bilioni 619.8. Kati ya fedha hizo, kiasi cha Shilingi Bilioni 579.9 ni kutoka katika michango ya wanachama, Kiasi cha Shilingi Bilioni 36.3 ni mapato yatokanayo na uwekezaji na kiasi cha Shilingi Bilioni 3.5 ni kutoka katika vyanzo vingine vya mapato. Mapato yaliyokusanywa ni ongezeko la asilimia 10 ikilinganishwa na kiasi cha Shilingi Bilioni 560.8 kilichokusanywa kipindi kama hicho mwaka 2023/24 kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 7**.

***Jedwali Na. 7. Mwenendo wa Ukusanyaji wa Mapato ya Mfuko kati ya mwaka 2023/24 na mwaka 2024/25.***

| Mapato | MIEZI TISA (JULAI - MACHI) UTEKELEZAJI 2023/24 | | | MIEZI TISA (JULAI - MACHI) UTEKELEZAJI 2024/25 | | | ONGEZEKO/ PUNGUFU (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Malengo (in '000) TZS) | Halisi (in '000) TZS) | Asilimia ya lengo | Malengo (in '000) TZS) | Halisi (in '000) TZS) | Asilimia ya lengo | |
| *Michango* | 534,963,054 | 521,980,614 | 98% | 603,032,075 | 579,999,093 | 96% | 10% |
| *Uwekezaji* | 50,238,195 | 34,257,837 | 68% | 42,680,244 | 36,316,438 | 85% | 6% |

| Mapato | MIEZI TISA (JULAI - MACHI) UTEKELEZAJI 2023/24 | | | MIEZI TISA (JULAI - MACHI) UTEKELEZAJI 2024/25 | | | ONGEZEKO/ PUNGUFU (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Malengo (in '000) TZS) | Halisi (in '000) TZS) | Asilimia ya lengo | Malengo (in '000) TZS) | Halisi (in '000) TZS) | Asilimia ya lengo | |
| *Mengineyo* | 1,125,000 | 4,617,053 | 410% | 5,352,224 | 3,493,138 | 65% | -32% |
| *Ufadhili* | 7,687,500 | - | - | 16,447,376 | - | - | - |
| ***Jumla*** | **594,013,749** | **560,855,504** | **94%** | **667,511,919** | **619,808,669** | **93%** | **10%** |

**346.** ***Mheshimiwa Spika,*** michango kutoka kwa wanachama imeendelea kuwa chanzo kikuu cha mapato ambapo kwa kipindi cha kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025 ilikuwa ni asilimia 93 ya mapato yote yaliyokusanywa ikiwa ni asilimia 92 ya lengo la kukusanya kiasi cha Shilingi Bilioni 603. Kiasi hicho ni ongezeko la asilimia 6 ikilinganishwa na kiasi cha Shilingi Bilioni 521 kilichokusanywa kwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2023/24.

**347.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mfuko umetumia jumla ya **Shilingi Bilioni 506**, ambapo kiasi cha Shilingi Bilioni 438.1 ni kwa ajili ya ulipaji wa madai kwa watoa huduma, kiasi cha Shilingi Bilioni 66.4 ni matumizi ya kiutawala ikijumuisha malipo ya mishahara na kiasi cha Shilingi Bilioni 1.7 ni matumizi mengineyo ikijumuisha miradi ya maendeleo. Matumizi ya malipo ya madai kwa watoa huduma yamepungua kwa asilimia 34 kwa mwaka 2024/25 ikilinganishwa na kiasi cha Shilingi Billioni 587.7 kilicholipwa kwa watoa huduma kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Vilevile, matumizi ya uendeshaji wa Mfuko yameongezeka kutoka asilimia 74 ya matumizi mwaka 2023/24 hadi

kufikia asilimia 83 ya matumizi mwaka 2024/25 kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 8**.

***Jedwali Na. 8. Mwenendo wa Matumizi ya Fedha ya Mfuko kwa kipindi cha mwaka 2023/24 na mwaka 2024/25.***

| MATUMIZI | MIEZI TISA (JULAI - MACHI) UTEKELEZAJI 2023/24 | | | MIEZI TISA (JULAI - MACHI) UTEKELEZAJI 2024/25 | | | ONGEZEKO/ PUNGUFU (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Malengo (in '000) TZS) | Halisi (in '000) TZS) | % | Malengo (in '000) TZS) | Halisi (in '000) TZS) | % | |
| Malipo ya Madai | 444,417,275 | 587,737,296 | 132% | 432,000,000 | 438,083,6858* | 101% | **-34%** |
| Matumizi ya kiutawala | 70,493,489 | 52,408,512 | 74% | 79,645,115 | 66,383,405 | 83% | **21%** |
| Miradi ya maendeleo | 1,989,560 | 690,513 | 35% | 143,176,867 | 1,744,079 | 1% | **60%** |
| **Jumla** | **516,900,324** | **640,836,321** | **124%** | **654,821,982** | **506,211,169** | **77%** | **-27%** |

***348. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, **jumla ya madai 55,817** yamechakatwa na jumla ya kiasi cha Shilingi Bilioni 438 sawa na asilimia 101 ya lengo kimelipwa. Aidha, kiasi kilicholipwa ni asilimia 91 ya madai yote yaliyowasilishwa na hivyo kufanya madai yaliyokataliwa kuwa ni asilimia 9 ikilinganishwa na asilimia 22 ya madai yaliyokataliwa katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Madai hayo yalichakatwa kwa wastani wa siku 58 ikilinganishwa na siku 66 kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Vilevile, asilimia 40.8 ya madai yalilipwa kwa vituo vya kutolea huduma vya Serikali na asilimia 59.2

yalilipwa kwa vituo vya kutolea huduma vya binafsi. Takwimu zinaonesha kuwa, fedha za NHIF kwa sasa zinachangia wastani wa asilimia 80 ya mapato ya vituo vya kutolea huduma za afya nchini.

**349.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mfuko umeendelea kuongeza wigo wa **usajili wa vituo** vya kutolea huduma za afya ambapo kwa kipindi cha kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025 Mfuko umesajili jumla ya vituo vya kutolea huduma 397 ambapo vituo 97 ni usajili wa mara ya kwanza, vituo 279 vilihuisha usajili na vituo 9 vilibadilishiwa hadhi, vituo 12 viliongeza huduma na kubadilisha umiliki. Aidha, usajili huu umefanya jumla ya vituo vilivyosajiliwa na Mfuko kufikia 10,004 ikiwa asilimia 72 ni vituo vya Serikali, asilimia 20 ni vituo binafsi na asilimia 8 ni vituo vya madhehebu ya kidini.

**350.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha huduma za matibabu nchini, Mfuko unatoa mikopo nafuu ya vifaa tiba, dawa na ukarabati wa vituo. Tangu kuanzishwa kwa mpango huo, jumla ya vituo 431 vilivyokidhi vigezo vimenufaika na mikopo yenye thamani ya Shilingi Bilioni 50.3. Kwa kipindi cha kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, vituo 5 vimepatiwa mikopo yenye thamani ya Shilingi Millioni 449.2 ikiwa ni pungufu ya asilimia 89 ikilinganishwa na kiasi cha Shilingi Bilioni 2.6 kilichotolewa mwaka 2023/24 kipindi kama hicho. Aidha, kati ya mikopo iliyotolewa kwa kipindi cha kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, Shilingi Billioni 428.2 sawa na asilimia 95 zilitolewa kwa vituo vinavyomilikiwa na Serikali na kiasi cha

Shilingi Millioni 21. sawa na asilimia 5 Kituo cha mtu binafsi. Utaratibu huo umesaidia kujenga uwezo wa vituo katika kutoa huduma za afya kwa wanachama na wananchi kwa ujumla.

351. ***Mheshimiwa Spika,*** Mfuko umeendelea **kupambana na kudhibiti udanganyifu** kutoka kwa watoa huduma, waajiri binafsi, wanufaika wa huduma na watumishi kwa kutekeleza mikakati mbalimbali. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, Mfuko ulibaini kiasi cha Shilingi Bilioni 5.7 kinachotakiwa kurejeshwa kilitokana na madai yenye udanganyifu kutoka kwa watoa huduma. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kusitisha matumizi ya kadi za wanachama 983 wasiostahili na wanachama wanaotumia kadi zao kufanya udanganyifu na vituo vinne (4) vimesitishiwa mikataba ya huduma.

352. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza takwa la kisheria la kufanya **tathmini ya uhai na uendelevu wa Mfuko**, kila baada ya miaka mitatu, mfuko unatekeleza takwa hilo kwa kufanya tathmini ya uhai na uendelevu wake (actuarial valuation). Kwa kipindi cha kuishia Juni 2021. Matokeo na mapendekezo ya taarifa ya tathmini hiyo yametumika katika kufanya mapitio ya vifurushi vinavyotumiwa na wanachama binafsi pamoja na familia zao. Mnamo tarehe 17 Desemba 2024, Mfuko ulizindua vifurushi vipya viwili ambavyo ni Serengeti, Ngorongoro na kurejesha kifurushi cha Toto Afya Kadi (TAK). Kifurushi cha **Serengeti Afya** kina wigo mpana wa huduma za msingi, huduma za ubingwa na ubingwa bobezi zaidi

ya huduma 1,800 ambapo mchango unaanzia Shilingi 660,000 kwa mwaka kwa mtu mmoja. Kifurushi cha **Ngorongoro Afya** kina wigo mpana wa huduma za msingi, kibingwa na ubingwa bobezi, huduma zaidi ya 440 ambapo mchango unaanzia Shilingi 240,000 kwa mwaka kwa mtu mmoja na **Toto Afya Kadi (TAK)** ni kifurushi kwa ajili ya watoto chini ya umri wa miaka 17 wanaosajiliwa mmoja mmoja au kwa makundi kupitia shule. Kwa watoto wanaosajiliwa mmoja mmoja mchango kwa mwaka ni Shilingi 150,000 ambapo wanasubiri kwa miezi 3 kabla ya kuanza kunufaika na huduma. Michango ya watoto wanosajiliwa kwa makundi kupitia shule wanazosoma ni Shilingi 50,400 kwa mtoto mmoja. Watoto wanaosajiliwa kwa makundi, uanachama wao unaanza kwa pamoja na hakuna muda wa kusubiri ili kupata huduma. Aidha, wanachama wenye vifurushi vya Najali, Wekeza na Timiza wataendelea kupata huduma hadi muda wa uanachama wao utakapokoma na kisha kujiunga na vifurushi vipya vilivyopo.

***353. Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza ufanisi kwenye Mfuko na kuhakikisha azma ya bima ya afya kwa wote inatimia, Mfuko umefanya maboresho ya mifumo ya TEHAMA katika eneo la uandikishaji wa wanachama na uchakataji wa madai ambapo **Mfumo wa uandikishaji** umeboreshwa na kumwezesha mwanachama kujiandikisha na kujihudumia bila kulazimika kufika katika Ofisi za Mfuko. Mfumo huo unapatikana kupitia kiunganishi cha https://selfservice.nhif.or.tz. na **Mfumo wa Uchakataji Madai** umeongeza ufanisi kwa

kuchakata madai kwa haraka kwa kutumia Akili Unde, hivyo kuharakisha malipo ya madai ya Watoa Huduma.

**Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA)**

***354.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) ilianzishwa kwa Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba, Sura 219. Jukumu kuu la taasisi ni kulinda afya ya jamii kwa kuhakikisha usalama, ubora na ufanisi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya maombi 1,113 ya usajili wa dawa za binadamu yalipokelewa, kati ya hayo maombi 1,005 sawa na asilimia 90 yalifanyiwa tathmini. Maombi 540 sawa na asilimia 54 ya maombi yaliyotathminiwa yaliidhinishwa na hivyo dawa husika kusajiliwa. Aidha, kulikuwa na jumla ya maombi 124 ya usajili wa dawa za mifugo ambapo maombi 114 (asilimia 92) yalifanyiwa tathmini na maombi 83 (asilimia 92) yaliidhinishwa baada ya kukidhi vigezo. Pia, kulikuwa na maombi 390 ya usajili wa maeneo ya biashara zinazohusiana na dawa na vipukusi ambapo maombi 384 sawa na asilimia 94 yalifanyiwa tathmini na 374 kati yake sawa na asilimia 97 yalikidhi vigezo vya usajili na hivyo kupewa vibali vya biashara. Vilevile, Mamlaka ilifanya ukaguzi wa viwanda na maeneo 6,708 ya biashara ya dawa na vipukusi ambapo maeneo 5,853 sawa na asilimia 87 yalisajiliwa.

***355.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha **usalama, ubora na ufanisi wa vifaa tiba na vitendanishi**, jumla ya maombi 585 ya usajili wa vifaa tiba na

vitendanishi (vifaa tiba 379 na vitendanishi 206) yaliwasilishwa ambapo maombi 527 (vifaa tiba 341 na vitendanishi 186) sawa na asilimia 90 yalifanyiwa tathmini na maombi 193 (vifaa tiba 137 na vitendanishi 56) yaliidhinishwa. Aidha, maombi yaliyofanyiwa tathmini katika kipindi hiki ni ongezeko la maombi 273 ikilinganishwa na maombi 254 yaliyofanyiwa tathmini mwaka 2024. Vilele, Mamlaka ilipokea na kutathmini maombi 531 ya usajili wa maeneo ya biashara ya vifaa tiba na vitendanishi ambapo maeneo 519 sawa na asilimia 98 yalikidhi vigezo na kusajiliwa. Maeneo yaliyotathminiwa ni ongezeko la maeneo 60 ikilinganishwa na maeneo 471 yaliyotathminiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Ongezeko hili limetokana na uhamasishaji kupitia elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kuzingatia sheria na hivyo kuongezeka kwa uelewa wa wafanyabiashara wa bidhaa husika.

***356. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 Mamlaka ilikagua maeneo 492 yanayojihusisha na biashara za vifaa tiba na vitendanishi ambapo maeneo 478 sawa na asilimia 97 yalikidhi vigezo. Idadi ya maeneo ya biashara yaliyokidhi vigezo ni ongezeko la maeneo 61 sawa na asilimia 15 ikilinganishwa na maeneo 417 yaliyokidhi vigezo mwaka 2024. Ongezeko hili limechangiwa na uhamasishaji wa wadau kukidhi matakwa ya Sheria na kuimarika kwa shughuli za udhibiti.

**357.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha udhibiti wa uingizaji nchini na usafirishaji nje ya nchi wa bidhaa zinazodhibitiwa, Mamlaka ilipokea jumla ya maombi 6,574 ya kuingiza na 648 ya kusafirisha nje ya nchi bidhaa za dawa, vipukusi, vifaa tiba na vitendanishi na kufanya jumla ya maombi yaliyopokelewa kuwa 7,222. Kati ya maombi hayo, jumla ya vibali 6,458 vilitolewa (5,853 ni vibali vya kuingiza nchini na 605 ni vibali vya kusafirisha nje ya nchi). Kati ya vibali vilivyotolewa, vibali 6,174 (5,803 vibali vya kuingiza nchini bidhaa na 371 ni vibali vya kusafirisha nje ya nchi) vilikaguliwa katika vituo vya forodha. Aidha, idadi ya vibali vilivyokaguliwa katika kipindi hiki ni ongezeko la vibali 518 ikilinganishwa na vibali 5,656 vilivyokaguliwa kipindi kama hiki mwaka wa fedha uliopita. Hii imetokana na kuongezeka kwa wakaguzi na hivyo kuimarika kwa shughuli za udhibiti katika vituo vya forodha.

**358.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 Mamlaka ilifanya tathmini ya bidhaa za dawa, vifaa, vifaa tiba na vipukusi vilivyoko sokoni ili kujiridhisha na ubora wake ambapo jumla ya sampuli 260 zilifanyiwa uchunguzi na kati ya hizo 252 sawa na asilimia 97 zilikidhi vigezo. Mafanikio hayo yanaashiria uwepo wa ubora na usalama wa bidhaa zilizopo katika soko zinazodhibitiwa na mamlaka.. Aidha, Mamlaka imeendelea kulinda mipaka ya nchi kwa kuzuia uingizwaji wa bidhaa duni, bandia na ambazo hazijasajiliwa kwa kufanya doria na ukaguzi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama.

***359. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 elimu kwa umma ilitolewa kwa makundi mbalimbali ya wananchi pamoja na kutangaza huduma za Mamlaka kupitia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufanya mihadhara 160, vipindi vya redio na runinga na matangazo mafupi ya redio na runinga. Mihadhara ya utoaji elimu ilifanyika kwa vikundi mbalimbali vya wananchi wakiwemo wazalishaji wa bidhaa, vijana, wanawake, wanafunzi na walimu kutoka Shule mbalimbali ambapo jumla ya washiriki 76,358 walifikiwa. Aidha, jumla ya wateja 9,535 walihudumiwa kupitia madawati ya huduma kwa wateja Makao Makuu na Ofisi za Kanda.

**Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA)**

***360. Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ilianzishwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Sura 177 yenye jukumu la kufanya uchunguzi wa kimaabara wa sampuli mbalimbali na vielelezo, utoaji ushahidi wa kitaalam mahakamani na usimamizi na udhibiti wa kemikali za viwandani na nyumbani.

***361. Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka imeendelea kufanya uchunguzi wa kisayansi wa maabara wa sampuli na vielelezo nchini. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 **Mamlaka ilipokea jumla ya sampuli**

**133,852 kwa ajili ya uchunguzi wa kimaabara** ambazo zinajumuisha sampuli za sumu, dawa za kulevya, mauaji, majanga, ubakaji, utambuzi wa uhalali wa wazazi kwa mtoto na jinsi tawala, vyakula, dawa za binadamu na mifugo, dawa asili, maji, kemikali, maji taka, na bidhaa nyingine za viwandani. Sampuli zilizofanyiwa uchunguzi ni 132,737 sawa na asilimia 99.3 ya sampuli zilizopokelewa na asilimia 63.7 ya lengo la mwaka la kuchunguza sampuli 208,322.

***362.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Sampuli zilizofanyiwa uchunguzi zilipungua kwa asilimia 6.3 ikilinganishwa na sampuli 141,683 zilizochunguzwa kwa kipindi kama hicho cha mwaka 2024. **Kupungua kwa sampuli zilizochunguzwa kunatokana na juhudi za Serikali za kuzuia uhalifu na biashara haramu ya madawa kulevya nchini**. Matokeo ya uchunguzi wa kimaabara wa sampuli na vielelezo umeiwezesha Wizara kupitia Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kuchangia katika kulinda afya za wananchi na mazingira pamoja na utoaji wa haki katika vyombo vya maamuzi kwa kutoa ushahidi wa kitaalam katika mahakama mbalimbali nchini.

***363.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha ubora wa matokeo ya uchunguzi yanayokubalika kitaifa na kimataifa, Mamlaka imeendelea kutekeleza viwango vya Mifumo ya Ubora ya Maabara (ISO 17025:2017) na kufanikiwa kuendelea kuwa na vyeti vya ithibati vya Maabara za Vinasaba, Chakula, Mazingira,

Toksikolojia na Maabara zilizopo ofisi ya Kanda ya Ziwa.

**364.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 Mamlaka iliendelea na usajili wa wadau 1,295 wanaojishughulisha na biashara ya kemikali sawa na asilimia 86.3 ya lengo la kusajili wadau 1,500 kwa mwaka. Wadau waliosajiliwa waliongezeka kwa asilimia 32.9 ikilinganishwa na Wadau 974 waliosajiliwa kwa kipindi kama hicho katika mwaka 2024. Lengo la kusajili wadau hawa ni kuendelea na juhudi za kulinda afya, mazingira na usalama wa nchi dhidi ya kemikali hatarishi na bashirifu zinazotumika kutengeneza dawa za kulevya au silaha za kemikali. Pia, Mamlaka ilitoa mafunzo juu ya usafirishaji salama wa Kemikali nchini kwa wadau wa kemikali 7,969 sawa na asilimia 128.5 ya lengo la kuelimisha wadau 6,200 kwa mwaka. Mafunzo hayo yamesaidia kuwapa uelewa wa namna bora ya kujilinda, kulinda watu wengine pamoja na kulinda mazingira wakati wa usafirishaji wa kemikali hizo.

**365.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imeendelea kuboresha miundombinu kwa kujenga Ofisi na Maabara pamoja na ununuzi wa vifaa na mitambo ya maabara. Katika kipindi hiki Mamlaka imeendelea kutekeleza miradi ya ujenzi wa majengo ya Ofisi katika Kanda ya Mashariki Dar es Salaam na Kanda ya Kusini Mtwara. Aidha, Mamlaka imeendelea kukamilisha

mipango ya ujenzi wa nyumba za watumishi katika mipaka ya Mtukula, Kabanga, Namanga na Holili.

**366.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha Mamlaka inakuwa na Vifaa vya kutosha kulingana na mahitaji na teknolojia ya kisasa, Wizara imeiwezesha Mamlaka kununua mitambo mikubwa minne (4) aina ya *Fourier Transform Infrared Spectrometer (FTIR), Inductively Coupled Plasma Optical Emission spectrometer (ICP-OES), Portable Gas Chromatography, Gas Chromatography* na mitambo midogo 20. Mitambo hii ya maabara imeongeza ufanisi na kasi ya utoaji wa matokeo ya uchunguzi wa kimaabara kwa wakati kwani baadhi ya mitambo imesimikwa kwenye Ofisi za Kanda kwa lengo la kusogeza huduma karibu na wananchi na hivyo kutolazimika kufuata huduma Makao Makuu.

### Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR)

**367.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 23 ya Mwaka 1979 ikiwa na jukumu la kuratibu, kudhibiti na kusimamia utekelezaji wa tafiti mbalimbali za afya hapa nchini, Taasisi imekuwa ikipokea maombi kutoka kwa watafiti mbalimbali waliopo katikaTaasisi za tafiti ndani na nje ya nchi, watalaam kutoka katika vyuo vikuu na watu wengine wenye nia ya kufanya utafiti katika eneo la afya. Taasisi kupitia Kamati ya Uratibu wa

Tafiti za Afya imekuwa ikipitia maombi yote yanayowasilishwa, baada ya kuyapitia na kujiridhisha, yale yanayokidhi vigezo hupatiwa kibali (Ethical Clearance) kwaajili ya kuanza kufanya tafiti husika. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 Taasisi ilitoa vibali 519 kati ya maombi 534 yaliyowasilishwa sawa na asilimia 97.

***368.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi imeendelea kufanya tafiti mbalimbali na kutumia matokeo ya tafiti hizo kwa ajili ya kuboresha huduma za afya nchini. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Taasisi imetekeleza miradi ya tafiti 133 kati ya 150 iliyopangwa kwa mwaka 2024/25 ambayo ni sawa na asilimia 89. Aidha, tafiti hizo zililenga magonjwa ya kuambukiza na yasiyoambukiza, uimarishaji wa mifumo ya afya na pia kuelewa viashiria vya kijamii na mazingira pamoja na Tiba Asili. Aidha, Taasisi inaendelea na **Utafiti wa kufuatilia hali ya maambukizi ya Malaria** nchini kwa kutumia mbinu za vinasaba katika mikoa 13 ya Tanzania Bara (MSMT) ulioanza mwaka 2020. Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza mabadiliko ya vimelea vya malaria ili kubaini kama mbinu tunazotumia kupambana na ugonjwa huu zinafanya kazi ipasavyo, kufuatilia ubora na uwezo wa dawa za kutibu ugonjwa wa malaria na ufanisi wa vipimo vya haraka vya kupima malaria (mRDTs). Vilevile, Taasisi imefanya **majaribio ya dawa mpya** zitakazofupisha muda wa matibabu ya kifua kikuu kutoka miezi sita (6) hadi minne (4). Matokeo ya awali ya tafiti hizi yameonesha kuwa dawa mpya zina uwezo wa

kufupisha muda wa matibabu toka miezi sita hadi miezi minne kwa wagonjwa wasio na kifua kikuu sugu.

***369. Mheshimiwa Spika,*** Taasisi imetekeleza **utafiti wa kuangalia hali ya afya baada ya matibabu ya kifua kikuu.** Matokeo yameonesha asilimia 70 ya wagonjwa wanaomaliza dawa za kifua kikuu mapafu yao yanakuwa hayafanyi kazi vizuri. Utafiti zaidi unaendelea kuangalia madhara mengineyo ya kiafya na kugundua mbinu za kuboresha afya ya mapafu baada ya kumaliza dawa za kifua kikuu ili kuboresha huduma kwa wagonjwa wenye kifua kikuu na waliomaliza tiba hiyo.

***370. Mheshimiwa Spika,*** Taasisi imeendelea kufanya **tafiti katika eneo la tiba asili na tiba mbadala** ambapo dawa nne (4) za tiba asili za NIMREGENIN kwa ajili ya kutibu tezi dume, TANGESHA kwa ajili ya kutibu seli mundu, PERSIVIN kwa ajili ya kutibu tezi dume na WARBUGISTAT kwa ajili ya kutibu magonjwa nyemelezi zinaendelea kufanyiwa uchunguzi wa usalama. Matokeo ya awali ya utafiti huu yameonesha kuwa dawa hizi ni salama katika hatua za majaribio kwa wanyama. Kuhusu Dawa ya tiba asili ya NIMREGENIN imeonekana kuwa na nguvu ya kupunguza uvimbe unaotokana na saratani na inatoa mchango mkubwa katika kupambana na magonjwa ya saratani nchini. Hivyo, Wizara imeendelea na utafiti wa kuangalia ikiwa dawa ya NIMREGENIN inaweza kusaidia tiba ya saratani za

Tezi Dume, saratani ya shingo ya kizazi na saratani ya ubongo.

371. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi imeendelea na **utafiti wa kuzuia ugonjwa wa Kisukari** ambapo tafiti hizi zimeonesha kuwa wagonjwa wenye virusi vya UKIMWI wapo katika hatari kubwa ya kupata ugonjwa wa kisukari. Aidha, Taasisi inafanya utafiti wa jaribio nasibu la awamu ya tatu ili kuangalia ikiwa matumizi ya dawa ya *Metformin* kwa watu wenye virusi vya UKIMWI wenye dalili za awali sana za kisukari yanaweza kupunguza uwezekano wa watu hawa kupata ugonjwa wa kisukari. Jaribio hilo linafanyika katika Mkoa wa Dar es Salaam. Washiriki 1,634 wameandikishwa na ufuatiliaji utafanyika kwa miaka minne (4) ili kuweza kujua ikiwa dawa hii inasaidia kukinga watu kupata ugonjwa wa kisukari.

372. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi kwa kushirikiana na wadau imeendelea na utafiti wa kupunguza magonjwa nyemelezi yanayotokana na maambukizi ya fangasi ya uti wa mgongo (Cryptococcal Meningitis). Kupitia matokeo chanya ya utafiti huu, Shirika la Afya Duniani na Wizara zimeboresha Miongozo ya Utambuzi na matibabu ya magonjwa nyemelezi ya maambukizi ya uti wa mgongo.

373. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi inaendelea kufanya **utafiti wa miaka mitano (2021 mpaka 2025)** katika Mikoa ya Mbeya na Songwe ili kutathmini kama asilimia 2 (kwa kipimo cha OV-16 ELISA) inafaa

kuwa kiwango cha juu cha maambukizi ya ugonjwa wa Usubi. Matokeo ya utafiti wa awali yanaonesha kuwa maambukizi yapo chini ya asilimia 2. Kama matokeo ya tathmini ya mwisho wa mwaka 2025 yatahakiki kiwango hicho cha maambukizi, utafiti huu utasaidia katika kufanya maamuzi ya kusitisha ugawaji wa Kingatiba katika maeneo yenye maambukizi na kuokoa pesa inayotumika katika kutekeleza afua hii.

**Utekelezaji wa Majukumu ya Bodi za Usajili na Mabaraza ya Kitaaluma**

***374.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jukumu la kusimamia utendaji wa wataalam wa Sekta ya Afya. Katika kutekeleza hilo, Mabaraza ya Kitaaluma na Bodi za Usajili wa Vituo ziliundwa kwa mujibu wa Sheria kwa ajili ya kusimamia maadili ya Kitaaluma, kusajili wataalam na kusimamia ubora wa huduma zinazotolewa na Wataalam wa Kada husika.

***375.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jumla ya Mabaraza ya Kitaaluma nane (8) na Bodi za Usajili mbili (2). Mabaraza na Bodi hizo ni pamoja na; Baraza la Madaktari Tanganyika, Baraza la Afya Mazingira, Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala, Baraza la Uuguzi na Ukunga, Baraza la Famasia, Baraza la Wataalam wa Optometria, Baraza la Wataalam wa Radiolojia, Baraza la Wataalam wa Maabara, Bodi ya Maabara Binafsi za Afya na Bodi ya Ushauri wa Hospitali Binafsi.

**376.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, Mabaraza ya Kitaaluma yalisajili jumla ya watalaam **31,315**, usajili wa Maduka ya Dawa **509**, usajili wa watarajali **3,076**, Mashauri ya Kinidhamu yaliyofanyiwa kazi ni **135**, mafunzo endelevu ya kitaaluma (CPD) yametolewa kwa watalaam **84,947** na ukaguzi wa vituo binafsi vya kutolea huduma za afya **3,483.** Aidha, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi 2025, Bodi na Mabaraza ya Kitaaluma yametekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

**Baraza la Uuuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC)**

**377.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 Jumla ya Wauguzi na Wakunga **4506** wamesajiliwa, sawa na asilimia 90 ikilinganishwa na lengo la kusajili wataalam 5,000. Kati yao, Wauguzi Wasajiliwa 4,399 (14) wataalam wa dawa ya usingizi na ganzi tiba, 107 wameorodheshwa (EN). Hili ni ongezeko la wataalam 2,327 ikilinganishwa na wataalam 2,179 waliosajiliwa katika kipindi kama hiki mwaka 2023/24. Idadi hiyo inafanya jumla ya wataalam waliosajiliwa na Baraza hadi sasa kufikia 57,200. Aidha, Wauguzi na Wakunga Watarajali 745 wamepewa usajili wa awali ikilinganishwa na watarajali 576 katika kipindi kama hicho 2023/24. Watarajali wanaendelea na mafunzo ya vitendo katika Vituo 31 zikiwemo Hospitali ya Taifa, Hospitali za Rufaa za Kanda (4) na Hospitali za Rufaa za Mikoa 27.

378. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 Baraza la Uuguzi na Ukunga lilipokea maombi manne (4) ya kuanzisha huduma binafsi za Uuguzi na Ukunga katika Mikoa ya Dar es Salaam na Tabora. Vituo vyote vilikaguliwa na kuonekana kuwa vimekidhi vigezo na hivyo kupewa vibali. Hii inafanya jumla ya *Nursing and Maternity Homes and Services* zilizosajiliwa kutoa huduma kufikia 94 kwa nchi nzima.

379. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 mpaka Machi 2025, Wauguzi na Wakunga 37,405 wamefanya mafunzo ya kujiendeleza (CPD) kwa njia tofauti tofauti ili kujengewa uwezo wa kutoa huduma, na uwezo wa kufanya tafiti mbalimbali. Idadi hii imeongezeka ikilinganishwa na Wauguzi na Wakunga 32,643 katika kipindi cha 2023/24. Ongezeko hili limetokana na elimu na uhamasishaji kuhusu umuhimu wa wataalam kujiendeleza kwa ajili ya kujengewa uwezo wa kutoa huduma bora za uuguzi na ukunga pamoja na kukidhi vigezo vya kuhuisha leseni za kutolea huduma. Aidha, jumla ya moduli 42 za mafunzo ya kujiendeleza zilipokelewa na kuhakikiwa na kupata ithibati ya Baraza. Moduli zililenga katika maeneo ya afya ya mama na mtoto, magonjwa ya mlipuko na yasiyoambukiza, chakula na lishe, kukinga na kudhibiti maambukizi (Infection Prevention and Control), huduma za upasuaji na utoaji salama wa dawa za ganzi tiba, afya ya akili,

huduma za wagonjwa mahututi (Critical Care) na mbinu za ufundishaji (Teaching Methodology).

**380. *Mheshimiwa Spika,*** Baraza limeendelea kutekeleza jukumu lake la kuhakikisha Wataalam wa kada ya Uuguzi na Ukunga wanazingatia maadili, sheria na miongozo ya taaluma yao. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya mashauri saba (7) ya tuhuma za uvunjifu wa maadili yalipokelewa. Mashauri haya yako katika hatua mbalimbali za uchunguzi na kisha hatua stahiki kuchukuliwa kulingana na Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya mwaka 2010. Aidha, idadi ya mashauri ya ukiukwaji wa maadili imepungua ikilinganishwa na mashauri 11 yaliyopokelewa katika kipindi kama hiki mwaka 2023/24.

**Baraza la Madaktari Tanganyika**

**381. *Mheshimiwa Spika,*** Baraza limeendelea kutekeleza majukumu yake ya kusimamia usajili, utendaji na maadili ya watalaam pamoja na Taaluma ya Udaktari kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu. Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 Baraza la Madaktari Tanganyika limesajili jumla ya watalaam 3,794 kati ya 6,610 waliotarajiwa kusajiliwa sawa na asilimia 57. Hii ni pungufu ya wataalam 2,414 ikilinganishwa na wataalam waliosajili katika kipindi kama hicho mwaka 2024 ambapo walisajiliwa watalaam 6,208. Hadi kufika Machi 2025, Jumla ya wataalam waliosajiliwa imefika 42,937. Aidha, jumla ya watalaam 674 wamepatiwa leseni kwa mara ya

kwanza na watalaam 5,621 wamehuisha leseni zao na hivyo kufanya jumla ya watalaam waliopatiwa Leseni na kuhuisha Leseni kufikia 18,700.

**382.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza jukumu lake la usimamizi wa mitihani ya watarajali Baraza huandaa mitihani kabla watarajali hawajaanza mafunzo na baada ya kumaliza mafunzo. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya watalaam 1,193 walifanya mtihani wa kabla ya mafunzo ya utarajali, kati yao watarajali wa Udaktari walikuwa 1,053, Udaktari wa Meno 58, Fiziotherapia 43 na wataalam wa lishe na tiba ya chakula 39. Aidha*,* katika kipindi hicho jumla ya watarajali 1,278 waliomba na kukidhi sifa za kufanya mtihani wa baada ya mafunzo ya utarajali kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025. Kati ya waliofanya mtihani, watarajali wa Udaktari ni 1,209, Udaktari wa Meno 64, Fiziotherapia wane (4) na Mtaalam wa tiba kwa vitendo mmoja (1).

**383.** ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza linatambua usajili wa mafunzo ya *fellowship* kama mbadala wa Shahada ya Uzamili (MMed). Mafunzo haya yalianza kutambulika rasmi nchini mwaka 2020 ingawa yalikuwa yakitolewa katika nchi nyingine tangu mwaka 2012. Mafunzo ya *fellowship* yamejikita zaidi katika njia ya vitendo na yanalinganishwa na Shahada ya Uzamili inayotolewa katika vyuo vikuu. Mafunzo hayo yamegawanyika katika makundi ya Watalaam wanaopata usajili wa shahada ya kwanza

ya uzamili na kutambuliwa kama Bingwa na Watalaam wanaopata Shahada ya pili ya Uzamili na kutambuliwa Bingwa bobezi. Aidha, Baraza limeandaa miongozo tisa ya kupima na kutathmini sifa za ziada kwa njia ya *fellowship* ili kuhakikisha ubora na ulinganifu wa mafunzo hayo. Hadi Machi 2025, jumla ya watalaam 59 wamekamilisha mafunzo ya *fellowship* na kutambuliwa kuwa na sifa za ziada katika taaluma zao.

***384.*** ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya watoa mafunzo endelevu 82 walisajiliwa ikilinganishwa na kipindi kama hiki 2024/25 ambapo watoa mafunzo 37 walisajiliwa. Watoa mafunzo hao wanahusisha Hospitali Maalum, Hospitali za Rufaa za Kanda, Hospitali za Rufaa za Mikoa, Hospitali za wilaya, Vituo vya afya, Zahanati, Vyuo Vikuu, Vyuo vya Kati, Taasisi za Serikali, Taasisi zisizo za Serikali na Makampuni. Aidha, jumla ya kozi 515 zilipewa ithibati ikilinganishwa na kipindi kama hiki 2024/25 ambapo kozi za mafunzo endelevu 292 zilipatiwa ithibati. Vilevile, jumla ya watalaam 19,600 walifanya mafunzo mbalimbali ya kitaaluma ikilinganishwa na kipindi kama hiki 2024/25 ambapo jumla ya watalaam 16,116 walifanya mafunzo endelevu ya kitaaluma.

***385.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 Baraza lilifuatilia ukiukwaji wa maadili ya kitaaluma ambapo jumla ya malalamiko 22 yalipokelewa. Kati ya hayo Malalamiko 19 yalichunguzwa na Kamati ya Uchunguzi wa Mashauri ya Kitaaluma na mashauri 10 yalisikilizwa na Baraza

dhidi ya wataalam waliotuhumiwa kwenda kinyume na maadili ya taaluma zao. Maamuzi yaliyotolewa ni pamoja na walalamikiwa wawili (2) kupewa onyo, watano (5) kufungiwa leseni za kutoa huduma kwa muda wa miezi sita (6) na kuelekezwa kwenda kwenye mafunzo ya lazima ya weledi kwa kipindi cha miezi mitatu (3) wakiwa chini ya uangalizi kwa kipindi cha miaka miwili (2). Mlalamikiwa mmoja (1) amefungiwa Leseni kwa kipindi cha miezi tisa (9) na mmoja (1) kwa kipindi cha miaka miwili (2). Walalamikiwa wanne (4) hawakukutwa na hatia yoyote na kuachiwa huru.

**Baraza la Famasi**

**386.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Baraza limesajili jumla ya wafamasia 148, fundi sanifu dawa 820 wameandikishwa na fundi sanifu dawa wasaidizi 75 wameorodheshwa na kufikisha jumla ya wataalam 14,322. Kati yao, wafamasia ni 3,937; fundi sanifu dawa ni 9,252; fundi sanifu dawa wasaidizi ni 1,133 wanaotambuliwa. Aidha, asilimia 70 ya watalaam wamehuisha na kuwa na leseni hai za utendaji. Katika kuhakikisha kada inatoa watoa huduma wenye vigezo, Baraza limefanikiwa kusimamia jumla ya watarajali 456 katika vituo 36 vya kutolea huduma za afya.

**387.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki, maduka ya dawa 509 (rejareja 412, Jumla 35 na jumla na

rejareja 53 na maghala 09) yamesajiliwa kutoa huduma ya dawa nchini, hivyo kufanya jumla ya maduka ya biashara ya Famasi kuwa 3,345. Vilevile, jumla ya watalaam 10,026 walishiriki mafunzo endelevu (CPD) katika maeneo mbalimbali ambapo Wafamasia 3,072, Fundi Sanifu Dawa 6,506 na Fundi Sanifu Dawa Wasaidizi 448.

***388. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya mashauri ya kinidhamu 99 yalipokelewa, kati ya hayo malalamiko 25 yanaendelea na hatua ya uchunguzi. Malalamiko 74 uchunguzi wake ulikamilika na maamuzi yaliyotolewa ni pamoja na walalamikiwa 31 kupewa onyo, tisa (9) walifungiwa Leseni za kutoa huduma katika maduka ya famasi kwa kipindi cha miezi 12, mmoja (1) alitakiwa kulipa fidia ya hasara aliyosababisha, mmoja (1) aliongezewa muda wa mafunzo kwa vitendo na watalaam 31 hawakukutwa na hatia.

**Baraza la Wataalam wa Radiolojia**

***389. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Baraza lilipitia maombi ya usajili wa wataalam wa Radiolojia kwa kada mbalimbali. Aidha, Wataalam waliokidhi vigezo walisajiliwa kulingana na usajili walioomba. Usajili wa matazamio (wataalam 176), usajili kamili (161), usajili wa muda (Mtaalam mmoja), uandikishaji (5) na uorodheshaji (5) na kufanya idadi ya wataalam waliosajiliwa kwa kipindi hicho kufikia 344. Idadi hiyo inapelekea jumla ya wataalam wote waliosajiliwa na Baraza tangu kuanza

usajili mwaka 2011 kufikia 1,840. Vilevile, katika kipindi hiki jumla ya wataalam 810 kati ya wataalam 1,400 walihuisha leseni zao sawa na asilimia 58 ya waliotegemewa kuhuisha leseni kwa mwaka 2023/24.

***390. Mheshimiwa Spika,*** Baraza limeendelea kusimamia watarajali wa kada za Radiolojia nchini ambapo jumla ya watarajali 49 walipewa mafunzo juu ya sheria, kanuni, miiko na maadili na kupangiwa vituo vya utarajali. Aidha, mafunzo juu ya matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa usajili (HPRS) yameendelea kutolewa kwa wataalam wa radiolojia nchini. Jumla ya wataalam 1,450 kati ya 1,840 sawa na asilimia 78 wameweza kutumia mfumo kujisajili na kuhuisha leseni. Pia, jumla ya wahitimu 49 wa ngazi ya shahada wameweza kuchagua vituo vya utarajali kwa njia ya mfumo huo.

***391. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 Baraza lilitoa mafunzo kuhusu sheria, kanuni, miiko na maadili kwa wahitimu 307 wa shahada, na stashahada katika fani za Radiolojia nchini. Aidha, Baraza lilishiriki kuandaa Kongamano la Siku ya Radiografia nchini lililofanyika Arusha na Dar es Salaam ambapo jumla ya Wataalam 750 walipatiwa mafunzo mbalimbali.

***392. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 Baraza lilipokea jumla ya mashauri matatu (3) ya uvunjifu wa miiko na maadili ya

kitaaluma. Mashauri yote yapo katika hatua za uchunguzi, yatakapokamilika hatua stahiki zitachukuliwa kulingana na sheria, kanuni, miongozo ya miiko na maadili ya taaluma.

**Baraza la Wataalam wa Macho (Optometria)**

***393.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Baraza limesajili jumla ya wataalam 40 kwa usajili wa kudumu na kufanya jumla ya wataalam waliosajiliwa usajili wa kudumu kufikia 453.

***394.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya wataalam 420 walipatiwa elimu kuhusu mafunzo endelevu ya kitaaluma (CPD) ya fani ya Optometria katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, Baraza lilifanikiwa kufanya kikao na wataalam wa Optometria waliopewa usajili wa kudumu na usajili wa awali mkoani Dodoma ambapo jumla ya wataalam 80 walikumbushwa juu ya kuzingatia maadili, kutoa huduma bora, Sheria ya Optometria, matumizi ya Mfumo wa usajili wa wataalam (HPRS) ili kuongeza ufanisi na kuboresha huduma za macho. Katika kuhakikisha kada inatoa watoa huduma wenye vigezo, Baraza limefanikiwa kusimamia jumla ya watarajali watano (5) katika vituo vya kutolea huduma.

### Baraza la Wataalam wa Maabara ya Afya

**395.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya wataalam 1,221 wapya wa maabara wamesajiliwa kwa usajili wa kudumu na kuandikishwa, hivyo kufanya jumla ya wataalam waliosajiliwa na Baraza kufikia 16,655. Aidha, katika kipindi hiki, wataalam 5,981 wamehuisha leseni zao na katika kipindi cha mwaka 2024/25, wataalam 6,862 wamehuisha leseni zao. Hivyo kufanya Wataalam wenye leseni hai kufika 9,596 hadi Machi 2025.

**396.** ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza lilisimamia mitihani ya usajili kwa ngazi zote (Astashahada, Stashahada na Shahada) ambapo jumla ya maombi 1,299 yalipokelewa kati yao wataalam wa Astashahada walikuwa 108; Stashahada 875 na Shahada 316. Ufaulu wa jumla ulikuwa asilimia 60 ikilinganishwa na ufaulu wa asilimia 54 mwaka 2023/24. Baraza limeongeza kituo kimoja (1) cha mafunzo ya utarajali cha Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini – Mtwara na kufanya jumla ya vituo vinavyotambuliwa na Baraza kuwa 25. Vilevile, Baraza lilitoa mafunzo endelevu (CPD) kwa wataalam wa Maabara 10,954.

**397.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Baraza limefanya ukaguzi katika vituo 214 vya Maabara pamoja na vyuo katika Mikoa ya Dodoma, Mtwara, Lindi, Dar es Salaam, Manyara, Mwanza, Arusha, Iringa, Kagera, Mara na Singida.

Lengo la ukaguzi lilikuwa ni kuangalia viwango vya ubora katika utoaji wa huduma kwenye vituo na utoaji wa mafunzo kwenye vyuo. Zoezi hili lilienda sambamba na utoaji wa elimu kuhusiana na Sheria, Kanuni na mwongozo wa mafunzo endelevu ya taaluma. Aidha, kuna ongezeko la uhuishaji wa leseni na kusoma mafunzo endelevu ya taaluma (CPD) kwa wataalam 1,558 waliopata alama za CPD Mwaka 2023/24 hadi wataalam 10,954 kufikia Machi, 2025. Katika kipindi hiki, Baraza lilifuatilia ukiukwaji wa maadili ambapo jumla ya mashauri manne (4) yalifunguliwa, kati ya hayo mashauri matatu (3) yanaendelea na uchunguzi na shauri moja (1) limefungwa.

***398. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Baraza limesajili watarajali 398 ambao wamepangwa katika vituo vya mafunzo 25. Watarajali 376 walianza mafunzo Mwezi Novemba, 2024 na Watarajali 22 walianza mafunzo Mwezi Aprili, 2025.

**Baraza la Wataalam wa Afya Mazingira**

***399. Mheshimiwa Spika*** katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, idadi ya wataalam wapya waliosajiliwa na Baraza la Afya Mazingira ni 448 ikilinganishwa na wataalam 382 waliosajiliwa katika kipindi kama hiki mwaka 2024 na hivyo kufanya jumla ya wataalam waliosajiliwa kufikia 4,997. Kati ya wataalam 4,997 waliosajiliwa, wenye usajili kamili ni

2,057, Usajili wa kuorodheshwa 2,215, Usajili wa kuandikishwa 581 na Usajili wa Muda 144.

**400.** ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza limeratibu mafunzo ya utarajali ambapo kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya watarajali 145 wanaendelea na mafunzo katika mikoa 25 ya Tanzania Bara na Vyuo Sita (6) vinavyotoa taaluma ya Afya Mazingira Ngazi ya Stashahada na Watarajali 164 wamehitimu mafunzo hayo mwezi Oktoba, 2024 ikiwa ni ongezeko la wahitimu 55 kutoka mwaka 2024. Aidha, Baraza limeendelea kufanya ufuatiliaji wa usajili, uhuishaji wa leseni na watarajali katika mikoa yote ya Tanzania Bara.

**401.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Baraza limeendelea kutekeleza jukumu lake la kuhakikisha Wataalam wa kada ya Afya Mazingira wanazingatia maadili, sheria na miongozo ya taaluma yao. Katika kipindi hicho, jumla ya wataalam 670 wa shahada na stashahada ya Afya Mazingira walipatiwa mafunzo maalum kuhusu sheria, kanuni, miiko na maadili ya taaluma. Aidha, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 hapakuwa na taaarifa za uvunjifu wa maadili iliyowasilishwa katika Ofisi ya Msajili.

### Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala

402. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya wataalam (waganga na wasaidizi wa tiba asili na tiba mbadala na wauza dawa za asili) 6,713 wamesajiliwa, sawa na asilimia 149 ya lengo la kusajili wataalam 4,500 kwa mwaka, na kufanya jumla ya wataalam waliosajiliwa na Baraza hadi sasa kufikia 59,878. Kati ya wataalam 6,358 waliosajiliwa, wataalam 4,880 walipatiwa usajili wa awali na 1,468 usajili wa kudumu. Aidha, Baraza limesajili vituo vya tiba asili 273 na kufanya jumla ya vituo kuwa 2,108 hadi Machi 2025.

403. ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza lilitekeleza zoezi la ukaguzi wa maduka ya kuuza dawa za asili, vituo vya kutolea huduma katika mikoa ya Mwanza, Kilimanjaro, Arusha na Dodoma. Dhumuni kuu lilikuwa ni kukagua ubora wa huduma zinazotolewa kwa wananchi na kutoa mwongozo wa uboreshaji wa huduma hizo. Ukaguzi huu ulifanyika katika maduka 165 ya kuuza dawa za asili na vituo 57 vya kutolea huduma. Aidha, wauzaji wa maduka ya dawa asili pamoja na maduka ambayo hayakuwa na leseni walielimishwa na kuwasajili papo hapo.

404. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 Baraza lilifuatilia ukiukwaji wa maadili ya kitaaluma ambapo jumla ya malalamiko manne (4) yalipokelewa. Kati ya hayo uchunguzi wa malalamiko mawili (2) umekamilika na hatua stahiki zimechukuliwa.

## Bodi ya Maabara Binafsi za Afya

**405.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, idadi ya vituo vilivyosajiliwa na Bodi ya Maabara Binafsi za Afya ni 317 ikilinganishwa na vituo 238 katika kipindi kama hicho mwaka 2024 sawa na ongezeko la vituo 79, hivyo kufanya jumla ya Maabara Binafsi nchini kufikia 4,353. Kati ya hizo, maabara zinazojitegemea ni 1,555 na zilizojishikiza kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ni 2,798.

**406.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi imefanikiwa kufanya ufuatiliaji wa huduma na kutoa elimu ya sheria, kanuni na miongozo mbalimbali inayotumika katika usimamizi na uendeshaji wa huduma zitolewazo kwenye maabara binafsi za afya 844 katika mikoa nane (8) ambayo ni Morogoro, Mbeya, Katavi, Rukwa, Songwe, Geita, Mwanza na Arusha. Kati ya hizo, maabara 676 sawa na asilimia 80 zilikidhi vigezo.

## Bodi ya Ushauri wa Hospitali Binafsi

**407.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi, 2025 Bodi ilikuwa imesajili jumla ya vituo vya kutolea huduma 3,483 kati ya vituo hivyo vituo vinavyofanya kazi ni 3,328, vilivyofungwa moja kwa moja vituo 36 na vituo 119 vimefungwa kwa muda kutokana na sababu mbalimbali. Aidha, katika vituo vinavyofanya kazi Hospitali ni 224, vituo vya afya 309, Zahanati 1,954, Kliniki 402, *Polyclinics* 395, Kliniki za kuchuja damu 22 na vituo vya uchunguzi 22.

**408.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 jumla ya maombi 339 ya vituo binafsi yaliwasilishwa, kati ya hayo maombi 204 yalikuwa maombi ya vituo vipya, maombi 49 yalikuwa ya vituo vinavyoomba kupandishwa daraja na maombi mengineyo vituo 86. Kati ya maombi hayo, vituo 262 vilisajiliwa (Kliniki 23, *Polyclinics* 38, Hospitali ngazi ya Mkoa 10, Hospitali ngazi ya Kanda tatu (3), ngazi ya Wilaya tisa (9), vituo vya afya 19 na Zahanati 159 na kituo cha Uchunguzi kimoja (1), sawa na asilimia 77 ya maombi yote.

**409.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi iliendelea na zoezi la ukaguzi wa vituo binafsi vya kutolea huduma za afya katika mikoa ya Mwanza na Dar es Salaam ambapo jumla ya vituo 523 vilikaguliwa ikilinganishwa na vituo 272 vilivyokaguliwa katika kipindi kama hiki mwaka 2024 ikiwa ni ongezeko la vituo 251. Kati ya vituo hivyo, vituo 495 sawa na asilimia 95 vilikidhi vigezo vya uendeshaji wa vituo.

## SEHEMU YA V: VIPAUMBELE VYA WIZARA YA AFYA NA BAJETI YA MAPATO, MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/26.

**410.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendeleza mapinduzi ya Sekta ya Afya yaliyofanywa na Serikali ya Awamu ya sita, Wizara imeainisha Vipaumbele kumi (10) vitakavyotekelezwa kwa mwaka 2025/26 ambavyo ni:-

i. Kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa ya kuambukiza yakiwemo magonjwa ya milipuko, magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele, magonjwa yasiyoambukiza na huduma za Lishe;
ii. Kuimarisha upatikanaji na ubora wa huduma za afya zinazotolewa katika ngazi zote kuanzia Zahanati hadi Taifa;
iii. Kuimarisha mifumo ya ugharamiaji wa huduma za afya nchini ikiwa ni pamoja na kuendelea na utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote;
iv. Kuendelea kufanya tafiti na kuhimiza matumizi ya matokeo ya tafiti hizo kwa maeneo ya kimkakati;
v. Kuimarisha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto ili kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na watoto wachanga;
vi. Kuimarisha upatikanaji na uendelezaji wa wataalam katika Sekta ya Afya kwa fani za kati, ubingwa na ubingwa bobezi;
vii. Kuimarisha huduma za matibabu ya

ubingwa na ubingwa bobezi pamoja na kuimarisha tiba utalii nchini;

viii. Kuendeleza na kusimamia afua za Tiba Asili na Tiba Mbadala;

ix. Kuimarisha upatikanaji wa huduma za tiba dhidi ya magonjwa ya kuambukiza, magonjwa yasiyoambukiza na magonjwa ya mlipuko; na

x. Kuimarisha huduma za afya ya akili, huduma za utengamao hususan kwa watoto, wazee na watu wenye ulemavu.

***411.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Kiasi cha **Shilingi Trilioni moja, Bilioni mia sita kumi na nane, milioni mia moja tisini na moja, laki mbili na elfu thelathini na tano (1,618,191,235,000.00)** kimekadiriwa kutumika kutekeleza vipaumbele hivyo na afua mbalimbali kama ifuatavyo: -

**i. Kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa ya kuambukiza yakiwemo magonjwa ya milipuko, magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele, magonjwa yasiyoambukiza na huduma za Lishe, ambapo kiasi cha Shilingi Bilioni 166.01 zitatumika kutekeleza afua zifuatazo:**

a. Kuendelea kuimarisha usimamizi katika Mikoa 20 na kuanzisha vituo vya Operesheni ya Matukio ya Dharura za Afya (PHEOCs) katika mikoa sita (6) ya Simiyu, Geita, Pwani**, Njombe, Singida** na Shinyanga kwa ajili ya kuratibu, kujiandaa, kukabiliana na dharura za afya ikiwemo

milipuko ya magonjwa;

b. Kuendelea kutoa elimu kwa umma na kuhamasisha jamii kuhusu ulaji unaofaa, kufanya mazoezi, kuzingatia lishe bora kwa watu wa rika zote, matumizi sahihi ya sukari, chumvi, mafuta, athari zitokanazo na matumizi ya tumbaku, pombe ili kuzuia na kukabiliana na magonjwa yasiyoambukiza;
c. Kukamilisha uanzishwaji wa Programu ya Taifa wa Lishe nchini.
d. Kuendelea kuimarisha huduma za afya mipakani kwa kujenga Miundombinu ya kuwatenga wahisiwa wa magonjwa ya kuambukiza katika mipaka 16 na ununuzi wa magari matano (5), Ambulance boat tatu (3) na vipima joto tembezi (Walkthrough thermoscanners) 28.
e. Kuendelea kutekeleza Programu ya Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii Serikali kwa kuwajengea uwezo Wahudumu 28,000 kutoka Mikoa.
f. Kuendelea kuimarisha huduma za chanjo kwa kuwafikia Watoto wenye umri chini ya miaka mitano, wasichana na mama wajawazito.

**ii. Kuimarisha upatikanaji na ubora wa huduma za afya zinazotolewa katika ngazi zote kuanzia Zahanati hadi Taifa, ambapo kiasi cha Shilingi Bilioni 309.51 kimetengwa kutekeleza afua zifuatazo, -**

a. Kuimarisha matumizi ya TEHAMA ikiwemo

matumizi ya akili mnemba (Artificial Intelligence) ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma na kuunganisha mifumo iweze kusomana, kubadilishana taarifa na kupunguza gharama za huduma za afya nchini;

b. Kuhuisha na kuzindua Sera ya Afya pamoja na Mkataba wa Huduma kwa Mteja (Client Service Charter);

c. Kuanzisha Taasisi ya Taifa ya Afya ya Jamii (National Public Health Institute);

d. Kuimarisha Hospitali ya Benjamin Mkapa ili kuwa na hadhi ya Hospitali ya Taifa;

e. Kuanzisha kituo cha umahiri cha Afrika Mashariki cha matibabu ya magonjwa ya damu na uloto katika hospitali ya Benjamin Mkapa;

f. Kuanzisha kituo cha kimataifa cha upandikizaji figo katika Hospitali ya Benjamin Mkapa. Kituo hicho kitakuwa ni kituo kikubwa na kitaongoza katika ukanda wa kusini mwa jangwa la sahara;

g. Kuzitangaza na kuzipa hadhi ya kuwa taasisi Hospitali za Afya ya Akili Mirembe na Hospitali ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto na Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya;

h. Kuimarisha ufuatiliaji, uratibu na udhibiti wa usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa (Antimicrobial Resistance) na kusimamia uingizaji na matumizi sahihi ya Antibiotics nchini;

i. Kuongeza kasi ya matumizi ya Tiba Mtandao (Telemedicine) ili kusaidia utoaji

wa huduma za ushauri, ubingwa na ubingwa bobezi kwa maeneo yasiyo na wataalam hao;

j. Kuweka mazingira wezeshi ya viwanda vya ndani vya kuzalisha bidhaa za afya ili kuwezesha upatikanaji wa bidhaa hizo kwa urahisi na unafuu wakati wote;

k. Kuendelea kuimarisha upatikanaji wa bidhaa za afya (dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi) kwa kuboresha mifumo ya maoteo, ununuzi, utunzaji na usambazaji wa dawa na bidhaa nyingine katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya;

l. Kuendelea kuimarisha utekelezaji wa afua za kukabiliana na usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa (Anti Microbial Resistance);

m. Kuwezesha Hospitali ya Taifa, Hospitali Maalum, Hospitali za Rufaa za Kanda na Hospitali za Rufaa za Mikoa kujiunga katika mchakato wa kupata ithibati ya kimataifa hivyo kuongeza viwango vya ubora wa huduma na kukuza utalii wa tiba nchini;

n. Kuongeza idadi ya Hospitali za Rufaa za Mikoa zenye uwezo wa kutoa huduma za ubingwa muhimu nane (8) kutoka hospitali moja (1) hadi kufikia tisa (9). Huduma hizo ni Magonjwa ya ndani, Magonjwa ya watoto, Magonjwa ya wanawake na afya ya uzazi, huduma za upasuaji, huduma za dawa za usingizi na ganzi, upasuaji wa mifupa, radiolojia na Magonjwa ya dharura; na

o. Kuwezesha upatikanaji wa huduma za mama mwambata na matumizi ya chati ya

uchungu iliyoboreshwa katika ngazi zote za kutolea huduma za kujifungua kwa akina mama wajawazito.

iii. **Kuimarisha mifumo ya ugharamiaji wa huduma za afya nchini ikiwa ni pamoja na kuendelea na utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, ambapo kiasi cha Shilingi Bilioni 49.80 kimetengwa kutekeleza afua zifuatazo: -**

a. Kutenga fedha kwa ajili ya kukabiliana na mabadiliko ya Sera yasiyotarajiwa kutoka kwa nchi za magharibi; na
b. Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote nchini kwa kuanza kutoa kadi za Bima ya Afya kwa makundi mbalimbali.

iv. **Kuendelea kufanya tafiti na kuhimiza matumizi ya matokeo ya tafiti hizo kwa maeneo ya kimkakati, ambapo kiasi cha Shilingi Bilioni 4.46 kimetengwa kutekeleza afua zifuatazo: -**

a. Magonjwa yasiyoambukiza ikiwemo Saratani na afya ya akili;
b. Magonjwa ya kuambukiza ikiwa ni pamoja na magonjwa ya milipuko;
c. Usugu wa vimelea dhidi ya dawa; na
d. Dawa za tiba asili na tiba mbadala.

v. **Kuimarisha huduma za afya ya uzazi,**

**mama na mtoto ili kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na watoto wachanga, ambapo kiasi cha Shilingi Bilioni 76.57 kimetengwa kutekeleza afua zifuatazo: -**

a. Kuendelea na ununuzi na usambazaji wa dawa muhimu za uzazi salama (Magnesium sulphate, Oxytocin, FeFo na SP) pamoja na dawa za uzazi wa mpango, dawa kinga za minyoo, dawa za kuongeza damu, dawa za Malaria, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi;
b. Kuimarisha upatikanaji wa dawa ya vidonge myenyuko vya amoxycillin, ORS/zinc kwa ajili ya kutibu nimonia na kuhara kwa watoto, dawa za Surfactant na vifaa vya kusaidia upumuaji (CPAP) ili kusaidia changamoto za upumuaji kwa watoto waliozaliwa kabla ya wakati na waliozaliwa na uzito pungufu; na
c. Kuendelea na ununuzi wa vifaa tiba vya wodi 100 maalum za watoto wachanga wagonjwa (Neonatal Care Unit - NCU) na waliozaliwa na uzito pungufu.

vi. **Kuimarisha upatikanaji na uendelezaji wa wataalam katika Sekta ya Afya kwa fani za kati, ubingwa na ubingwa bobezi, ambapo kiasi cha Shilingi Bilioni 80.38 kimetengwa kutekeleza afua zifuatazo: -**

a. Kuendelea kutoa ufadhili wa mafunzo ndani na nje ya nchi kwa utaratibu wa Seti kwa wataalam wa ngazi ya ubingwa na ubingwa

bobezi na kufadhili mafunzo ya kada za kati za kimkakati;

b. Kuendelea kutoa mafunzo ya afya ya kada za kati katika vyuo vya afya vya umma; na
c. Kusimamia ubora wa mafunzo katika vyuo vya umma na binafsi.

vii. **Kuimarisha huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi pamoja na kuimarisha tiba utalii nchini, ili kutekeleza afua hizi kiasi cha Shilingi Bilioni 123.93 kimetengwa: -**

a. Kuendelea kutoa huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi katika Hospitali ya Taifa, Hospitali maalum, Hospitali za Rufaa za Kanda na Hospitali za Rufaa za Mikoa pamoja na kuanzisha na kuimarisha huduma mpya kulingana na mahitaji zikiwemo**:**
   - Upandikizaji wa ini katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili kampasi ya Upanga na Kuanzisha huduma bobezi za mfumo wa mkojo na uzazi kwa wanaume (Uro-andrology) katika Hospitali ya Taifa Muhimbili kampasi ya Mloganzila.
   - Kuanzisha upasuaji na ubadilishaji wa mabega na viwiko (Shoulder and Elbow Replacement) katika Taasisi ya Mifupa Muhimbili.
   - Kuendelea kutoa huduma ya upasuaji wa ubongo, uti wa mgongo, nyonga na magoti kwa kutumia mfumo wa

akili mnemba katika Taasisi ya Mifupa Muhimbili MOI.

- Kuanzisha huduma ya matibabu ya wagonjwa waliopata kiharusi na mishipa ya damu ndani ya ubongo bila kufungua fuvu (Interventional Neuro-radiology) katika Hospitali ya Benjamin Mkapa.
- Kuanzisha huduma sita za kibingwa kwa fani za Radiolojia, Usingizi, Ngozi, Macho, Magonjwa ya akili na Magonjwa ya Damu Katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Maweni Kigoma.
- Kuanzisha huduma za kibingwa za upasuaji wa taya na uso (Maxillofacial Surgery) katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Iringa
- Kuanzisha huduma za kibingwa za masikio, pua na koo katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Kitete (Tabora).

b. Kuendelea na hatua za awali za utekelezaji wa mradi wa maboresho makubwa ya Hospitali ya Taifa Muhimbili;
c. Kuanzisha kiwanda cha kuzalisha viungo tiba na viungo saidizi (Prostheses Manufacturing Plant) katika Hospitali ya Kanda KCMC. na
d. Kuendeleza na kuimarisha huduma za mkoba za kimkakati za ubingwa na ubingwa bobezi ndani na nje ya nchi (International Medical Camps).

**viii. Kuendeleza na kusimamia afua za Tiba**

**Asili na Tiba Mbadala, ambapo kiasi cha Shilingi milioni 937.29 kimetengwa kutekeleza afua zifuatazo:-**

a. Kuongeza Hospitali zinazotoa huduma jumuishi za Tiba Asili kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa 14 hadi 21; na
b. Kuendeleza huduma za Tiba Asili kwa kufanya tafiti, kuongeza na kuendeleza mashamba ya miti dawa kwa kila kanda ili kuhamasisha uzalishaji endelevu wa dawa za tiba asili;

ix. **Kuimarisha upatikanaji wa huduma za tiba dhidi ya magonjwa ya kuambukiza, magonjwa yasiyoambukiza na magonjwa ya mlipuko, ambapo kiasi cha Shilingi Bilioni 173.94 kimetengwa kutekeleza afua zifuatazo:-**

a. Kuendelea kutekeleza afua za udhibiti na kutokomeza Malaria kwa kuua mazalia ya mbu, kuimarisha uzalishaji wa viuadudu katika viwanda vya ndani ikiwemo kiwanda cha Viuadudu Kibaha, kununua na kusambaza vyandarua, vitendanishi na dawa za Malaria.
b. Kuendelea kutekeleza afua za kudhibiti na kutokomeza Kifua Kikuu na Ukoma, UKIMWI, Homa ya Ini na magonjwa ya ngono kwa kuimarisha uwezo wa utambuzi na tiba ya magonjwa hayo kwa kununua vifaa, vifaa tiba, vitendanishi na dawa;

c. Kufufua kiwanda cha *Tanzania Pharmacetical Industry* (TPI) kilichopo Arusha kuanza kuzalisha ARV.

**x. Kuimarisha huduma za afya ya akili, huduma za utengamao hususan kwa watoto, wazee na watu wenye ulemavu, ambapo kiasi cha Shilingi Bilioni 6.61 kimetengwa kutekeleza afua zifuatazo:-**

a. Kuimarisha utambuzi wa mapema wa watoto wenye ulemavu kwa kununua vifaa vya uchunguzi wa usikivu na macho kwa Hospitali za Rufaa za Mikoa 14 na Hospitali za Kanda tano (5) na kuimarisha huduma za utengamao katika Hospitali za Halmashauri 50.
b. Kuongeza idadi ya Hospitali za Rufaa za Mikoa zinazotoa huduma tatu za utengamao za Viungo tiba na viungo Saidizi (Prosthetics and Orthotics), Fiziotherapia (Physiotherapy), Tiba kwa Vitendo (Occupational Therapy), kutoka nane (8) hadi 18;
c. Kuendelea na maandalizi ya uanzishwaji wa kituo cha umahiri cha huduma za utengamao katika Mkoa wa Tabora; na
d. Kuendelea kuhamasisha uanzishwaji wa Klabu za Afya za Wazee (Healthy Ageing Clubs) katika ngazi ya Halmashauri ili kuongeza idadi kutoka 14 hadi 30;

## SEHEMU YA VI: SHUKRANI

***412.*** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee natoa shukran zangu kwa Wakurugenzi na Wakuu wa Taasisi zote zilizo chini ya Wizara ambao ni **Bw. Mavere Ali Tukai (MSD), Dkt. Irene Charles Isaka (NHIF), Bw. Adam Mitangu Fimbo (TMDA), Prof. Said Shebe Aboud (NIMR), Dkt. Fidelice Mbaruku Mafumiko (Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali)**. Pia, nichukue fursa hii kuwashukuru Wakurugenzi wa Hospitali ya Taifa, Maalum na Kanda ambao ni **Prof. Mohamed Yakub Janabi** (Hospitali ya Taifa Muhimbili), **Mhe. Balozi Dkt. Mpoki Ulisubisya** (Taasisi ya Mifupa MOI), **Dkt. Peter Richard Kisenge** (Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete), **Dkt. Diwani Bakari Msemo,** (Taasisi ya Saratani ya Ocean Road), **Dkt. Leonard Maduhu Subi** (Hospitali ya Kibong'oto), **Dkt. Paul Sarea Lawala** (Hospitali ya Mirembe) na Wakurugenzi wa Hospitali za Rufaa za Kanda **Dkt. Godlove Fred Mbwanji** (Hospitali ya Rufaa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya), **Prof. Abel Nkono Makubi** (Hospitali ya Benjamin Mkapa), **Dkt. Brian Caesar Mawalla** (Hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato), **Dkt. Herbert George Msigati** (Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mtwara), **Dkt. Bahati Mgeni Wajanga** (Hospitali ya Rufaa ya Kanda Bugando), **Prof. Gileard Masenga** (Hospitali ya Rufaa ya Kanda KCMC) na **Bi. Brenda Kinemo Msangi** (Hospitali ya Rufaa ya Kanda CCBRT).

